

**JINSI UKABILA NA MIELEKEO YA WANAFUNZI HUATHIRI UTEUZI NA
MATUMIZI YA LUGHA VYUONI: MFANO WA CHUO KIKUU CHA EGERTON**

**GACHEIYA, RAPHAEL MWAURA
AM12/1102/03**

EGERTON UNIVERSITY IRRAK

**Tasnifu hii imewasilishwa kwa shule ya waliofuzu kutimiza baadhi ya mahitaji ya
shahada ya uzamili katika Kiswahili ya Chuo Kikuu cha Egerton.**

Chuo kikuu cha Egerton

MEI 2007.



Eger241279

2008/73022 X

IKIRARI NA IDHINI

IKIRARI

Tasnifu hii ni kazi yangu binafsi na haijatolewa kutahiniwa kwa mahitaji ya shahada yoyote katika chuo kikuu chochote.

Gacheiya, Raphael Mwaura

Sahihi  Tarehe 04.05.07

IDHINI

Tasnifu hii inawasilishwa kutahiniwa ili kutimiza baadhi ya mahitaji ya shahada ya uzamili katika Kiswahili kwa idhini yetu kama wasimamizi walioteuliwa rasmi na chuo kikuu.

Dkt. Furaha Tchai

Sahihi  Tarehe 08-05-07

Dkt. Onyango, J. Ogolla

Sahihi  Tarehe 16/05/07

Hatilinzi

Haki zote zimehifadhiwa. Hairuhusiwi kamwe kuiga, kutafsiri, kunakili au kuhifadhi tasnifu hii kwa njia au mfumo wowote ule pasina idhini ya mwandishi au / na Chuo Kikuu cha Egerton.

TABARUKU

**Kwa wazazi wangu:
Stephen Gacheiya Mwaura**

Na

Ann Njeri Gacheiya

**“Mliniaminia fedha zenu bila kujua hatima ya mradi wangu. Mmenipa amali ya
kukabiliana na utesi wa maisha daima”.**

Ahsanteni sana kwa kunilea na kunisomesha.

SHUKRANI

Jifya moja haliinjiki chungu; bila shaka kuhitimisha tasnifu hii nimepata muawana kutokana na watu kadhaa ambao ninawia shukrani. Nawashukuru wahadhiri wasimamizi wangu Dkt. Furaha Tchai na Dkt. James Onyango Ogolla. Hawa, walikuwa maridhia kunielekeza na kuniongoza katika kozi ya uzamili. Licha ya kazi zao nyingi, walisoma kazi yangu pasina kuchoka na hawakukawia kunipa mapendekezo ambayo yalinisaidia sana. Bila mwongozo wao, tasnifu hii haingefikia ufanisi huu. Namshukuru aliyekuwa Mkuu wa Idara ya Lugha na Isimu Dk. C. Kitetu na mhadhiri mwenzake Bw. Wendo K. Nabea. Hawa walinipa moyo na kunishajiisha wakati wowote nilipotamauka. Asanteni sana tangu mwanzo mmekuwa wanasihhi wangu kiakademia. Maelekezo na ushauri mlionipa ni dira maishani mwangu daima. Shukrani zangu pia ziwafikie wahadhiri wote wa Idara ya Lugha na Isimu hususan Dkt. Karisa Beja, Bw. Mayaka. Bw. Siteti wa Ngero, Bw. D. Chacha na Bi Ann Juma. Mawaidha yao yalinijenga kiasi si haba katika usomi na ufanisi wa kazi hii.

Pia, namshukuru kwa dhati mkuu wa Kitivo cha Sanaa na Sayansi Jamii Dk. M. M. Theuri na wahazili wake Bi. Mary Maina na Bi. Ann Kamau na msajili msaidizi katika Kitivo cha Sanaa na Sayansi Jamii Bw. S. M. Njema, kwa misaada yao ya mara kwa mara. Walinikongolea chembe za hali na mali wakati wa uhitaji wangu. Wote hawa ninawaombea baraka zake Maulana daima. Shukrani zangu ziwaendee wapenzi wazazi wangu Bw. na Bi. Gacheiya kwa kujikusuru na kunigharamia masomo haya. Hakika hii ni hisani na mapenzi yasiyo na kifani, na bila shaka ni muhali kuyalipa kwa shukurani au mali. Nawaombea Maulana awakirimie mahitaji yao yote. Aidha, naishukuru familia ya Bw. na Bi. P. Karanja kwa kunipa hifadhi na makao kwa muda wangu wote wa uzamili. Hakika walijinyima raha na starehe kwa kunihifadhi kama mmoja wa wanao.

Mwisho, nawashukuru wanafunzi wenzangu J. Kirobi, D. Muthigua, E. Chomba na R. Ogolla tulioshirikiana nao katika shughuli nyingi za kiusomi na mijadala ya kiakademia ambayo tulishiriki kwa pamoja. Hususan Bw. Kirobi aliyenitia shime pasina kukoma. Muhimu zaidi, ni urafiki na undugu ambao uliboresha mazingira yangu ya usomi. Nyinyi nyote na wengine wengi walionifaa kwa hali na mali na ambao sikuweza kuwataja hapa, nawatakia baraka zake Maulana aliye asili ya mema yote.

Asanteni Sana!

ABSTRACT

Various languages are used for communication in Kenya. Among them are: first languages that are used by different ethnic groups, Kiswahili and English. This creates an environment of linguistic diversity. In multilingual situations where many languages are in use, people embrace and use different languages depending on their ethnicity and attitude towards such languages. As a result, different patterns of language use may emerge. It is in this respect that this research sought to find out how students' ethnicity and attitude affect language choice in a multilingual context. The research premised that, ethnicity and attitudes are central to language choice in situations of linguistic diversity. The research hypothesized that there are many languages in use and that there is a co-relation between ethnicity, attitudes and patterns of language use. Reasoned Action Theory and Ethnolinguistic Identity Theory formed the theoretical framework of this research. The research was done among students of Egerton University. Ninety participants and eight informal contexts were selected purposively. Ethnographic approach involving participatory observation and survey method that involved questionnaire schedules was used to collect data. Data was analysed descriptively by use of statistical package for social sciences that generated percentage rates and frequency tables. In the findings, it emerged that universities are a representation of the Kenyan community. Further, that students use at least three languages in their day to day activities. These findings confirmed the presence of specific patterns of language use. Kiswahili language is widely used in the dining halls, in the field and in birthday parties. In the basking context, it was found that students use a mixture of Kiswahili and English. First languages are popular in the hostels and when the students are talking to shopkeepers who are from their ethnic background. Further it emerged that students' attitude towards the languages they use and their ethnolinguistic identity, influence the choice of a language. Even though it was found that students generally have a positive attitude towards English language, every language considered in this research was found to have specific domains in which it is used. This study is expected to increase awareness and consciousness of how ethnicity and attitude contribute to language choice in multilingual contexts among language teachers and language policy implementers. This is vital since consciousness is the first step towards action. The findings are expected to add significantly to the existing body of knowledge in Sociolinguistics especially on language, ethnicity and attitude.

IKISIRI

Lugha mbalimbali hutumiwa kwa minajili ya mawasiliano nchini Kenya. Miongoni mwazo ni: lugha asili ambazo hutumiwa na makabila mbalimbali, Kiswahili na Kiingereza. Hali hii huzua mazingira ya wingi lugha. Katika mazingira ya wingi lugha, watu hupendelea lugha tofauti tofauti katika matumizi yao kutegemea kundi kabila na mielekeo yao kwa lugha hizo. Ruwaza tofauti za matumizi ya lugha basi zinaweza kuibuka. Ni kwa mujibu huu ambapo utafiti huu ulitathmini jinsi ukabila na mielekeo ya wanafunzi huathiri uteuzi wa lugha katika muktadha wa wingi lugha. Mtafiti alikisia kwamba, ukabila na mielekeo kwa lugha ni muhimu katika uteuzi wa lugha katika jamii zenye wingi lugha. Pia kwamba, kuna uhusiano baina ya ukabila, mielekeo na ruwaza za matumizi ya lugha. Nadharia ya kitendo kilichofikiriwa na nadharia ya utambulisho wa kiethnoisimu ziliongoza utafiti huu. Utafiti ulifanyika miongoni mwa wanafunzi wa Chuo kikuu cha Egerton. Washiriki tisini na miktadha minane iliyohusisha hali zisizo rasmi iliteuliwa kwa njia iliyoazimiwa. Wanafunzi walipewa hojaji wazijaze kibinafsi. Mkabala wa kiethnografia uliohusisha uchunguzi shiriki na mkabala wa kinyanja uliohusisha hojaji, ulitumika kukusanya deta. Deta ilichanganuliwa kupitia mtindo wa kitakwimu wa tarakilishi. Uchanganuzi ulikuwa wa kimaelezo. Katika matokeo, ilibainika kuwa vyuo vikuu ni viunzi vidogo vya jamii nzima ya Kenya. Matokeo haya yalielekeza katika ukweli kwamba, kuna lugha nyingi zinazotumiwa na wanafunzi katika shughuli zao za kila siku. Pili kuna ruwaza bainifu za matumizi ya lugha vyuoni. Lugha ya Kiswahili inatumika na kupendelewa sana katika vyumba vya maakuli, uwanjani, na katika sherehe za kuzaliwa. Katika vikundi vya wanafunzi wakiota jua, mchanganyiko wa lugha ya Kiswahili na lugha ya Kiingereza ulitumika. Vile vile, ilidhihirika kwamba, kuna kuchanganya lugha. Zaidi ya hayo, ilibainika kuwa, mielekeo ya wanafunzi kwa lugha wanazozitumia na pia utambulisho wao wa kiethnoisimu unaathiri uteuzi na matumizi ya lugha. Mielekeo ya wanafunzi kwa lugha wanazozitumia ilibainika kuwa changamani. Lugha zilizoshirikishwa katika utafiti zilibainika kuwa zina maeneo mahususi ambamo zinatumiwa ugugunduzi ambao ulibainisha kupendwa na hivyo kuteuliwa kwa lugha mbalimbali katika maeneo tofauti tofauti. Hata hivyo, kwa ujumla, lugha ya Kiingereza ilibainika kupendwa na kutumika zaidi na wanafunzi. Ufahamu huu utawafaa walimu wa lugha pamoja na wanaounda na kutekeleza sera za lugha ikizingatiwa kuwa, ufahamu ndio hatua ya mwanzo katika kutenda na kutimiza jambo. Pia, tasnifu hii itaongezea ujuzi maridhawa katika uwanja wa Isimujamii hususan lugha, ukabila na mielekeo.

YALIYOMO

IKIRARI	i
IDHINI.....	i
HATILINZI.....	ii
TABARUKU.....	iii
SHUKRANI.....	iv
ABSTRACT.....	v
IKISIRI	vi
YALIYOMO.....	vii
DIBAJI YA MAJEDWALI.....	viii

SURA YA KWANZA: UTANGULIZI

1.1 Utangulizi.....	1
1.2 Usuli wa mada.....	1
1.3 Mada ya utafiti.....	5
1.4 Madhumuni ya utafiti.....	6
1.5 Nadharia tete za utafiti.....	6
1.6 Umuhimu na sababu za kuchagua mada.....	6
1.7 Upeo na mipaka ya utafiti.....	7

SURA YA PILI: MAPITIO YA YALIYOANDIKWA KUHUSU MADA YA UTAFITI

2.1 Utangulizi.....	8
2.2 Ujuzi wa Lugha.....	8
2.2.1 Lugha katika elimu.....	9
2.2.2 Lugha na mielekeo.....	10
2.2.3 Uteuzi na matumizi ya lugha.....	13
2.2.4 Vichochezi vya uteuzi wa Lugha.....	17
2.2.5 Ukabila na lugha.....	19
2.2.6 Lugha na utambulisho.....	21
2.3 Misingi ya nadharia.....	21
2.3.1 Nadharia ya Kitendo Kilichofikiriwa.....	21

2.3.2 Nadharia ya Utambulisho wa Kiethnoisimu.....	25
--	----

SURA YA TATU: MBINU ZA UTAFITI

3.1 Utangulizi	28
3.2 Mbinu za utafiti	28
3.3 Uteuzi wa wahojiwa	28
3.4 Vifaa vya utafiti na Ukusanyaji deta.....	29
3.5 Uchanganuzi wa deta	30

SURA YA NNE: JINSI MIELEKEO NA UKABILA UNAATHIRI UTEUZI

WA LUGHA VYUONI

4.1 Utangulizi	32
4.2 Jumuiya ya Wanafunzi chuoni.....	32
4.2.1 Idadi ya Lugha wanazozungumza wanafunzi.....	34
4.2.2 Namna ya Kuzungumza lugha.....	36
4.2.3 Kuchanganya lugha na kiasi cha kuchanganya lugha.....	38
4.3 Mielekeo ya wanafunzi kwa lugha wanazozitumia.....	40
4.3.1 Lugha inayopendelewa katika kuzungumza.....	40
4.3.2 Lugha inayopendelewa katika kuandika.....	42
4.3.3 Lugha ambayo wanafunzi wanapendelea kusikiliza.....	44
4.3.4 Lugha ambayo wanafunzi wanapendelea kusoma.....	45
4.3.5 Lugha ya kuandika barua.....	47
4.3.7 Lugha katika vyombo vya habari.....	50
4.3.8 Lugha inayopendelewa katika kusoma magazeti.....	51
4.3.9 Ufaafu wa lugha ya Kiswahili kutumika chuoni.....	53
4.3.10 Kutumika kwa lahaja ya Sheng’.....	55
4.3.11 Uhuru wa kutumia lugha asili popote pale chuoni.....	55
4.4 Ruwaza za Matumizi ya Lugha.....	58
4.4.1 Lugha katika dhifa za wanafunzi na katika michezo ya kuigiza.....	63

4. 4. 2	Lugha ya kuwasiliana na Wauzaji wa Kundi Kabila	65
4. 4. 3	Lugha na muuzaji asiye wa kundi kabila la mwanafunzi.....	67
4. 4. 4	Lugha nje ya darasa na wanafunzi wa kundi kabila.....	69
4. 4.5	Lugha ya Maingiliano.....	72
4.5	Hitimisho.....	73
 SURA YA TANO: MUHTASARI, HITIMISHO NA MAPENDEKEZO		
5.1	Utangulizi.....	76
5.2	Muhtasari wa tasnifu.....	76
5.3	Muhtasari wa matukio muhimu.....	78
5.4	Mafanikio na matatizo.....	80
5.5	Mapendekezo.....	81
5.6	Mapendekezo ya maeneo ya utafiti zaidi.....	82
 MAREJELEO		
KIAMBATISHO A:	HOJAJI KWA WANAFUNZI.....	88

DIBAJI YA MAJEDWALI

Jedwali 1: Makundi kabila ya wanafunzi.....	33
Jedwali 2: Idadi ya lugha wanazozungumza wanafunzi.....	35
Jedwali 3: Jinsi ya kuzungumza lugha asili.....	36
Jedwali 4: Jinsi ya kuzungumza Kiingereza.....	37
Jedwali 5: Kiasi cha kuchanganya lugha.....	39
Jedwali 6: Upendelevu wa kuzungumza lugha asili.....	41
Jedwali 7: Upendelevu wa kuzungumza Kiswahili.....	41
Jedwali 8: Upendelevu wa kuandika Kiswahili.....	43
Jedwali 9: Upendelevu wa kusikiliza Kiswahili.....	44
Jedwali 10: Upendelevu wa kusoma Kiswahili.....	45
Jedwali 11: Upendelevu wa kusoma Kiingereza.....	46
Jedwali 12: Lugha ya kuandika barua kwa wazazi.....	48
Jedwali 13: Kusoma gazeti kwa lugha asili.....	52
Jedwali 14: Ufaafu wa lugha ya Kiswahili kutumika chuoni.....	54
Jedwali 15: Uhuru wa kutumia lugha asili popote pale chuoni.....	56
Jedwali 16: Kupendelewa kwa Kiingereza kuliko Kiswahili na lugha asili.....	57
Jedwali 17: Lugha inayotumiwa na wanafunzi chumbani mwa kulala.....	59
Jedwali 18: Lugha ya kuwasilisha michezo ya kuigiza.....	64
Jedwali 19: Kutumia Kiswahili na muuzaji wa kundi kabila.....	66
Jedwali 20: Kutumia lugha asili na muuzaji wa kundi kabila.....	67
Jedwali 21: Kutumia Kiswahili na muuzaji asiye wa kundi kabila.....	68
Jedwali 22: Lugha nje ya darasa na wanafunzi wa kundi kabila.....	69
Jedwali 23: Lugha nje ya darasa na wanafunzi wasio wa kundi kabila.....	71

SURA YA KWANZA

UTANGULIZI

1.1 Utangulizi

Mambo sita ya kimsingi yamezingatiwa katika sura hii. Kwanza ni usuli wa mada ambao unaelezea hali ya wazungumzi kwa mujibu wa matumizi ya lugha nchini Kenya, katika nyanja za elimu na ulimwenguni kote. Pia, usuli wa Chuo Kikuu cha Egerton umefafanuliwa. Pili, kuna mada ya utafiti ambayo ndiyo iliyokuwa pengo la utafiti lililokusudiwa kujazwa na utafiti wa tasnifu hii. Tatu kuna madhumuni ambayo ni maazimio ya utafiti kisha kuna nadharia tete za utafiti zilizokuwa mihimili ya utafiti. Tano, ni umuhimu na sababu za kuteuliwa kwa mada ambapo sababu zilizopelekea kuteuliwa kwa mada zimefafanuliwa. Hatimaye kuna upeo na mipaka ya utafiti ambapo kina cha utafiti na tasnifu kinabainishwa.

1.2 Usuli wa Mada

Nchini Kenya kuna makabila mengi yanayo ingiliana na kushirikiana kilugha. Wingi huu hulifanya taifa hili kuwa jamii yenye lugha nyingi. Ukweli huu ni sawia na maoni ya Hoffmann (1991) kuwa, hali ya wingi lugha ni tukio la watu wanaozungumza lugha tofauti tofauti kuwekwa au kuwa katika taifa moja. Tasnifu hii inajihusisha na jinsi ukabila na mielekeo ya wanafunzi inaathiri uteuzi na matumizi ya lugha katika chuo kikuu. Utafiti wa tasnifu hii ulizingatia chuo kikuu kwa vile vyuo huakisi uhalisia wa jumuiya ya Wakenya. Chuo kikuu cha Egerton kilitumika kama sampuli na utafiti ulijikita katika hali na miktadha isiyo rasmi.

Kwa mujibu wa Mugambi (2005), Kenya ni taifa la wingi lugha likiwa na takriban lugha 40 tofauti za kiasili; hizi ni lugha zinazozungumzwa na Wakenya wa asili tofauti ya kikabila. Juu ya hayo, kuna lugha za kigeni ambazo huchangia katika wingi idadi wa mkusanyiko wa lugha nchini Kenya. Hali hii ya wingi lugha, hulifanya taifa hili kudumisha mfumo wa lugha tatu; Kiswahili, Kiingereza na lugha asili ambazo zinatumiwa katika shughuli tofauti tofauti. Katika historia ya ulimwengu na vyuo vikuu, utafiti huu ulichukulia kuwa mpangilio wa jamii ya watu katika mataifa unafuata kwa kiasi fulani, misingi ya kundi kabila au lugha.

Wazungumzaji wengi aghalabu huweza kutumia zaidi ya lugha moja. Uwili lugha na hata wingi lugha huwa ndiyo kaida ya wengi ulimwenguni (Wardhaugh 1992:103). Zaidi, anatoa rai kuwa kuna lugha takriban elfu tano duniani lakini mataifa ni mia moja na tisini pekee na basi nchi nyingi huakisi uhalisia wa wingi lugha.

Kutokana na hali hiyo, inabainika kuwa, wingi lugha ni uhalisia ulio na nguvu kote ulimwenguni, hali inayoibuka, katika usahihi wake, kutokana na haja ya kuwasiliana baina ya jamii lugha. Ryan na Wengine (1982), wanadai kuwa, hata kama mzungumzi anazungumza lugha moja au zaidi, washiriki wote katika mazungumzo huwa wa jamii lugha moja. Jamii ambayo wanachama wake, hushiriki lugha moja au namna sawa ya mazungumzo na kaida za matumizi mwafaka ya lugha hiyo. Tofauti za lugha miongoni mwa, na kati ya jamii lugha, yaweza kuhusisha lugha tofauti au mitindo inayotofautiana ya lugha moja.

Kwa mujibu wa Whiteley (1974), Wakenya wengi hutumia lugha tatu hivyo kuzua mfumo wa lugha tatu. Lililo dhahiri ni kwamba, iwapo jamii fulani ina lugha nyingi, lugha hizo hupata hadhi tofauti katika mazingira tofauti. Hivyo basi, mkusanyiko wa lugha waweza kugawanywa na kutumiwa kutekeleza majukumu mbalimbali ya mawasiliano. Majukumu haya yanaweza kuwa ya kiuchumi, kisiasa au kielimu. Kutokana na majukumu haya, wanaotumia lugha huzua mielekeo mbalimbali kwa lugha hizo. Mielekeo kwa upande wake, kama matokeo ya fikra, huathiri vitendo vya mtu, uteuzi na matumizi ya lugha fulani ikiwa ni mojawapo wa vitendo kama hivyo. Mielekeo huwa msingi muhimu katika kumwongoza mtu kufanya uteuzi wa kitu au hali moja miongoni mwa nyingine (Tchai 1991). Katika utafiti huu, ilichukuliwa kwamba, binadamu katika harakati za maisha, huhitaji uchaguzi wa vitu, hali au mambo ili kufanikisha maisha yao. Wazungumzaji kwa upande wao, hulazimika kuchagua lugha mahususi kati ya wanazozijua wanapoazimu kuzungumza.

Katika harakati za usomi, mfumo wa elimu nchini Kenya, huwalazimu wanafunzi kuteua vyuo vikuu mbalimbali ili kujiunga navyo. Ingawa Chuo Kikuu cha Egerton, hakina historia ndefu kama ilivyo kwa vyuo vya Kenyatta na Nairobi, kihistoria, chuo hiki kinaweza kuchukuliwa kama kilicho kikongwe zaidi nchini Kenya. Kiliasisiwa mwaka wa 1939 na Lodi Maurice Egerton wa Tatton ambaye alikuja nchini Kenya mwaka wa 1920. Hamu yake kubwa ya usasi na kupiga picha ndiyo iliyomleta Kenya. Nchini Kenya, aliishi katika taarafa ya Njoro wilaya ya Nakuru, kwanza katika nyumba ndogo iliyoramaniwa na msimamizi wa shamba lake Bwana Hugh Coltart (Lord Egerton Castle Museum 2005). Baadaye, alijenga kasri ya kifahari maarufu kwa jina *Kasri la Lodi Egerton* kama juhudi za kumpendeza mchumba wake. Hata hivyo, baada ya kuliona, mchumba wake hakukubali uchumba naye na akarudi Uingereza. Hapo ndipo Gabi Maurice aliazimia kuanzisha shule ambayo ingetoa mafunzo ya kazi ya ukulima kwa vijana weupe walowezi.

Ili kutimiza azima hiyo, Lodi Egerton aliipa serikali ya Kenya ekari elfu moja ya shamba lake ambapo shule hiyo ilijengwa na kuwasajili wanafunzi watatu wa kwanza. Shule hiyo ilizidi kupanuka na kukua kadri miaka ilivyozidi. Kabla ya uhuru, Chuo cha Kilimo cha Egerton kama kilivyojulikana wakati huo, kilifungua milango yake kwa wanafunzi anuwai nchini Kenya na pia kwa wanafunzi kutoka mataifa mengine kama vile Tanzania, Uganda, Zambia, Malawi na Nigeria. Mwaka wa 1986, chuo hiki kilichapishwa katika gazeti la serikali kama bewa la Chuo Kikuu cha Nairobi. Mwaka uliofuata 1987, Chuo Kikuu cha Egerton kilianzishwa kupitia azimio la bunge na kuwa chuo kamili kinachojisimamia na kuendesha shughuli zake. Kilihifadhi jina la mwanzilishi wake kama ishara ya utambuzi wa ukarimu wake na kuendelea kutumia kauli mbio iliyomo katika mnara wa kifamilia wa ukumbusho *Sic Donec-(Thus we Serve)*. Hivi sasa, chuo hiki kina mabewa zaidi ya matano miongoni mwayo; Bewa la Njoro ambalo ndilo bewa kuu, bewa la Laikipia, Kisii, Nakuru Mjini, bewa la Kenyatta na Bewa la Mashariki Chuka.

Kila mwaka, chuo hiki, hupokea wanafunzi anuwai. Jumuiya ya chuo hiki huwa na tofauti zilizokithiri kilugha, kikabila, kitamaduni na kidini. Kwa upande wa kabila, takriban kila kabila nchini Kenya huwa limewakilishwa. Kwa upande wa lugha, chuo hiki ni jumuiya yenye lugha nyingi. Kwanza, kunazo lugha za kiasili kama vile Kikikuyu, Kikalenjin na Kijaluo. Kwa mujibu huu, utafiti huu ulitumia mgao ule wa vikundi vitatu vikuu vya aina za lugha kulingana na Greenberg katika Mugambi (2005). Alitoa rai kuwa, lugha asili za Kikenya zaweza kuanishwa katika vikundi vitatu vikuu ifuatavyo: kundi la lugha za Kibantu kama vile Kimeru, Kiluhya, Kikuria n.k. kundi hilo hushirikisha asilimia 65 ya jumuiya ya Wakenya. Kundi la lugha za Kinailotiki kama vile Kijaluo, Kikalenjin n.k ambalo hushirikisha asilimia 30 ya jumuiya ya Wakenya. Kundi la lugha za Kikushi kama vile Kiborana, Kirendille na Maa ambalo hushirikisha asilimia 5 ya Wakenya.

Aidha, kuna lugha ya Kiswahili ambayo ni lugha unganishi. Lugha hii ni ya kibantu na huzungumzwa kama lugha ya kwanza na watu wa Pwani ya Kenya. Pia, ni lugha sambazi, na lugha ya pili kwa Wakenya wengi. Huwaunganisha watu wa asili mbalimbali licha ya kuwa lugha ya kwanza ya Waswahili asilia. Mbali na hayo, kuna lugha ya Kiingereza. Nchini Kenya, hii ndiyo lugha rasmi na ya kutolea mafunzo katika daraja zote za usomi.

Kwa mujibu wa Schmied (1991), hali rasmi katika taifa lolote lile, lazima ilingane na ujuzi, matumizi na mielekeo kwa lugha hiyo ambayo imeshamiri katika taifa hilo. Kwa maoni yake anadai kuwa, mgawo wa lugha kama lugha ya kigeni, lugha ya mama au lugha ya pili,

huwa na misingi yake katika mwingiliano changamani wa tofauti nyingi za kiisimujamii na kiisimu. Kwa mfano, umri na muktadha wa kupata lugha: lugha ya mama kwa kawaida mtu hujifunza kutoka kwa wazazi wake (na ndiposa zina hayo majina), na lugha za kimataifa, kupitia mfumo rasmi wa elimu; lugha za pili zinaweza kupatikana kupitia mitagusano ya kijamii, haswa baina ya vikundi vya rika; lakini, pia, hata nyumbani au kupitia miaka ya mwanzo katika mfumo wa elimu. Kwa kuwa chuo kikuu ni daraja mojawapo ya usomi, lugha hii imeshamiri kiasi kwamba takriban arifa zote chuoni humo hutolewa kwa Kiingereza. Hali hii ni dhihirisho la uegemeo wa matumizi ya lugha fulani.

Katika Chuo Kikuu cha Egerton, wakati wa uwasilishaji wa mapendekezo ya utafiti, wanafunzi wa lugha ya Kiswahili, hulazimika kuwa na ikisiri kwa Kiswahili na Kiingereza. Hali hii ni dhihirisho la kuwepo kwa mielekeo fulani kwa lugha tofauti tofauti miongoni mwa watawala wa chuo na sera zao. Mtindo huu huishilia kuathiri uteuzi wa lugha ya matumizi miongoni mwa wanafunzi ikizingatiwa kwamba lugha zote zina hiari ya kuteuliwa na kutumika. Jambo hili ni tofauti na hali ilivyo katika shule za upili ambapo lugha ya Kiingereza hushurutishwa kutumika (Kaniu 2003:1). Wanafunzi wengi katika vyuo vikuu huishia kupendelea kutumia lugha ya Kiingereza kwani hawana budi kuandika ikisiri yenye mantiki kwa Kiingereza jambo ambalo huwalazimu wawe na uzoefu wa lugha ya Kiingereza.

Kwa kuwa wanafunzi wa vyuo vikuu hutofautiana kwa misingi ya kundi kabila na lugha, ruwaza tofauti za matumizi ya lugha zinaweza kuibuka. Kwa jinsi ambavyo wanafunzi waweza kutumia lugha yoyote kati ya zile wanazozijua kuwasiliana. Wanafunzi kila wanapoazimu kuwasiliana, hulazimika kuteua lugha mahususi kuitumia. Kulingana na Chai (1991), popote ambapo mtu huhitajika kuchagua kati ya vitu viwili au zaidi, swala la mielekeo hujitokeza na hivyo kuathiri kwa namna chanya au hasi uteuzi huo. Mathooko (2003), anatoa rai kwamba, lugha huonyesha utambulisho wa kikabila. Hii ni kwa sababu, lugha ni dhana ya utamaduni wa jamii kama ulivyo ukabila. Aidha, lugha ni kipengele chenye umuhimu mkubwa katika maisha ya mwanadamu kwani ni kiungo msingi katika mawasiliano ya watu.

Onyango (1990), anadai kwamba, vyuo vikuu huwa mstari wa mbele katika kuwatoa wasomi wanaoigwa na wengi. Hata hivyo, alitambua kuwa, wasomi hawa wana mielekeo hasi kwa Kiswahili na lugha mama. Kenya kama taifa lenye wingi lugha, dhana ya sera ya lugha katika elimu huzua malumbano mengi (Whiteley, 1974). Nchini Kenya, kuna lugha asili takriban 40 kama yalivyo makabila. Juu ya hayo, kuna lugha za kigeni zinazochangia katika ugumu na

utata wa hali ya lugha. Katika shule za msingi na za upili wakati wote, sera za lugha huhitaji wanafunzi kutumia lugha mahususi (Kaniu 2003:4).

Tofauti na tafiti kama hizo, katika vyuo vikuu hakuna ushurutishaji huu. Chuoni huwa ni mahali penye lugha nyingi na palipo na hiari ya uteuzi wa matumizi ya lugha. Hii ni hali ambayo huleta haja ya uteuzi wa lugha moja badala ya nyingine au hata kuchanganya lugha katika miktadha na hali maalum. Uteuzi kama huu, hutawaliwa miongoni mwa mambo mengine na: mielekeo aliyonayo mtu kwa lugha husika (Tchai 1991). Katika utafiti huu, mtafiti alipiga hatua zaidi na kujumlisha kabadala cha ukabila ambacho alikisia kuwa kinaathiri uteuzi wa lugha.

Hoffmann (1991), anatoa rai kuwa, mtagusano wa lugha kawaida huzua msambao usio sawa wa ruwaza za matumizi ya lugha katika kundi husika. Kama maenezi yangukuwa yanafanana, yaani kama lugha husika zingetazamwa kuwa na hadhi sawa na kila moja kutumika kwa kiwango sawa na katika hali sawa, basi labda hakungekuwa na shida yoyote. Hata hivyo, hali sivyo ilivyo. Ni kutokana na misingi hiyo ambapo utafiti huu ulifanywa kuchunguza matumizi ya lugha katika vyuo vikuu hususan jinsi ukabila na mielekeo huchangia katika uteuzi wa lugha. Katika kufanya hivyo, utafiti ulikuwa ukizingatia umuhimu wa vyuo vikuu kama daraja kati ya usomi na ulimwengu wa kazi huku vikiakisi uhalisia wa miktadha ya uhiari wa matumizi ya lugha.

1.3 Mada ya Utafiti

Jamii ya vyuo vikuu huwa na tofauti zilizokithiri kuanzia umri wa wanafunzi, kozi wanazozisoma mielekeo yao kwa mambo tofauti tofauti hadi kwa kundi kabila lao. Katika mazingira ya wingi lugha, uteuzi na matumizi ya lugha huwa jambo la kimsingi. Uteuzi huu huwa kwa mikabala mbalimbali. Kutokana na hiari ya matumizi ya lugha na ukweli kwamba, jamii ya vyuo vikuu huwa anuwai, haijulikani jinsi mielekeo na ukabila huathiri uteuzi wa lugha vyaoni. Utafiti huu ulijikita katika kuchunguza hali hii ili kuweza kuweka wazi mielekeo waliyonayo wanafunzi wa vyuo vikuu kuhusiana na lugha mbalimbali wanazozitumia katika harakati za kila siku chuoni pamoja na kubainisha jinsi mielekeo hii na ukabila wa wanafunzi huathiri uteuzi na matumizi ya lugha chuoni na kuzua ruwaza tofauti za matumizi ya lugha.

1.4 Madhumuni ya Utafiti

Utafiti huu ulizingatia madhumuni yafuatayo:

1. Kuchunguza mielekeo ya wanafunzi kwa lugha wanazozitumia.
2. Kupambanua ruwaza za matumizi ya lugha miongoni mwa wanafunzi wa chuo kikuu cha Egerton.
3. Kuchunguza uhusiano kati ya ukabila, mielekeo na ruwaza za matumizi ya lugha.

1.5 Nadharia Tete za Utafiti

1. Wanafunzi wana mielekeo tofauti tofauti kwa lugha wanazozitumia.
2. Kuna ruwaza zilizokithiri za matumizi ya lugha miongoni mwa wanafunzi wa chuo kikuu cha Egerton.
3. Kuna uhusiano kati ya ukabila, mielekeo na ruwaza za matumizi ya lugha.

1.6 Umuhimu na Sababu za kuchagua mada

Lugha ni ala muhimu katika elimu. Basi, uchunguzi wa taasisi za elimu katika darubini za lugha ni jambo muhimu katika kufanikisha mipango ya elimu. Kwa kuangazia matumizi ya lugha miongoni mwa wanafunzi, na kubainisha jinsi ukabila na mielekeo huathiri uteuzi wa lugha, umaarufu wa lugha mbalimbali ulipatikana. Huo ni mchango mkubwa hususan katika kuwawezesha wakufunzi wa stadi za mawasiliano kukabiliana na kutatua tatizo la kimawasiliano miongoni mwa wanafunzi. Juu ya hayo, kama tasnifu ilivyotanguliza, vyuo vikuu huwa jumuiya anuwai, yenye asili tofauti, inayoingiliana na kuwasiliana kwa mapana na marefu. Jambo hili huzua wingi lugha na hapo kuzua matumizi ya lugha nyingi. Hata hivyo, uteuzi na matumizi ya lugha moja kati ya nyingine nyingi zinazozungumzwa katika jamii lugha huweza kuathiriwa na mielekeo na ukabila wa wanajamii wa jamii lugha husika.

Utafiti wa aina hii haukuwahi kufanywa ili kuthibitisha jinsi ukabila na mielekeo huathiri uteuzi wa lugha miongoni mwa wanafunzi wa vyuo vikuu. Fauka na hayo, hapana utafiti wowote ambao uliwahi kufanywa kuhusiana na tabia ya wanafunzi katika kiwango cha vyuo vikuu kuhusiana na matumizi ya lugha. Zaidi ya hayo, chuo kikuu huwa ni daraja kati ya ushurutishaji (shule za msingi na za upili ambapo lugha fulani hushurutishwa), mazingira ya hiari ya lugha na ulimwengu wa kazi. Mathooko (2003), anadai kuwa, ukabila na uhusiano wake

na lugha ni jambo la kijamii linalohitaji uchunguzi zaidi. Mada hii ilichaguliwa kwa minajili ya kujaza pengi hilo miongoni mwa mengine.

Kwa kuwa ubadala wa lugha kama dhana inayosaidia kudumisha umoja, ustahimilivu na uvumiliano baina ya makabila hauwezi kupuuzwa katika jamii kama hii, utafiti huu ulikuwa ni muhimu. Haja ya kuendeleza na kukuza nadharia za lugha na dhana zinazohusiana nayo pamoja na hamu ya kutaka kugundua jinsi wanafunzi hukabiliana na daro la wingi lugha chuoni ilikuwa ni motisha tosha. Wingi wa hali baina ya makundi kabila, mielekeo kwa lugha tofauti na mikakati ya kiethnoisimu ambayo wanafunzi hutwaa na kutumia chuoni ilikuwa ni daro kuu la utafiti huu. Pia ufafanuzi uliopatikana baada ya utafiti, ulinuiwa kuongezea ujuzi katika uwanda wa Isimujamii.

1.7 Upeo na Mipaka ya Utafiti

Utafiti ulijikita katika kuchunguza matumizi ya lugha miongoni mwa wanafunzi wa vyuo vikuu. Ulichunguza jinsi ukabila na mielekeo huathiri uteuzi wa lugha katika vyuo vikuu. Upeo wa utafiti haukuruhusu kushughulikia jamii ya wafanyikazi wa chuo. Utafiti wenyewe ulijikita katika chuo kikuu cha Egerton, bali bewa la Njoro pekee. Utafiti ulilenga daraja hii ya usomi kwani, vyuo vikuu huchukuliwa kama kiwakilishi cha jamii nzima ya Kenya.

Matumizi ya lugha katika shughuli na hali zisizo rasmi kama vile matumizi ya lugha vyumbani mwa wanafunzi, katika vikundi vyao wanapostarehe, na dukani yalichunguzwa. Shughuli rasmi hazikuzingatiwa kwani kunazo kaida na sheria zinazoandamana na urasmi. Kaida na sheria hizo humfunga mzungumzi kutumia lugha mahususi kwa namna mahususi inayoafiki hali na shughuli kama hizo. Kwa upande wa lugha, utafiti ulijikita katika lugha za kiasili, Kiswahili na Kiingereza. Upeo huu ulipelekea utafiti kuziorodhesha lugha zote za kwanza katika kundi moja yaani, lugha asili. Pia haikuwa wajibu wa utafiti kuzingatia lahaja mbalimbali za lugha asili hizo kwani haikuwa katika upeo wa utafiti.

SURA YA PILI

MAPITIO YA YALIYOANDIKWA KUHUSU MADA YA UTAFITI

2.1 Utangulizi

Jambo hili ingawa halijashughulikiwa kwa kina katika vyuo vikuu, kuna kazi zinazomulika swala la lugha, ukabila na mielekeo kwa ujumla ingawa kwa kuisisitiza vipengele tofauti. Mapitio haya yaligawanywa katika vijisehemu saba. Vijisehemu hivi ni: ujuzi wa lugha, lugha katika elimu, lugha na mielekeo, vichochezi vya uteuzi wa lugha, uteuzi na matumizi ya lugha, ukabila na lugha na hatimaye lugha na utambulisho. Vijisehemu hivi vimeshughulikiwa kwa kina hapa chini.

2.2 Ujuzi wa Lugha

Kiwango cha kutumiwa kwa lugha fulani kawaida hutegemea zaidi ujuzi wa mzungumzaji wa lugha husika. Aidha, ikiwa ni sehemu ya mkusanyiko wa lugha za mzungumzaji, ikiwa imeamuriwa na sheria rasmi, au, ni jambo la mjadala wa kibinafsi wa utambulisho wa kijamii katika mazungumzo (Philip 1997). Kioko, na wengine (2001), wanadai kuwa ni kweli kwamba, Afrika ni bara changamani kiisimu. Ukweli huu unaakisiwa na idadi kubwa ya lugha zinazozungumzwa na Waafrika.

Wengi wa Waafrika husema kuwa, wanaweza kuzungumza lugha nne au hata tano. Utaratibu wa kuzungumza unazingatia hadhi zao. Katika mataifa matatu ya Kiafrika kwa mfano; kule Zambia; Kiingereza kinashikilia nafasi ya kwanza kikifuatwa na Kibemba na hatimaye Kinyanja. Kule Tanzania; Kiswahili kinashikilia nafasi ya kwanza kikifuatwa na Kiingereza. Nchini Kenya, Kiingereza kinaongoza, Kiswahili kinafuata na hatimaye lugha asili. La muhimu zaidi katika madai hayo ni kwamba, nchini Kenya na Zambia, Kiingereza kinatawala zaidi kuliko lugha asili wakati ambapo lugha ya Kiswahili ni muhimu zaidi Tanzania. Hali hii itaendelea ikiwa wazazi wana usemi katika upataji lugha wa wanao. Aidha kupitia ufundishaji wa moja kwa moja nyumbani, au, kuwatia shime watoto wao kujifunza lugha ya Kiingereza kule nje. Maoni hayo yalikuwa muhimu katika utafiti huu kwa vile, ujuzi wa mtu wa lugha fulani, huweza kuathiri mielekeo yake kwa lugha hiyo. Hata hivyo, ingawa maoni hayo yalinufaisha utafiti huu, upeo wa kazi hii ulimhini mtafiti kushughulikia swala la ujuzi wa lugha.

2.2.1 Lugha katika Elimu

Lopez (2000), anasema kwamba, mifumo ya elimu duniani kote, hutambua umuhimu na nafasi ya lugha katika kujifunza na kufunza. Alipiga hatua zaidi na kuvitazama vitendo hivi vya kujifunza na kufunza, kama mazungumzo ya watu wawili na wenye kupenda kuwasiliana. Kwa mkabala huu anasema, “Mawasiliano kwa upande mmoja, ni hali ya kati mno katika kufunza na kusoma na katika upande ule mwingine, ni chombo na njia ambayo kwayo walimu na wanafunzi hufasili jitihada zao za kila siku katika darasa” (Lopez 2000). Kulingana na kauli hiyo, inabainika kwamba, hii ndiyo sababu kila mahali ulimwenguni, mfumo wa elimu huhimiza sana mawasiliano na lugha. Aidha, dhana hizi mbili hutazamwa kama sehemu zilizo muhimu zaidi katika mtaala wa elimu. Hali hii inafafanua sababu za kuwepo kwa somo la stadi za mawasiliano katika vyuo vikuu nchini Kenya kama somo la lazima na la msingi kwa kila mwanafunzi. Zaidi, inadhihirika kuwa lugha na mawasiliano huwa na uhusiano wa karibu kwani, dhana hizi mbili zinajengana. Uhusiano huu ni wa karibu mno na unalinganishwa na uhusiano uliopo kati ya lugha na mawazo kama alivyodai Crystal (1994).

Ingawa haya ni maoni ya kweli katika utaratibu wa kujifunza na kufunza katika jamii zote, matatizo mahususi huibuka katika jamii zenye wingi lugha ambapo wanafunzi hujiunga na mfumo wa elimu wakiwa na lugha asili ambazo huzitumia kufasili na kuzua maana ya ulimwengu unaowazunguka. Aidha, ujuzi wao wa lugha za kwanza unakuwa masharti ya kujifunza lugha nyingine (Lopez 2000; World Bank 1988). Lugha hizo nyingine ambazo mwanafunzi hukumbana nazo kwa kiasi kikubwa, huwa ni lugha za mawasiliano mapana katika jamii. Wanafunzi katika jamii kama hii, huhitajika kujifunza lugha hizi ili kuweza kutenda kazi vyema katika serikali yao na pia katika ulimwengu kwa ujumla. Licha ya kurutubisha utafiti, hizo ni kauli zilizolingana sana na muktadha wa vyuo vikuu nchini Kenya, muktadha ambao ulizingatiwa katika utafiti.

Matumizi ya lugha asili kama lugha ya kutolea mafunzo, inaaminika kwamba yanarahisisha ukuaji wa dhana za wanafunzi ambazo huwawezesha kupata ujuzi katika lugha ya pili au hata ya tatu na zaidi, kusaidia kuweka wazi kwa wanafunzi tamaduni za jamii zao (Sifuna, 1980; Milon, 1992). Mbali na hayo, lugha ya kutolea mafunzo huwa pia ni namna ambayo kwayo, wanafunzi huweza kueleza tajiriba zao katika utaratibu wa kusoma. Haya ni maoni yaliyoufahamisha utafiti huu hususan katika kuzingatia kwamba, swala la lugha katika elimu, huonekana kama dhana muhimu katika kusoma na kufunza.

Hutasoit (1965), anatoa rai kuwa, ushawishi kuwa lugha asili ndiyo lugha pekee ambayo kwayo mwanafunzi anaweza kupata masomo halisi na kuwa tayari kuandika katika darasa la kwanza ulizua mabadiliko katika mijadala ya lugha ya kutolea mafunzo nchini Kenya. Anderson akinukuliwa na Makau (1980), anatomelea rai hii kwa kudai kuwa, tajiriba kubwa yaelekea kuwa, lugha asili kama namna ya kutolea mafunzo, ni bora kielimu kwani, kufunza dhabiti, lazima kwa kiwango fulani kuingiliane na maisha ya nyumbani ya mwanafunzi. Aidha, lazima kujifunza huku, kuwe katika misingi ya dhana ambazo mwanafunzi amejifunza katika tajiriba zake za mwanzo shuleni. Hata hivyo, Whiteley (1974), anadai kuwa, elimu nchini Kenya haiungi mkono kikamilifu ukuaji wa lugha asili anapodondoa sifa za kukosekana kwa fedha, wataalamu na namna sanifu ya mfumo wa kuandika. Anapiga hatua na kudai kuwa, sera za lugha katika elimu zimeipa lugha ya Kiswahili kipaumbele na kupuuza lugha asili hali ambayo huishilia kutoteuliwa kwa lugha asili kutumika katika nyanja mbalimbali.

Kufikia mwaka wa 1976, lugha asili zilichukuliwa kuwa lugha bora zaidi kutumiwa kwa wanafunzi wengi wa madarasa ya mwanzo (Ministry of Education 1976). Faida za kutumiwa kwa lugha asili katika miaka hii ya mwanzo kama lugha za kutolea mafunzo, zilianzishwa hata ilipokuwa wazi kuwa kujua kusoma na kuandika katika Kiingereza kulikuwa azima kuu. Katika shule zilizokosa lugha asili ya jumla katika darasa, Kiswahili kilitumika (Ministry of Education 1976). Kwanzia wakati huo hadi sasa, sera ya lugha nchini Kenya, huhitaji kuwa, lugha asili zitumike katika madarasa ya mwanzo (darasa la kwanza hadi la tatu) kama lugha ya kutolea mafunzo. Lugha ya Kiingereza na lugha ya Kiswahili hufunzwa kama somo, lakini kuanzia darasa la nne hadi la nane lugha ya Kiingereza inachukuliwa kama lugha ya kutolea mafunzo (Kenya, Republic of, 1976). Sasa hivi, lugha hii inatumika kama lugha ya kutolea mafunzo kwanzia shule za chekechea hadi chuo kikuu.

2.2.2 Lugha na Mielekeo

Okwany (1995), akitafitia mielekeo katika kujifunza lugha ya Kiswahili katika shule za upili mkoani Nairobi, alibainisha kuwa wanafunzi walikuwa na mielekeo chanya kuhusu somo hilo. Hata hivyo, kuna tafiti zinazodhihirisha kuwepo kwa mielekeo hasi kwa Kiswahili hivi sasa. Hata hivyo, utafiti huo ulinufaisha utafiti huu katika mbinu za utafiti haswa ukusanyaji na uchanganuzi wa deta. Kwa vile aliangazia mielekeo ya wanafunzi, utafiti wake ulikuwa msingi muhimu wa kujenga utafiti huu ingawa utafiti huu haukuingilia ujifunzaji wa lugha.

Onyango (1990), alichunguza mielekeo ya wasomi kuhusu matumizi ya Kiswahili nchini Kenya. Aligundua kuwa, wasomi hawasisitizi matumizi ya Kiswahili katika miktadha rasmi. Badala yake, wanajitambulisha rasmi na lugha ya Kiingereza. Yeye aliangazia wahadhiri wala sio wanafunzi. Pia hakuzingatia hali zisizo rasmi ambazo hazina kaida zinazofunga matumizi ya lugha jambo lililoangaziwa na utafiti huu. Ingawa mtafiti hakuonyesha athari ya mielekeo ya wasomi hao kwa matumizi ya lugha ilhali wasomi ni vielelezo vya jamii na huigwa na wengi, uangavu wa maelezo yake ya nadharia ya kitendo kilichofikiriwa, yalikuwa ni dafina katika kujenga msingi wa nadharia iliyoongoza utafiti huu.

Momanyi (2004), katika *East African Standard* (Saturday 24th – 05 – 04), alizungumzia matatizo yanayolikumba somo la Kiswahili katika ngazi za juu za usomi. Aliratibisha mtazamo wa wanafunzi unaohusu miongoni mwa mambo mengine; mielekeo hasi kwa Kiswahili; alidai kuwa mtazamo huu unachangia katika kuamua lugha ya matumizi. Alipiga hatua zaidi na kusema kwamba, baadhi ya wanafunzi huiona lugha ya Kiswahili kama lugha iliyoshindwa kufungua milango ya ufanisi kiuchumi. Wengine huiona lugha hii kama iliyoshindwa kukidhi mahitaji ya uvumbuzi wa kisayansi. Ingawa hakutathmini matumizi ya lugha, kauli hizo zilichochea pakubwa utafiti huu hususan katika kubainisha mielekeo ya wanafunzi kuhusiana na lugha ya Kiswahili ikilinganishwa na Kiingereza na lugha za kiasili.

Nchini Kenya, kuna magazeti matatu makuu ya Kiingereza (*Nation, Standard na People*) ilhali kuna gazeti moja tu la Kiswahili *Taifa Leo* (Kaniu 2003). Hivi majuzi, gazeti la *The Leader* ambalo limeanzishwa mwaka wa 2005 na kampuni ya *Royal Media Services* limeingia katika msururu wa magazeti ya Kiingereza; hivyo, kufikisha idadi ya magazeti kwa Kiingereza kuwa nne. Katika utangazaji, idhaa za radio kama vile *Kiss 100*, licha ya watangazaji wake kutumia maneno ya Kiswahili hapa na pale katika utangazaji wa vipindi vyao, hawana hata kipindi kimoja mahususi kwa lugha ya Kiswahili. *Radio Nation* ilikuwa nacho kijulikanacho kama *Kamusi ya Changamuka* ingawa kishaondolewa. Kuondolewa kwa kipindi hiki ni pigo kuu kwa lugha ya Kiswahili. Mbali na hayo, muda unaopewa vipindi kwa lugha ya Kiswahili, ni mfupi mno ukilinganishwa na muda wa vipindi kwa lugha ya Kiingereza. Aidha, vipindi katika lugha ya Kiswahili ni vichache sana tofauti na idadi ya vipindi kwa lugha ya Kiingereza.

Kwa upande ule mwingine, lugha asili zimepata natija kuu kwani kumeanzishwa idhaa zinazopeperusha matangazo yao kwa lugha asili. Hizi idhaa ni kama vile; *Kameme kayu ka muingi, Coro, Inoro, Ramogi, Musyi, Mulembe*.

Jitihada kama hizo, ziwe chanya au hasi, zilikuwa kigezo muhimu katika kuthibitisha ikiwa wanafunzi wa chuo kikuu wanapendelea kusoma maandishi ya Kiswahili au ya Kiingereza na hupenda kusikiliza idhaa zipi za utangazaji. Zaidi ya hayo, kwa mujibu wa nadharia ya utambulisho wa kiethnoisimu, juhudi kama hizi za lugha kuungwa mkono na taasisi mbalimbali huchangia sana katika nguvu-tendi za kiethnoisimu. Kutokana na hali hiyo ilikuwa rahisi kuweza kutathmini matumizi ya lugha hizo kwani jinsi mtu anavyosikiliza na kusoma makala za lugha fulani, ndivyo anavyoshawishika kuipenda na kuitumia lugha hiyo.

Gorman (1974), akinukuliwa na Tchai (1991), alieleza kuwa, baadhi ya wanafunzi walikuwa na mielekeo hasi kwa lugha ya Kiswahili na wala hawakuonyesha hamu ya kutaka kujifunza lugha yenyewe. Hapa aliangazia hali ya lugha ya Kiswahili katika kiwango cha shule za upili tofauti na utafiti huu ulioangazia ngazi ya chuo kikuu. Kauli yake kuhusu wanafunzi kuwa na mielekeo hasi kwa lugha ya Kiswahili ilikuwa ni amali muhimu katika utafiti huu. Isitoshe, utafiti huo unathibitisha kuwepo kwa swala la mielekeo kwa lugha ya Kiswahili. Strong (1984), katika Mesthrie (2001), anadai kuwa utoshelevu ambao wanafunzi hupata kutoka kwa shughuli za usomi wowote huathiri mielekeo yao kuhusu kujifunza lugha fulani. Wanafunzi walio katika chuo kikuu, huchukuliwa kuwa na utoshelevu katika elimu. Hii ndiyo ngazi ya juu zaidi ya usomi. Hivyo, kuwatafiti wanafunzi hawa kulichukuliwa kwamba kungetoa picha halisi kwa mujibu wa mielekeo ya wanafunzi kwa lugha wanazozitumia.

Hoffmann (1991), akizungumzia nafasi ya mielekeo kwa lugha, anasema kuwa, ujozi lugha huzuka kutokana na mtagusano wa wazungumzaji. Aidha, kuenea kwa uwili lugha katika jamii nzima na kudumu kwake, hutegemea masharti ya kukua kwake kama ni mwafaka. Kulingana naye, haya huamuliwa na mielekeo ya mtu binafsi na pia, ya kundi zima kwa jumla kwa lugha husika. Mielekeo kwa uwili lugha, huanzia kuungwa mkono kirasmi au kukubaliwa, hadi kutoa idhini na haki kwa baadhi ya sehemu za taifa kutumia lugha zao za kimaeneo katika utawala na elimu. Hoffmann (1991), anatoa mfano kuwa, ni mataifa machache ambayo huruhusu kufunzwa kwa lugha za kiasili katika mfumo wa elimu. Hii ni hali ambayo inawiana sana na hali ilivyo nchini Kenya.

2.2.3 Uteuzi na Matumizi ya Lugha

Kabla ya ripoti ya elimu ya Afrika, (*African Education Report*) nchini Kenya mwaka wa 1949, wanafunzi wa shule za msingi walifunzwa katika lugha asili zao miaka mitatu ya mwanzo (Colony na Protectorate 1949). Kwa upande ule mwingine, ripoti ya utafiti wa sera ya elimu na utekelezaji, (*The report of the study of Educational Policy and Practice*) katika Afrika Mashariki ya 1951, ilipendekeza kufutiliwa mbali kwa lugha ya Kiswahili kama lugha ya kutolea mafunzo katika madarasa ya mwanzo.

Ripoti iliyofuatia hiyo mwaka wa 1953, ikapendekeza kwamba, katika miaka minne ya mwanzo katika shule za msingi, lugha asili ziwe lugha za kutolea mafunzo (Nuffield Foundation na Ofisi ya Kikoloni, 1953). Mapendekezo haya yalitekelezwa kikamilifu na serikali ya kikoloni. Miaka ya 1950 yote, wanafunzi katika shule za msingi nchini Kenya, walifunzwa kwa lugha zao asili katika ile miaka minne ya mwanzo; nayo lugha ya Kiingereza, ikafunzwa kama somo kwa miaka miwili au mitatu; na hapo baadaye, ikawa lugha ya kutolea mafunzo katika darasa la tano hadi saba (Sifuna 1980).

Kufikia katikati ya miaka ya 1950, kulikuwepo na kutoridhika kwa kiasi kikubwa kuhusu matokeo mabaya ya watoto wa Kikenya na Kirusi katika mitihani ya kitaifa iliyoandikwa kwa Kiingereza wakilinganishwa na wenzao kutoka Ulaya (Sifuna 1980). Wizara ya elimu, kwa kudai kuwa, kutofanya vyema huku kulitokana na matumizi ya lugha asili kama lugha ya kutolea mafunzo, ilianzisha kituo cha kipekee katika idara ya ukaguzi wa shule mwaka wa 1957. Kazi ya kituo hiki ilikuwa kutengeneza vifaa vya kufunzia na walimu kufanyia majaribio ya kuanzishwa kwa Kiingereza kama lugha ya kutolea mafunzo.

Mwaka wa 1957, lugha ya Kiingereza ilifanywa rasmi kuwa lugha ya kufunzia katika mfumo wa elimu nchini Kenya. Hii ni kwa sababu serikali ya kikoloni wakati huo, ilihisi kwamba, lugha za kiasili hazifai katika elimu (Kaniu 2003:2). Hata hivyo, mwaka wa 1976 arifa ya mawaziri ilitolewa kusisitiza kwamba, lugha za kiasili ndizo mwafaka zaidi katika ukufunzi. Lugha hizo zilitumika na walimu kufundishia, hususan katika madarasa matatu ya chini ingawa lugha ya Kiingereza ilibakia kutumika katika madarasa ya juu (Kaniu 2003:2). Inadhihirika hapa kuwa, jambo lililoanza kama jaribio lilishikilia nafasi kubwa katika mabadiliko makuu yaliyotokea katika shule za msingi nchini Kenya yaliyojulikana kama *New Primary Approach* (Hutasoit na wengine 1965).

Mwaka wa 1974, lugha ya Kiswahili ilitangazwa rasmi kuwa lugha ya taifa. Kufuatia mapendekezo ya Tume ya Elimu ya Mackay, somo la Kiswahili lilitangazwa kuwa somo la lazima na la kutahiniwa katika shule za upili na zile za msingi mwaka wa 1985 (Chimerah 1998). Tafiti hizo zilirahisisha kutambua jinsi ambavyo, juhudi hizo zimeathiri uteuzi na matumizi ya lugha katika chuo kikuu huku swala la mielekeo na ukabila likizingatiwa pamoja na uhiari wa lugha uliopo chuoni.

Abdulaziz (1982), ameeleza matumizi ya lugha mbalimbali katika sehemu za mashambani na sehemu za mjini nchini Kenya. Anadai kwamba, lugha za kikabila na Kiswahili hutumika sana katika sehemu za mashambani. Kauli hizo zilikuza ufahamu wa mtafiti kuhusu matumizi ya lugha mbalimbali. Hata hivyo, hayo ni tofauti na hali ilivyo ambapo lugha hizo zimeshamiri vilivyo katika chuo kikuu. Aidha, chuo kikuu cha Egerton kinaakisi mandhari ya sehemu za mashambani na mjini. Uvumbuzi huu ulikuwa ni motisha ya kutafitia hali halisi ilivyo.

Duran (1975) akinukuliwa na Tchai (1991), alifanya utafiti katika jamii yenye wingi lugha huko Lumbwa. Yeye aliangalia nafasi ya Kiswahili miongoni mwa lugha za kiasili kama vile Kijaluo, Kiluhya, Kikikuyu na Kikalenjin katika sehemu za mashambani. Yeye alijikita zaidi na mahusiano ya Kiswahili na lugha asili za Kikenya tofauti na utafiti huu ambao uliangazia uteuzi na matumizi ya lugha katika chuo kikuu.

Scotton (1980), akinukuliwa na Tchai (1991), alichunguza uteuzi wa lugha katika jamii yenye wingi lugha na kuthibitisha kwamba, uteuzi wa lugha unaweza kulinganishwa na kuhusishwa na sifa za kijamii za wazungumzaji, na pia, hali na mahali wanamojikuta. Alithibitisha kwamba, uteuzi wa lugha fulani unaweza kueleweka katika muktadha maalum wa maingiliano ambamo uteuzi huo hutokea. Alionyesha uteuzi wa lugha kama matokeo ya wazungumzaji kuathiriwa na muktadha maalum wa mazungumzo wala sio utambulisho wao kitabaka. Huu ulikuwa ni mshawasha mkubwa kutaka kutambua kama hali hii ni kweli katika vyuo vikuu nchini Kenya.

Platt (1980), naye alifanya utafiti juu ya uteuzi wa lugha na akaonyesha kuwa, katika jamii yenye lugha nyingi zenye hadhi tofauti tofauti, uteuzi wa mojawapo ya lugha hizo hautegemei lugha anazozijua mzungumzaji huyo tu, bali pia, lugha anazozijua anayezungumziwa.

Nader (1968), anasema kwamba, hamu ya kutaka kujiendeleza kihadhi ni mojawapo ya sababu muhimu ya wanafunzi kuwa na motisha ya kujifunza na kutumia lugha maalum. Tofauti na utafiti huo, huu haukuchunguza dhana za hamu ya kujiendeleza kihadhi au motisha ya kujifunza lugha bali ulizingatia uteuzi wa lugha mahususi.

Lambert na wengine (1968), wanasema kwamba mielekeo chanya humpa mtu motisha ya kujifunza na kutumia lugha. Kauli hiyo ni muhimu kwani motisha huwa na nafasi muhimu katika uteuzi wa lugha. Tchai (1991), alitafitia jinsi mielekeo inavyoathiri uteuzi wa lugha miongoni mwa wakaaji wa Malindi. Aligundua kwamba, mielekeo huwa muhimu katika uteuzi wa lugha ya kutumiwa miongoni mwa watafitiwa. Utafiti huu ulipiga hatua zaidi na kuchunguza athari za ukabila katika uteuzi wa lugha. Isitoshe, yeye alijikita kijiografia kule Malindi. Utafiti huu ulijikita katika eneo la Njoro ambapo pana chuo kikuu. Pia, yeye aliangazia lugha za kigeni kama vile Kiitaliano na Kijerumani jambo ambalo utafiti huu haukujihusisha nalo. Hata hivyo, utafiti wake ulipanua na kurutubisha ufahamu wa mtafiti kuhusu mielekeo kuhusiana na lugha, Kiswahili kikiwa miongoni mwa lugha alizoshughulikia.

Marylyn (1978), akizungumzia uteuzi na matumizi ya lugha katika shule za upili nchini Kenya, aligundua kwamba, wanafunzi wanaoenda shuleni, hukabiliwa na mazingira ya wingi lugha. Aligundua kwamba, wanafunzi hujikuta katika hali ambazo huwalazimu kufanya uamuzi wa mara kwa mara kuhusu uteuzi na matumizi ya lugha. Hii ni hali inayolingana sana na hali halisi ya vyuo vikuu nchini Kenya. Hata hivyo, katika shule za upili kuna ushurutishaji jambo ambalo halipo katika vyuo vikuu. Dhana hii ya ushurutishaji ndiyo iliyotofautisha utafiti wake na huu. Katika vyuo vikuu, hakuna ushurutishaji wa kutumia lugha jambo lilokuwa la muhimu mno katika utafiti huu.

Marylyn (1978), alihitimisha kwamba, mkusanyiko wa lugha mama ulishikilia nafasi kubwa katika kuteua lugha inayofaa zaidi katika kuwasiliana. Utafiti wake ulidhamiria kutambulisha ruwaza za matumizi ya lugha zinazoibuka wakati wanafunzi wanapotangamana baina yao. Tofauti ya utafiti huu na ule uliofanywa ni kwamba, utafiti huu ulipiga hatua zaidi na kujaribu kutambulisha jinsi dhana za mielekeo na ukabila huathiri uteuzi wa lugha na hivyo kuzua ruwaza hizo huku mtafiti akizingatia uhiari wa lugha vyaoni.

Obura (1990), akizungumzia hali ya matumizi ya lugha katika jamii ya Wakenya, anasema kwamba, uteuzi na matumizi ya lugha yoyote ile, huamuliwa na dhana kama vile mada, mpokeaji na motisha.

Matokeo hayo yalikuwa kiungo muhimu katika utafiti huu; kwa kuzingatia dhana hizo, uwazi wa jinsi dhana hizo huathiri uteuzi wa lugha na matumizi yake ulipatikana. Ilichukuliwa kwamba, katika mazingira ya wingi lugha, kuna mkinzano na ushindani katika matumizi ya lugha. Mazingira haya hutambulishwa na uhamishaji ndimi. Kuhusiana na swala hili la kuchanganya ndimi, Obura (1990), aligundua kwamba, kuchanganya ndimi ni hali ya kawaida katika shule za Kikenya. Iwapo ni kweli hali hizi hutambulisha mazingira ya shule ambapo kuna ushurutishaji wa lugha, mtafiti alistajaabia jinsi hali ilivyo katika vyuo vikuu ambapo hakuna ushurutishaji huu na hapo kuzua ari ya kutafitia hali ya vyuo vikuu.

Kimemia (2001), alitathmini dhana tofauti katika mawasiliano ya mdomo kuhusu uteuzi na ubadilishaji kutoka lugha moja hadi nyingine. Aligundua kwamba, hali hiyo inahusu vibadiliki kama vile maarifa ya washiriki, mkusanyiko wa lugha, mahusiano ya kijamii na kiuchumi, na manufaa au hasara inayokisiwa na mzungumzi katika kutumia lugha moja badala ya nyingine. Dhana alizozitafitia ni muhimu katika lugha yoyote ile ingawa ni vigumu kubashiri lugha ipi wazungumzaji watatwaa katika muktadha wowote ule. Hili ni pengo lililokusudiwa kujazwa kupitia utafiti huu.

Whiteley (1974), akizungumzia kuhusu matumizi ya lugha nchini Kenya, alidai kwamba, wazungumzaji huteua lugha katika hali fulani mahususi kulingana na tajiriba ambayo inaweza kutumika kimwafaka bila kuzua kero. Tafiti hizi zilitoa habari muhimu kuhusu hali ya uteuzi na matumizi ya lugha na washiriki mbalimbali. Utafiti huu hata hivyo, uliangazia dhana ambazo ni tendi tu katika vyuo vikuu.

Kulingana na Mugambi (2005), ni wazi kuwa, Kiingereza katika Afrika kinatumika zaidi katika mawasiliano ya maandishi kuliko mazungumzo, na zaidi pia, katika tabia pokezi kuliko zalishi. Zaidi, katika maeneo ya matumizi ya lugha, lugha ya Kiingereza haitumiki katika mawasiliano yanayoshirikisha kina babu na nyanya. Kauli hii inatilia uzito ukweli kuwa, hali hii inahusiana sana na utamaduni wa kanuni za heshima ambazo hulazimu kwamba, lugha asili itumike katika maswala yanayohusiana na ukabila na uridhi. Pia kuwa wazee hawa waweza kutokuwa na ujuzi wa kutosha wa lugha hii. Lugha ya Kiingereza na lugha ya Kiswahili zinatawala kwa sababu zina hadhi wakati ambapo lugha asili hazina hadhi hiyo. Lugha ya Kiingereza hutumika rasmi. Lugha ya Kiswahili kwa upande wake, ni lugha ya taifa na hutumika katika nyanja kama vile za siasa na bunge. Zaidi anadai kuwa, lugha asili hazijapewa hadhi hizo natumika katika mazingira ya nyumbani kwa ajili ya mawasiliano ya kikabila.

Rai nyingine inayotolewa na Mugambi ni kuwa, ingawa lugha ya Kiingereza na lugha ya Kiswahili huonekana kama lugha za kifahari kwa vile zinabeba uwezekano wa faida za kiuchumi, Wakenya huweka thamani kubwa katika lugha zao za kikabila kwa vile zinaendeleza utamaduni wa watu na historia yao. Haya ni mawazo dhabiti sana yaliyojenga utafiti uliofanyika. Hata hivyo, tofauti na utafiti wa Mugambi, huu haukujihusisha na uwezekano wa lugha hizi kupotea jambo aliloliangazia.

Kutokana na kauli hizo, inaelekea kwamba, nchini Kenya, hadhi ya lugha ya Kiingereza kama lugha rasmi na lugha ya Kiswahili kama lugha ya taifa, inazidi kushikilia nafasi muhimu katika mijadala ya sera ya lugha. Nafasi ya lugha asili haijatiliwa maanani sana kwa mujibu wa kuunda sera. Imechukuliwa na viongozi kuwa, kila mtu, anaelewa Kiingereza na Kiswahili; hivyo, kuafiki matumizi ya lugha zote mbili katika mikutano ya kisiasa na mabaraza.

2.2.4 Vichochezi vya Uteuzi wa Lugha

Hoffmann (1991) anatoa kauli kuwa, dhana zinazoathiri uteuzi wa lugha huwa sawa kwa watu wazima na watoto ingawa zinatenda kazi kwa viwango tofauti. Dhana hizi zina mchango kwa utafiti uliofanywa ingawa kwa upande wake, mtafiti hakujishughulisha kwa kiasi chochote na tofauti hiyo ya viwango vya utenda kazi wa dhana hizo. Kwanza, dhana aliyoiratibisha Hoffmann ni: mhusika katika kitendo neni. Alidai kuwa, hii ndiyo dhana iliyo muhimu sana katika uteuzi wa lugha kwa watoto. Katika utafiti wake, alibainisha hali ambapo baadhi ya watoto, wanawazungumzia wazazi wao kwa lugha tofauti. Pia, wajibu wa mhusika kwa mujibu wa mtoto waweza kufikiriwa kuwa wenye uamuzi kwa mfano yaya au walimu ambao huja kuhusishwa na lugha mahususi.

Hoffmann anapiga hatua na kusema kuwa, watoto wenye uwili lugha wanapozungumza na mhusika ambaye anafahamu lugha moja, mazungumzo huwa katika lugha ya huyo mshiriki na matokeo ya kuchanganya lugha huwa machache mno. Hata hivyo, watoto hawa wanapokutana na wenzao wa lugha mbili au zaidi, wanawazungumzia kwa aidha lugha na matokeo ya kuchanganya lugha kuwa mengi. Kauli hii ndiyo iliyokuwa muhimu zaidi kwa utafiti huu kwani, ulifanyika katika mazingira ya wingi lugha. Tofauti na utafiti huo, huu haukujihusisha na watoto bali na watu waliokomaa hivi kwamba uteuzi wao wa lugha huwa wenye weledi.

Pili, aliorodhesha dhana ya kazi au haja ya mazungumzo kama kichochezi cha lugha itakayoteuliwa na mshiriki kutumika. Mjadala wake kuhusu kauli hii, hususan uliegemea, watoto walio na ujozi lugha au wingi-lugha hutumia lugha kama wenzu wa ulimwengu. Harrison na Piette (1980), wanatoa mfano wa mtoto ambaye alihama kutoka lugha moja hadi nyingine huku akitarajia kuwa mshiriki atakubaliana na matakwa yake ya kucheza zaidi. Hii ni dhana iliyokuwa muhimu sana katika kujenga ile kauli ya lugha inayoteuliwa na wasailiwa wanapohudumiwa na wauzaji wa kundi kabila lao na wale wasio wa kundi kabila lao. Kauli hizi, zilichangia kiasi kikubwa kutambulisha sababu zinazoambatanishwa na lugha inayoteuliwa.

Rai nyingine anayoitoa Hoffmann ni kuwa, lugha fulani yaweza kuteuliwa aidha kutenga au kuhusisha washiriki wengine waliopo katika mazungumzo. Alibainisha kuwa, watoto wanaweza kuamua kuteua lugha mahususi badala ya nyingine ili kusimulia kisa tena, au kufanya mzaha au kumnukuu mtu mwingine anapohusika katika dhima fulani. Katika namna hizi zote, uteuzi hufanywa kwa makusudio kuwa ujumbe lazima ubebe maana mahususi au uwe na athari mahususi. Kauli hizi zilifaa utafiti huu katika kujua kwa nini wanafunzi wanateua lugha moja badala ya nyingine katika miktadha mbalimbali hasa ilipobainika kuwa, vikundi vyao mara nyingi huwa havijajitenga kwa misingi ya kikabila. Hata hivyo, utafiti huu haukingilia maswala kama vile ya kumnukuu mtu au utafsiri ambao utafiti wa Hoffmann ulishughulikia miongoni mwa mengine. Pia, haikuwa katika shabaha ya utafiti huu kujihusisha na maana ya ujumbe au athari zinazotokana na ujumbe huo.

Kauli ya nne aliyoitoe Hoffmann ni ustadi wa kiisimu. Alidai kuwa kiwango cha ustadi alichonacho mtu katika lugha, kinaweza kushirikisha sababu za kiisimu au za elimunafsia za kuteuliwa kwa lugha. Mzungumzaji anaweza kuamua kutumia lugha ambayo anajiamini kuwa na uwezo wa kuitumia kwa sababu ya fedheha inayotokana na kutoweza kuisema ipasavyo na kwa urahisi. Katika hali ya namna hii, sababu zile zingine, zinaweza kupitwa na dhana hii ya kuwepo kwa lugha; kadri mzungumzaji anavyokwazika katika umahiri wa lugha husika, ndivyo ilivyo rahisi kuwa dhana hii itaibuka na kuamua lugha itakayotumika. Kauli hizi zinaingiliana sana na utawala wa lugha katika swala zima la uteuzi na matumizi ya lugha. Utafiti huu haukingilia swala la ustadi kwa jumla au ni kiwango kipi cha umahiri walichonacho wanafunzi katika lugha wanazozitungumza licha ya kuufahamisha kwa kiasi kikubwa utafiti huu kuwa hii ni dhana moja na ya kati iliyo na mchango mkuu katika uteuzi wa lugha.

2.2.5 Ukabila na Lugha

Uhusiano wa lugha na uwanachama wa kundi kabila unaweza kudhaniwa kuwa ni moja ya mahusiano yaliyo wazi ya kitamaduni. Hata hivyo hali ni kinyume. Lugha nyingi za ulimwengu, kwa mfano huhusishwa kwa kiasi kikubwa na kundi fulani la kikabila au kitamaduni. Ukabila ni msingi katika utambulisho wa kibinafsi, na ujuzi wa lugha ya kundi kabila hutambulisha watu na jamii yao na kuwafanya wanachama (Mathooko 2003).

Lowley (1983), anasema kuwa, uhusiano baina ya lugha na ukabila umeonyeshwa katika tafiti nyingi. Kwa mfano, aliwahoji wawakilishi wa vikundi vya makabila matatu ya Kimarekani. Aligundua kwamba, vikundi hivi vyote vilitaka kudumisha utambulisho wao pamwe na utambulisho wao wa Kimarekani. Pia kwamba, walifasiri lugha zao za kikabila kuwa muhimu mno. Tofauti na utafiti huo, huu ulijikita nchini Kenya.

Akitafitia ukubalifu kati ya lahaja ya Lwitakho na Logooli za lugha ya Kiluhya, Kabeya (1993) katika Mathooko (2003), aligundua kwamba, katika maingiliano ya lahaja, lugha huwa kidokezi muhimu cha utabaka wa kijamii. Zaidi hutazamwa kuwa muhimu sana na chenye dhamani katika utambulisho wa vikundi. Uvumbuzi huu ni sawa na ule wa Robinson (1972), katika Giles na wengine (1987), kwamba, kuhamisha lugha kuelekea lugha asili huonyesha uwanachama kwa kundi fulani kikabila. Tofauti na tafiti hizo, utafiti huu haukuchunguza maingiliano ya lahaja za lugha asili. Hata hivyo, kauli zao kuhusu umuhimu wa lugha katika utambulisho wa vikundi ulinufaisha utafiti huu kwa kiasi kikubwa.

Angogo (1980), anatoa rai kuwa, hisia za wanachama wa kila kundi huwa kwamba, lugha yao ni nzuri, bora na yenye hadhi zaidi kuliko lugha nyingine. Haya ni mawazo yaliyojenga utafiti huu hususan katika kuchangia ari ya kutaka kujua hisia za wanafunzi kwa lugha zao, jambo ambalo huwa la msingi katika kubainisha mielekeo ya mtu.

Mesthrie (2001), anadai kwamba, uhusiano baina ya lugha na ukabila hueleweka vyema zaidi katika kiunzi cha ekolojia, yaani, kama uhusiano wa kimaingiliano kati ya mazingira ya kijamii na wazungumzaji wa lugha ambao umeunganishwa kimuundo katika mazingira hayo. Zaidi, anatoa rai kuwa, uhusiano huo, sio wa moja kwa moja na hutazamwa kupitia jinsi wazungumzaji wanavyotumia lugha kuakisi utambulisho wa kikabila.

Katika kutathmini umuhimu wa lugha, Fishman (1970), anadai kwamba, lugha haitumiki tu kama kifaa cha mawasiliano na kujieleza; uteuzi na matumizi ya aina fulani ya lugha ni ishara ya utambulisho wa mzungumzaji.

Zaidi, jinsi ambavyo lugha hiyo inavyotumika kupitia matamshi, muundo wa kisintaksia pamoja na msamiati, haurejelei uwanachama wa wazungumzi kwa kundi kabila bali hueleza dhana muhimu za kitamaduni. Ingawa matumizi ya lugha fulani hayalazimu kuwa sehemu muhimu ya utambulisho wa kikabila, yaweza kuonyesha kwamba, ambapo lugha ina hadhi ya kiishara kama hiyo, kuna uhusiano wa karibu baina ya utambulisho wa mzungumzaji na kundi kabila

Kuhusiana na swala la kujinasibisha na mtu akiwa Mhindi badala ya Mwingereza, Mercer (1979), aligundua kwamba, kiasi cha utambulisho wa mtu akiwa Mhindi badala ya Mwingereza, kilihusiana kichanya na matumizi na udumishaji wa Kigujerati. Lowley (1983), akitafitia wawakilishi wa kiethnoisimu wa vikundi vitatu vya Marekani; Wafaransa, Wahispania na Wayiddish, aligundua kwamba, vikundi hivi vilitamani kudumisha utambulisho wao wa kikabila pamoja na utambulisho wao wa Kimarekani. Hata hivyo, utambulisho ule wa kikabila ulibainika kuwa muhimu zaidi. Utafiti huo wa Lowley ulikuwa muhimu katika utafiti huu, hususan katika kuchunguza iwapo kuna uhusiano wa matokeo yake kule Marekani na matokeo ya utafiti huu hapa nchini Kenya.

San Antonio (1987), katika Giles na wengine (1980), alitathmini lugha inayotumika kama utambulisho wa kiethnoisimu katika utafiti wake wa mawasiliano baina ya vikundi katika shirika la Marekani huko Japan. Alibainisha kwamba, wafanyikazi wa Kijapani walitumia lugha ya Kiingereza na hapo kuashiria utambulisho unaodaiwa wa kuwa Mjapani ambaye Wamarekani wa Kaskazini wangepanya kazi naye. Hii iliongeza hadhi yao katika shirika. Wafanyikazi ambao walikuwa na ufasaha wa Kiingereza, 'waliwakinga' wenzao ambao hawakuongea Kiingereza vizuri katika mikutano kwa kujibu maswali ya Wamarekani.

Ryan, Hustone na Giles (1984), walifafanua kauli zao Giles na Ryan (1982), na kudai kwamba, utathmini wa wazungumzaji au watumizi wa lugha ni uamilifu wa: -

1. Muktaba wa muundo wa kijamii kama vile, usanifishaji au uwastanishaji na nguvu za lugha.
2. Hali halisi na ya papo hapo ya kijamii kama vile, maeneo au milki yake na kiwango cha urasmi.
3. Watumizi au wazungumzaji lugha wenyewe kwa mujibu wa sifa za kiisimu za lugha, mielekeo ya mtu au kundi na maudhui yaliyomo katika ujumbe.

2.2.6 Lugha na Utambulisho

Schiffman (1996), anatoa rai kuwa, lugha huwapa watu utambulisho, ni chombo cha uzoefu wa utamaduni wa kigeni. Basi, uteuzi wa lugha ya kutolea mafunzo na maingiliano, ni muhimu katika ukuaji wa watu. Hata hivyo, ingawa maoni ya mtafiti huyu yalikuwa changamoto katika utafiti uliofanywa, nchini Kenya, hali iliopo inaakisi jamii isiyo na lugha moja ya jumla. Yaani, watu wanaoshikilia heba za kikoloni za kutumia Kiingereza na kupuuza lugha zao za kiasili. Hata ikiwa lugha ya Kiingereza inaonekana kama lugha inayopunguza utata wa lugha katika taifa la Kenya, hali hii ni tatizo kubwa kwani, utambulisho wa kitaifa wa watu hauwezi kubadilishwa. Kama anavyodai Abdulaziz (1982) kuwa, "Elimu lazima itaifishe watoto na iwape hisi ya utambulisho wa kitamaduni wa jumla unaolingana na maadili ya kitaifa."

Utambulisho wa kitamaduni wa Wakenya uko ndani ya lugha zao, utamaduni na historia yao. Kutokana na dhana hizi, yafaa kuibuliwe maadili ya kitaifa. Uteuzi wa lugha ya kati kisiasa (lugha ya Kiswahili) ni mwanzo tu wa kutimiza maadili haya ya kitaifa (Whiteley 1974), "*Nahisi kuwa nina jukumu muhimu kama mzazi kuwapa watoto wangu nilichopewa na mamangu. Zawadi isiyothaminika-lugha asili, lililo muhimu zaidi ni kuwasaidia wanangu kuwa na ustadi wa Kikikuyu na kujua utambulisho wao wa Kiafrika na watu wao*" (Whiteley 1974), akimnukuu mama wa asili ya Kikikuyu. Nukuu hili, linabainisha imani ya mama huyu kuwa, lugha ni ala muhimu katika utambulisho wa wanawe, na kwamba, ujuzi wa usuli wao wa kitamaduni, ni sehemu muhimu ya kujistahi. Haya ni madai yaliyochangia pakubwa utafiti wa tasnifu hii.

2.3 Misingi ya Nadharia.

Katika kufanya utafiti, mtafiti aliongozwa na nadharia mbili: Nadharia ya Kitendo Kilichofikiriwa na Nadharia ya Utambulisho wa Kiethnoisimu.

2.3.1 Nadharia ya Kitendo Kilichofikiriwa

Nadharia ya kitendo kilichofikiriwa iliasisiwa na Fishbein na Ajzen (1975: Ajzen na Fishbein 1980). Msingi wa nadharia hii ni maelezo ya Bogardus (1931) na Allport (1935) katika Stuart (1991) kwamba:


Mwelekeo ni uelekeo au namna ya tabia kuhusiana na au dhidi ya kitu katika mazingira, ambapo panakuwa na mwelekeo chanya au hasi (Tafsiri yangu) Bogardus (1931).

Mwelekeo ni hali ya kuwa tayari kimawazo ambayo imeratibishwa kupitia tajiriba, inayotoa athari ya moja kwa moja au athari inayobadilika badilika kwa mwitikio wa mtu kuhusu vitu vyote na hali zote zinazohusiana (Tafsiri yangu) W.Allport (1935).

Nadharia ya kitendo kilichofikiriwa ina misingi yake katika uwanja wa saikolojia ya jamii. Awali, katika miaka ya 1862, Wanasaikolojia walianza kubuni nadharia zilizosawiri jinsi mielekeo inavyoathiri tabia na vitendo. Nadharia hizo za wakati huo, zilitoa rai kuwa, mielekeo ingeweza kueleza tabia na vitendo vya watu. Nadharia ya kitendo kilichofikiriwa iliendelezwa mwaka wa 1967. Wakati wa miaka tangulizi ya 1970, nadharia hii iliangukiwa upya na kupanuliwa na Ajzen na Fishbein. Waasisi hawa walichukulia kuwa, watu huwa razini na hutumia mfumo taratibu wa habari wanazopata. Mbali na hayo, kwamba, watu hutathmini matokeo ya vitendo vyao kabla ya kuamua kutenda au kutotenda. Kufikia mwaka wa 1980, nadharia hii ilitumika kutafitia tabia za watu. Mwaka wa 1988, nadharia ya tabia iliyopangwa iliongezwa katika kielelezo msingi cha Nadharia ya Kitendo Kilichofikiriwa ili kutatua tatizo lililokuwa limetambuliwa na waasisi hawa. Katika miaka hii ya kuasisiwa kwa nadharia hii, mambo mawili yalikuwa na ushawishi mkubwa katika kuelewa uhusiano uliopo kati ya mielekeo na vitendo au tabia.

1. Mwaka wa 1929, L. L. Thurston alizua mbinu ya kupima mielekeo kutumia vipimo vya nafasi baina ya vituo vilivyopelekea kubuniwa kwa mfumo maarufu wa mizani ya Likert
2. Mwaka wa 1935, G. W. Allport, alinadhariisha kuwa, mielekeo hutazamwa kama mfumo changamani inayoundwa na dhana tatu kuu. Hizi ni: imani za mtu kuhusu kitu, hisia zake kwa kitu hicho na mwelekeo wake wa vitendo kwa mujibu wa kitu hicho.

Kielelezo cha Nadharia ya kitendo kilichofikiriwa



Asili: Ajzen, A., na Fishbein, M. (1980).

Nadharia hii ina makisio matatu, Ajzen na Fishbein (1980): Kwanza, wanadamu huwa razini na hutumia mfumo taratibu wa habari wanazozipata. Pili, watu hutathmini matokeo ya vitendo vyao kabla ya kuamua kujihusisha au kutojihusisha na vitendo vyao.

Tatu, kuwa, vitendo vya mtu huamuliwa na nia yake ya kutenda kitendo hicho. Nia hii ni tokeo la mielekeo kwa kitendo hicho na imani kuhusu nini wengine watafikiria kuhusu kitendo fulani.

Kwa mujibu wa makisio hayo, nadharia hii ina misingi yake katika msisitizo kwamba, binadamu hutenda jambo kwa misingi ya imani zake na habari anazozipata. Inashikilia kwamba, makusudio ya tabia ya binadamu, huwa kiashiri bora cha jinsi atatenda, na kwamba, makusudio hayo yaweza kubashiriwa kwa kujua mielekeo na imani ya mtu. Nadharia hii ya mielekeo hushikilia kwamba, vitendo vyote vyenye umuhimu wa kijamii hutawaliwa na matarajio ya mtu mwenyewe ambapo, anaamua kutenda au kutotenda jambo hilo. Nadharia hii inapiga hatua zaidi na kutambua kwamba, binadamu ana uwezo wa kifikra na huweza kutumia kwa utaratibu habari anazozipata; kwamba, watu hukadiria matokeo ya vitendo vyao kabla ya kuamua kujihusisha au kutojihusisha na vitendo fulani.

Giles na Johnson (1981) na Agheyisi na Fishman (1970) wanatambua kwamba, mielekeo ina uhusiano na vitendo kwa sababu, vitendo vya binadamu ni njia moja muhimu ya kudhihirisha mielekeo yake kuhusu kitu au swala fulani. Ajzen na Fishbein (1980:90), wanaunga wazo hilo mkono na kudai kwamba, makusudio ya tabia fulani (k.v. kuteua somo fulani au hali fulani), ni matokeo ya dhana mbili;

- (i) Mielekeo ya mtu kwa tabia hiyo inayoongozwa na mambo ya kibinafsi hasa jinsi mtu anovyosawiri kutenda jambo hilo aidha ni zuri au ni baya.

Jambo hili ndilo humpa mtu mwelekeo wake kuhusu kitendo chenyewe kama atakipendelea au kutokipendelea.


- (ii) Kaida za kidhahania kuhusu nini jamii inafikiria afaa afanye. Yaani, athari za kijamii kwa ambavyo inamtarajia kutenda au kutotenda jambo fulani. Hali hii ya kupenda au kutopenda ndiyo hufahamika kama mwelekeo kuhusu jambo

Kuhusiana na dhana hizi, Fishbein na Ajzen (1980) wanasema: “Kwa kawaida watu hutarajia kutenda jambo baada ya kulitathmini na kulipenda na wanapoamini kuwa watu wengine muhimu na mashuhuri katika jamii wanafikiri mtu huyo anapaswa kulitenda jambo hilo”. Zaidi, wanadai kuwa, katika nadharia hii, mielekeo ya mtu kwa tabia fulani huhusu imani kuwa tabia fulani huelekeza katika matokeo fulani. Ikiwa matokeo yana mwegemeo wa kuwa na faida kwa mtu, basi anaweza kukusudia kujihusisha na tabia hiyo. Sheria zinazozua kitendo au tabia fulani zinaweza kuwa na athari kwa mielekeo ya mtu katika kujihusisha na kitendo hicho.

Aidha, nadharia hii imesitiza kuwa, mielekeo ina muundo wa kimsingi wa kinadharia unaoshirikisha vijenzi vitatu (Stuart 1991:8-9). (*Tafsiri yangu*) Vijenzi hivi ni:-

1. Kijenzi cha sehemu ya kifikra ambacho huhusu mawazo na imani aliyonayo mtu kwa hali, mtu au kitu fulani. Kwa mfano, *lugha ya Kiswahili ina manufaa sana*. Basi kulingana na kijenzi hiki, mielekeo ni matokeo ya imani. Kwa kawaida, mtu anayeamini kuwa kutenda jambo fulani kutaleta matokeo mema, atakuwa na mwelekeo mwema juu ya kutenda jambo hilo (Ajzen na Fishbein 1980).
2. Kijenzi cha hisia ambacho hurejelea hisia na mihemuko ambayo mtu anayo kwa hali, mtu au kitu kwa mfano: *Sipendi lugha ya Kiswahili*.
3. Kijenzi cha kitabia ambacho huhusu vitendo vya mtu kwa hali, mtu au kitu fulani. Kwa mfano: *Kamwe situmii lugha ya Kiswahili katika chuo kikuu*. Kijenzi hiki, kinawiana na msimamo wa Fishman na Agheyisi (1970), katika Tchai (1991:12), kuwa, mielekeo inaweza kujulikana kwa kuchunguza na kuangalia vitendo vya watu katika miktadha ya kijamii.

Pia kwamba, vitendo vya kijamii vya mtu, viwe vitendo vya kidini, kiuchumi, kisiasa au kibiashara, vyote hutawaliwa na kuongozwa na mielekeo yake. Vijenzi hivi vyaelekeza katika maoni ya Edwards (1985), kwamba, kawaida mtu anapaswa kupata ufahamu na kujenga imani kuhusu kitu, hali au mtu fulani, kisha hisia za mwitikio na kubaini tabia maalum ya kitu, hali au mtu huyo.



Asili: Stuart (1991: 9)

Nadharia ya kitendo kilichofikiriwa ilifaa utafiti huu hususan ikichukuliwa kuwa uteuzi wa lugha moja badala ya nyingine ni kitendo ambacho kwanza kinafikiriwa na kutathminiwa kabla ya kutendwa. Basi, iliongoza utafiti kwa mujibu wa jinsi kitendo cha kuteua na kupendelea lugha moja badala ya nyingine hutawaliwa na imani aliyonayo mzungumzaji kuhusu lugha hiyo na kwamba, imani hii ndiyo inayoiongoza mielekeo yake kwa lugha ambayo hutawala vitendo vya kutumia lugha moja badala ya nyingine.

2.3.2 Nadharia ya Utambulisho wa Kiethnoisimu

Mvuto wa ushikamano uliopo kati ya lugha na utambulisho, ulipelekea kubuniwa na kuendelezwa kwa nadharia hii (Beebe na Giles 1984; Giles na Johnson, 1981; 1987). Nadharia hii, inahusisha vidokezo vya nadharia ya utambulisho wa kijamii (Tajfel na Turner 1979), na, nguvu-tendi za kiethnoisimu, inayoshikilia kuwa, vikundi vya kikabila hunuia kuwa na tofauti za kisaikolojia na makundi ya nje kwa kutumia lugha kama namna ya ulinganisho na vikundi hivi. Kwa kuwa watu kawaida ni wanachama wa makundi kabila tofauti, ni kupitia lugha ambapo vikundi hivi hujitokeza kiwazi (Giles na Johnson 1987).

Nadharia hii iliasisiwa kueleza dhana ya ni nani katika kundi kabila atatumia lugha ipi, mikakati ipi ya lugha, lini na kwa nini katika mawasialiano baina ya makundi kabila. Msingi wa nadharia hii ni maelezo ya waasisi wake Giles na Johnson (1981), katika Giles na Johnson (1990), kwamba: - lugha inatekeleza angalau majukumu manne ya kinafsia kulingana na ukabila.

1. Ishara ya uwanachama. Kwamba aina fulani ya uzungumzi au matumizi ya lugha fulani ni ishara ya uwanachama wa kundi fulani la kikabila.
2. Kidokezo cha uainisho. Kwamba ni kidokezo muhimu cha uainisho baina ya makabila.
3. Utambulisho. Kwamba ni dhana muhimu ya utambulisho wa kikabila.
4. Ushikamano. Kwamba ni chombo muhimu cha kurahisisha ushikamano ndani ya vikundi.

Giles na wengine walipiga hatua zaidi na kuasisi kwamba, makundi kabila yanaweza kulinganishwa kwa mujibu wa nguvu-tendi za kiethnoisumu ambazo kwazo, dhana tatu kuu muhimu huchangia. Hizi ni:-

1. Dhana za kauli kama vile ufahari wa kiuchumi, kisiasa na kilugha.
2. Dhana za kidemografia kama vile idadi kamili ya wanajumuiya, mkusanyiko wa watu katika eneo la kijeografia n.k.

3. Dhana ya kuungwa mkono na taasisi mbalimbali kama vile, kutambuliwa kwa kundi na pia lugha yao na vyombo vya habari, katika elimu na serikali.

Hizi ni hoja zilizochangia pakubwa katika utafiti kwa sababu, kwa mujibu wa wingi idadi wa kundi kabila fulani, na pia kutambuliwa kwa lugha ya kundi hilo katika vyombo vya habari, kuliwezesha utafiti kumaizi jinsi dhana hizi zinavyochangia katika uteuzi na matumizi ya lugha katika vyuo vikuu nchini Kenya. Hususan hoja hizi, ziliongoza utafiti katika kushughulikia kauli za kusikiliza na kusoma magazeti kwa wanafunzi katika lugha mbalimbali.

Nadharia hii pia inapiga hatua zaidi na kutoa madai kuwa, watu hufasiri mawasiliano kwa misingi ya kikabila na kung'ang'ania utambulisho chanya wa kikabila kwa kutilia mkazo lugha yao au namna yao ya maongezi. Hii ilikuwa ni hoja muhimu katika kushughulikia ule muktadha ambapo wasailiwa wanashirikiana na wenye duka wa kabila lao na wale wasio wa kabila lao. Zaidi, katika maingiliano baina ya wasailiwa na washiriki wasio wa kundi-kabila lao katika miktadha mingine iliyoshughulikiwa. Nadharia hii pia huchota kutoka kwa nadharia ya utambulisho wa kijamii ambayo inashikilia kuwa: - watu hugawa ulimwengu na hivyo kujiona kama wanachama wa vikundi mbalimbali. Utambuzi huu ndio hufahamika kama utambulisho wa kijamii na waweza kuwa chanya au hasi.

Giles na wengine (1990), walifafanua nadharia hii na kuiunganisha na mielekeo na motisha wa wanachama wa kundi tawala na kundi tawaliwa. Kwa mujibu wa nadharia hii, utafiti wa McNamara (1987), katika Giles na wengine (1990), uligundua kuwa, mabadiliko katika utambulisho wa kijamii huandamana na mabadiliko katika mielekeo ya lugha inayopendelea lugha moja kuliko nyingine. Hizi zilikuwa hoja muhimu katika utafiti huu haswa katika mielekeo kwa lugha na lugha za kundi lingine la kikabila.

Nadharia hii aidha inadai kwamba, wazungumzaji watafasiri maingiliano kwa misingi ya kikabila husan kabila la ndani na wapambanie utambulisho wa kundi kikabila ulio chanya kwa kutilia mkazo aina fulani ya uzungumzi au lugha mahususi. Zaidi inaasisi kwamba, utambulisho wa kijamii na mtazamo wa nguvu za kiethnoisimu huathiri mahusiano baina ya vikundi na mwelekeo kwa lugha kuu. Nchini Kenya, lugha kuu ni Kiingereza na Kiswahili ambazo zilikuwa uti wa utafiti huu. Nadharia hii inabainisha mitazamo miwili mahususi ambayo hutumiwa kutathmini hali na uteuzi wa lugha: -

1. Mtazamo unaohimiza hadhi au umoja.
2. Mtazamo unaohimiza ubinafsi wa mtu binafsi au ubinafsi wa kikundi.

Nadharia hii inafafanua mitazamo hii na kudai kwamba, katika hali ambazo mtazamo unaohimiza umoja au ubinafsi wa kikundi unatawala matumizi ya lugha, watu hutofautiana kilugha na wanachama wa kundi la nje. Iwapo mtazamo unaosisitiza hadhi au ubinafsi wa mtu binafsi unatawala, watu huungana kilugha na wanachama wa kundi la nje. Hii ilikuwa mitazamo ya kati katika utafiti huu na ilirutubisha na kuongoza utafiti huu. Umuhimu mwingine wa nadharia hii ni kuwa inashirikisha athari za muundo wa kijamii kwa makundi kabila yaliyo katika mtagusano na jinsi makundi haya hutazamwa na wanachama wake.

SURA YA TATU

MBINU ZA UTAFITI

3.1 Utangulizi

Sura hii inawasilisha mbinu za utafiti zilizomwezesha mtafiti kutekeleza utafiti. Hizi ni pamoja na: mfumo wa utafiti, jumuiya, sampuli na uteuzi wa sampuli, vifaa vya utafiti, ukusanyaji wa deta na uchanganuzi wa deta.

3.2 Mbinu za Utafiti

Utafiti ulifanyika nyanjani katika chuo kikuu cha Egerton- bewa la Njoro. Utafiti wa nyanjani ulifanywa ili kupata habari mahususi na zinazohusiana na ruwaza za matumizi ya lugha katika vyuo vikuu. Sababu ya utafiti kujikita katika chuo hiki ilikuwa kumwezesha mtafiti kutekeleza mbinu ya uchunguzi shiriki bila kuamsha hisia zozote kwa watafitiwa kwani alikuwa mmoja wa wanafunzi wa chuo hicho. Utafiti uliangazia matumizi ya lugha miongoni mwa wanafunzi katika hali zisizo rasimi kama vile katika starehe zao, katika shughuli zao za ununuzi chuoni, wanafunzi wakiandamana kwenda kuhudhuria mihadhara n.k.

Maoni, hisia na imani za wanafunzi wa chuo hicho kwa lugha wanazozitumia kila siku yalizingatiwa. Mbinu ya kiethnografia inayohusisha uchunguzi shiriki na hojaji ilitumika katika kukusanya deta. Uchanganuzi wa deta ulifanywa kwa njia ya mtindo wa kitarakimu wa tarakilishi. Matokeo ya uchanganuzi yaliwekwa katika jedwali za maratokezi na asilimia na kutolewa ufafanuzi.

3.3 Uteuzi wa Wahojiwa

Utafiti ulikusudia kutambulisha mielekeo na ruwaza za matumizi ya lugha miongoni mwa wanafunzi wa chuo kikuu cha Egerton. Kutokana na tofauti za wanafunzi kwa misingi ya asili zao za lugha na maeneo, ilikuwa muhimu kuwaweka wanafunzi katika vikundi vya kiwilaya kupitia orodha ya vikundi hivi iliyopo katika ofisi ya mshauri wa wanafunzi. Vikundi vya kiwilaya vya wanafunzi chuoni, viliorodheshwa kama hatua ya mwanzo ili kujua ni vingapi. Mathalan ilibainika kuwa, kuna vikundi vya aina hii hamsini na tatu. Kwa kuwa kuna vikundi vya kiwilaya vya wanafunzi kutoka mkoa mmoja ingawa vinawakilisha lahaja tofauti za lugha moja, vikundi hivi viliwekwa pamoja na kuwa kundi moja.

Sababu ya kufanya hivi ilikuwa ni ili kushirikisha vikundi ambavyo vina deta muhimu. Hatua ya pili ilikuwa ni kuwateua washiriki wa utafiti. Wanafunzi tisini waliteuliwa kwa njia iliyoazimiwa kutoka kwa vikundi hivyo. Wanafunzi hawa walikuwa ni wa mwaka wa kwanza hadi wa nne na kutoka vitivo vyote chuoni hicho. Aidha, walikuwa ni wa uana wa kiume na kike. Sampuli hii iliteuliwa kwani, kulingana na Milroy (1987), kundi ndogo la sampuli humwezesha mtafiti kupata habari za kina kuhusiana na mada ya utafiti.

3.4 Vifaa vya Utafiti na Ukusanyaji Deta

Mtafiti alitumia vifaa viwili mahususi katika utafiti huu: Hojaji na uchunguzi-shiriki. Kulikuwepo na hojaji moja tu (Kiambatisho A) iliyokuwa na maswali funge na wazi ili kuwaruhusu washiriki kutoa habari nyingi. Washiriki hawa, walipewa hojaji hiyo wajaze kibinafsi kwa kuandika katika hojaji hiyo. Baadaye, hojaji zilikusanywa na kusahihishwa. Hojaji hiyo ilishirikisha maswali 21 yaliyokuwa na hali tisa muhimu katika utafiti huu. Swali la kwanza lilitafiti kuhusu makundi kabila chuoni na mkusanyiko wa lugha. Swali la pili lililenga kutambulisha kuridhika kwa wanafunzi katika kutumia lugha zilizoshirikishwa katika utafiti katika hali mbalimbali. Jinsi ya kuzungumza lugha ilibainishwa na swali la tatu. Maswali ya nne, kumi na moja, kumi na mbili, kumi na tatu, kumi na nne na kumi na tano yalitumika katika kugundua ruwaza za matumizi ya lugha katika maeneo mbalimbali.

Katika sehemu ya sita, lugha ya matumizi mahususi ilitafitiwa kwa kutumia swali la tano, sita, saba na kumi na sita. Katika kubainisha utambulisho wa kiethnoisimu, swali la nane, tisa, kumi na moja, kumi na mbili na kumi na tano yaliwekwa katika sehemu ya saba. Kufuatia mapendekezo ya Martinelli (1984), ili kupima kiwango cha utambulisho wa wasailiwa, mizani ya utambulisho wa kikabila ilibuniwa ikiwa na peo tatu: situmii, chache, nyingi ili kuweza kuafiki lengo hilo. Hali ya kuchanganya lugha na kiasi cha kuchanganya lugha ilikuwa katika sehemu ya nane na ikawakilishwa na swali la kumi. Swala la mielekeo ya wanafunzi kwa lugha lilikuwa la sehemu ya tisa na lilibainishwa na swali la kumi na saba hadi la ishirini na moja.

Kisha, kitabu maalumu cha kodi kilitengenezwa kwa mujibu wa kanuni za mtindo wa kitarakimu wa tarakilishi. Kila swali lilikodiwa na kila kbadala katika kila swali kilipewa thamani. Kwa kutumia majibu na maelezo ya wahojiwa, utafiti huu uliweza kubainisha kwa urahisi jinsi ukabila na mielekeo huathiri uteuzi wa lugha itakayotumika na wanafunzi chuoni na kuweza kubainisha ruwaza za matumizi ya lugha chuoni miongoni mwa wanafunzi.

Uchunguzi shiriki ulitekelezwa ili kuyapa ithibati majibu ya hojaji. Mbinu ya uchunguzi shiriki ni mbinu ya kujiunga na watu na kushiriki huku mtafiti akiangalia mambo muhimu yanayohusiana na mada tafitiwa (Seliger 1989). Kulingana naye, mbinu hii huwa mwafaka katika kukusanya habari ambazo hazionekani kirahisi kama vile, mielekeo na dhana za kibinafsi. Pia, hutumika kukusanya deta kuhusu mfumo unaotumika katika kutumia lugha na kupata usuli wa habari za wahusika kama vile umri, idadi ya lugha wanazozungumza n.k. Uzito mkubwa uliofanya mbinu hii iteuliwe, ni kwamba, kwa kuwa hojaji huwa sawa kwa kila mshiriki, deta inayopatikana huwa sare na ya aina moja. Mbali na hayo, kwa kuwa hojaji hizi hupewa washiriki wote kwa wakati mmoja, deta huwa sahihi zaidi. Mtafiti alijiunga na wanafunzi katika miktadha mahususi iliyoteuliwa.

Miktadha minane inayohusisha hali zisizo rasmi iliteuliwa kwa njia iliyoazimiwa. Miktadha hii ni pamoja na vyumba vya kulala, vya maakuli, vikundi vya wanafunzi wanapoota jua, dukani, misafara ya kwenda kuhudhuria mihadhara, uwanjani, ukumbi wa kuigizia na sherehe za dhifa za wanafunzi chuoni. Mtafiti alijiunga na wanafunzi na kushiriki nao katika matumizi ya lugha huku akiangalia jinsi lugha inavyotumika katika miktadha hiyo mahususi. Mtafiti aliratibu na kunakili mambo muhimu na hali halisi ilivyo katika kitabu maalum kuthibitisha majibu ya hojaji.

3.5 Uchanganuzi wa Deta

Deta ya utafiti huu ilikuwa ni hojaji zilizojazwa na kusahihishwa pamoja na mambo muhimu yaliyonakiliwa katika uchunguzi shiriki. Maswali katika hojaji yalikuwa takriban maswali 21 ambayo yaliaminika majibu yake, yalisawiri jinsi ukabila na mielekeo ya wanafunzi huathiri uteuzi na matumizi ya lugha katika vyuo vikuu. Jumla ya hojaji sabini na tatu zilirejeshwa kusahihishwa. Baada ya deta hii kupokelewa, ilichunguzwa kwa makini kuwezesha kuafikia madhumuni ya utafiti. Kisha, yalisahihishwa na kila swali lilikodiwa na kila kibadala katika kila swali kupewa thamani kulingana na kanuni za mtindo wa kitarakimu wa tarakilishi.

Majibu kwa kila swali yaliwekwa katika kundi na kuorodheshwa. Baadaye, deta hii iliingizwa katika tarakilishi tayari kwa uchanganuzi. Hii ilizua takwimu muhimu zilizotumika kueleza deta iliyowasilishwa na kuelezwa katika sura ya nne. Mbinu ya takwimu elezi ilitumika katika kupata maratokezi na asilimia. Uchanganuzi wa deta ulikuwa ni wa takwimu elezi.

Matokeo yalitolewa kwa njia ya jedwali na kufasiriwa na kutolewa maelezo kila baada ya jedwali. Asilimia na majedwali yalitumika kurahisisha uchanganuzi. Majibu ya hojaji nambari 18 hadi 21 kimahususi yalituzwa alama kulingana na mfumo wa upendelevu ulioasisiwa na Likert kama anavyoeleza Stuart (1991). Swali hupewa majibu matano. Kila jibu huonyesha kiwango cha kukubaliana au kutokubaliana. Majibu hutuzwa alama 1 – 5. Katika utafiti huu, majibu yalituzwa alama kwa kutumia mfumo huu. Swali la 18- 21, alama zilituzwa ifuatavyo: -

Nakubali kabisa	(5)	Sikubali	(2)
Nakubali	(4)	Sikubali kabisa	(1)
Sina uhakika	(3)		

Nayo maswali kuanzia swali la kwanza hadi la kumi na saba, mfumo huo huo ulitumiwa ambapo kila kabadiliki kilikodiwa na kupewa thamani kwanzia kiwango cha chini (alama 1) hadi cha juu sana (alama 10) kwa mujibu wa swali. Kutokana na majedwali ya matumizi ya lugha, lugha inayotumika na asilimia kubwa zaidi ilizingatiwa ili kutafuta lugha maarufu ya wahojiwa wote ili kuweza kuonyesha umaarufu wa lugha na lugha itumikayo zaidi kwa jumla. Majedwali yalitumiwa kuyaratibu majibu na matokeo.

SURA YA NNE

JINSI UKABILA NA MIELEKEO YA WANAFUNZI INAVYOATHIRI UTEUZI NA MATUMIZI YA LUGHA KATIKA VYUO VIKUU

4.1 Utangulizi

Sura hii inajadili matokeo ya jinsi ukabila na mielekeo ya wanafunzi inavyoathiri uteuzi na matumizi ya lugha katika vyuo vikuu kwa kulenga chuo kikuu cha Egerton. Misingi ya sura hii ni matokeo ya utafiti uliofanywa kwa muda wa miezi minane. Ili kuweza kujadili matokeo haya, sura hii imegawika katika sehemu nne. Kwanza ni sehemu inayojadili jumuiya ya wanafunzi chuoni. Pili ni sehemu inayojadili mielekeo ya wanafunzi ilhali katika sehemu ya tatu ruwaza za matumizi ya lugha zimejadiliwa. Sehemu ya nne ni hitimisho ambalo ni muhtasari wa wa sura hii kwa ujumla.

4.2 Jumuiya ya Wanafunzi Chuoni

Katika utangulizi, utafiti ulikisia kwamba, jumuiya ya wanafunzi huwa ni muungano wa makabila mbalimbali. Kiini cha kisio hili ni ukweli kwamba kamati inayowateua wanafunzi baada ya kuhitimu katika kidato cha nne haibanwi na misingi ya kikabila. Kila anayehitimu huwa na nafasi sawa ya kupewa mwaliko wa kujiunga na chuo kikuu chochote kile. Linalodhihirika hapa basi ni kwamba, jumuiya hii ni yenye lugha nyingi kadri yalivyo makabila nchini Kenya.


Ilibainika kuna takriban makabila 16 yaliyopo chuoni yanayoishi, kuingiliana na kushirikiana katika shughuli mbalimbali chuoni. Hii ni sababu moja ya kuwepo wingi lugha katika vyuo vikuu. Sababu hii yaweza kufafanuliwa kutokana na ukweli kwamba angalau kila kabila lingependa kutumia lugha yake. Kutokana na washiriki walioshirikishwa, ilithibitika kuwa, kuna tofauti za kiidadi za wanafunzi. Kwa mujibu wa nadharia ya utambulisho wa kiethnoisimu, idadi ya wazungumzaji lugha huwa muhimu kwani ni dhana moja inayochangia katika nguvu-tendi za kiethnoisimu (Giles na Johnson 1987). Katika daraja hii ya masomo, kuna idadi kubwa ya Wakikuyu, Wakalenjin, Wakamba, Waluo, Wataita na Wakisii. Mathalan kundi kabila la Wakikuyu liliwakilisha asilimia 15.1 ya wasailiwa wote ilhali makundi ya Wakalenjin, Wakamba yaliwakilisha asilimia 9.6 ya wasailiwa kila moja.

Wingi wa wanafunzi wa kundi kabila la Wakikuyu laweza kufafanuliwa kwa misingi ya wingi wa idadi yao katika taifa la Kenya. Kundi kabila hili ni kundi lililo na wanajamii wengi zaidi ya makundi kabila mengine nchini. Aidha, ni kundi lenye uwezo mkubwa kisiasa na kiuchumi likilinganishwa na makundi mengine.

Jedwali 1. Asili: takwimu za utafiti 2005

**Makundi Kabila ya wanafunzi
chuoni**

Kabila	Maratokezi	Asilimia
Kikuyu	11	15.1
Kamba	7	9.6
Kalenjin	7	9.6
Luo	6	8.2
Taita	6	8.2
Kisii	6	8.2
Luhya	5	6.8
Kuria	5	6.8
Meru	5	6.8
Embu	4	5.5
Turkana	3	4.1
Somali	3	4.1
Rendile	2	2.7
Maasai	1	1.4
Giriama	1	1.4
Chonyi	1	1.4
Jumla	73	100.0



Hatua ya pili ilikuwa ni kuchunguza mgao wa washiriki kulingana na kigezo cha uana. Uhalisia wa tofauti za kiuana katika ngazi zote za elimu nchini Kenya ulidhihirika kutokana na washiriki walioshirikishwa. Ni bayana kuwa, wanaume ni wengi kuliko wanawake. Ilibainika kwamba asilimia 54.9 ya washiriki walikuwa ni wanaume ilhali asilimia 45.1 walikuwa ni wanawake. Matokeo haya yana misingi yake katika hali halisi ya kijamii. Huenda sababu kuu ya hali kuwa hivi ni uhalisia wa sababu kongwe za kijamii. Kwa mfano, hadi sasa kuna baadhi ya jamii ambazo bado zinashikilia kuwa kuwapa binti zao elimu ni kupoteza mali yao kwani, baada ya kuelimika wataolewa na kwenda kuwafaidi waume zao na aila zao. Matokeo haya na sababu kama hizo zinathibitisha kuwa, tofauti za kiuana huenda zikazidi kujidhihirisha licha ya kuwa jinsia zote mbili zimo katika nyanja ya masomo


La muhimu ni kwamba wasailiwa walioshirikishwa ni anuwai kwa misingi ya kitivo, mwaka wa kiakademia, uana na kabila. Kwa hivyo, majibu waliyoyatoa kuhusiana na kauli za hojaji za utafiti yaliweza kuwakilisha wanafunzi wote chuoni. Pia, uwazi wa kazi hii hadi hapo unaakisi uhalisia kuwa, vyuo vikuu ni jamii lugha yenye wingi-lugha kadri makundi kabila yalivyo mengi.

4. 2.1 Idadi ya Lugha Wanazozungumza Wanafunzi

Baada ya kuhakikisha kuwa jamii ya vyuo vikuu huwa anuwai, mtafiti alipiga hatua kubainisha idadi ya lugha wanazozizungumza wanafunzi. Washiriki waliagizwa kutaja idadi ya lugha wanazozitumia kila siku na pia kuziorodhesha. Habari hizi zilikuwa ni muhimu ili kutoa picha halisi ya uteuzi wa lugha moja badala ya nyingine. Ni bayana kwamba, ili kuwe na uteuzi wa jambo au hali fulani, ni lazima kuwe na zaidi ya hali moja ya jambo hilo. Kwa kulenga idadi ya lugha, asilimia 70 katika sampuli iliyoteuliwa ilionyesha kwamba wengi wao hutumia lugha tatu katika kuwasiliana na wanafunzi wenzao (Jedwali 2, uk 35). Hizi ni pamwe na lugha asili, Kiswahili na Kiingereza. Mtindo huu unakubaliana na maoni ya Kaniu (2003:1), kuwa Wakenya wengi hutumia lugha tatu; hivyo, kuzua mfumo wa lugha tatu. Matokeo hayo yanawiana na matokeo ya Tchai (1991). Alifanya utafiti wake kule Malindi, na kugundua kuwa, asilimia kubwa ya wakaaji wa Malindi wanajua lugha tatu: - lugha asili, lugha ya Kiswahili na lugha ya Kiingereza. Takwimu za utafiti huu zilidhihirisha idadi ya wanafunzi wanaotumia lugha nne kuwa 20.5%, ilhali washiriki 6.8% lugha mbili na 2.7% inawakilisha idadi inayotumia lugha tano. Asilimia hizi ni za chini zikilinganishwa na 70%.

Jedwali la 2: Idadi ya lugha wanazozungumza wanafunzi

Idadi ya lugha	Mara tokezi	Asilimia
Mbili	5	6.8
Tatu	51	70
Nne	15	20.5
Tano	2	2.7
Jumla	73	100.0



Kundi lile la lugha tano na nne linadhihirisha kuwepo kwa lahaja ya sheng' miongoni mwa wanafunzi na vile vile kwamba kuna wanafunzi ambao wamejifunza zaidi ya lugha asili moja. Matokeo haya yanaakisi hali halisi ya matumizi ya lugha ya jumuiya nzima ya Kenya. Wakenya wengi hutumia lugha asili, Kiswahili na Kiingereza. Wengi waliosema kutumia lugha nne, walitaja lahaja ya Sheng' na Lugha asili ya jamii nyingine. Hata hivyo, hawa wanaokiri kutumia lugha nne na tano, ilibainika katika uchunguzi shiriki kuwa, ujuzi wao wa lugha hii ya juu ni wa kadri tu. Iithibitika kupitia matukio neni, kuwa wanafunzi wana ufahamu wa kuweza kutosheleza mawasiliano ya kimsingi tu. Hususan matukio neni yaliyoibuka katika matumizi ya lugha ya wasailiwa yalikuwa katika kuamkuana na kujuliana hali.

Ugunduzi huo unawiana kwa kiasi kikubwa na jinsi hali inavyokuwa mtoto anapojifunza lugha. Lyons (1968), kwa mfano anatoa kauli kuwa mtoto hujifunza msamiati wa lugha kulingana na mahitaji aliyonayo. Pia, jambo hili linaweza kuelezwa kwa mujibu wa dhana ya wanafunzi kutaka kujitambulisha na kundi fulani la kikabila na hivyo kuzua dhana ya kupata lugha ili kuonyesha umoja na kundi hilo. Juu ya hayo, historia ya makundi kabila haya inachangia pakubwa katika kueleza sababu za hali kuwa hivi katika vyuo vikuu kwani, mengi hudaiwa kuwa na asili moja. Makundi kama vile ya Wakikuyu, Wameru na Waembu, lugha asili zao zina ukuruba mkubwa sana na hivyo, kuna uwezo wa wanafunzi wa kabila la Kimeru kuweza kuzungumza Kikuyu na kinyume chake.

Hali ni hiyo hiyo kwa makundi kabila ya Wakisii na Wakuria. Pia, jambo hili linaweza kuelezwa kwa misingi ya kijamii hususan nyanja ya ndoa ikizingatiwa. Jamii tofauti siku hizi, zinaruhusu kuoana kwa wanajamii tofauti. Kizazi kinachozaliwa hata hivyo; licha ya kuwa na uwezo wa kutumia lugha asili zote mbili, hujimudu zaidi katika lugha ya Kiswahili.

4.2.2 Namna ya Kuzungumza Lugha.

Mtafiti aliazimu kujua namna wanafunzi wanavyozungumza kila mojawapo ya lugha hizo. Habari kuhusu jinsi wanafunzi wanavyozungumza lugha asili, Kiswahili, Kiingereza zilikusanywa. Habari hizi zilikuwa muhimu ili kuthibitisha ikiwa wanafunzi huteuwa lugha wanayoizungumza vyema. Mosi, utafiti ulichunguza namna wanafunzi wanavyozungumza lugha asili. Kwa kutumia kipimo cha upendelevu (Likert) (majibu mawili yalitumika: - vibaya au vyema.

Matokeo ni kama yanavyoonyeshwa na jedwali la tatu hapa chini. Asilimia 94.5 ya wasailiwa walisema kuwa wao huzungumza lugha asili vyema. Wanafunzi asilimia 5.5 wanaizungumza lugha hii vibaya. Hali hii yaweza kuelezwa kwa ubayana kwamba, Wakenya wengi bado hujivunia lugha asili zao na huzitumia kujitambulisha. Hata hivyo, matokeo haya yanakinzana na yale ya jedwali la sita ambapo takriban asilimia 73.6 ya wanafunzi walisema kwamba hawapendelei lugha hii inapotumika katika hali ya kuzungumza. Hali hii ya ukinzani kati ya hizi asilimia yaweza kufafanuliwa kwa kuzingatia muktadha wa chuo kikuu. Huu ni muktadha ambao hushirikishwa na ustadi na ujuzi wa kiusomi. Wanafunzi wengi huchukulia kuwa uwezo wa kutumia lugha ya Kiingereza unaafiki hali hii na ndiposa hawatumii lugha asili.

Jedwali la 3: Jinsi ya kuzungumza Lugha Asili

Namna	Maratokezi	Asilimia
Vibaya	4	5.5
Vyema	69	94.5
Jumla	73	100.0

Hali hii inaweza kufafanuliwa kuwa, lugha asili ndio lugha inayotumika katika muktadha wa nyumbani. Kwa kuwa wanafunzi huwa wametumia muda wao mwingi nyumbani, basi, huwa wameikuza lugha hii na pia kupata umahiri wa kuweza kuizungumza vyema.

Pili, licha ya kuwa katika chuo kikuu hakuna ushurutishaji wa lugha na kuna miktadha mingi inayoafiki matumizi ya lugha yasiyo rasmi, ni bayana kuwa, vyuo vikuu hunasibishwa na lugha ya kiusomi ambayo kwa kiasi kikubwa ni lugha ya Kiingereza na kwa kiasi kidogo lugha ya Kiswahili.

Katika kuchunguza namna ya kuzungumza lugha ya Kiswahili, asilimia 2.7 ya wasailiwa huzungumza vyema ilhali asilimia 97.3 ya wanafunzi huzungumza lugha hii vibaya. Matokeo haya yana uwiano na matokeo ya utafiti kuhusu kupendelea kutumia lugha hii katika hali mbalimbali. Kwa mfano, katika jedwali la nane (uk.43), asilimia 89 ya washiriki walijibu kuwa hawapendelei lugha hii katika kuandika ilhali ni asilimia 9.6 ya wasailiwa ambao walisema kuwa wanapendelea lugha ya Kiswahili katika kuandika. Katika upeo wa kuzungumza, ni asilimia 97.3 ya wanafunzi ambao walijibu kuwa wanazungumza Kiswahili vyema.

Kwa upande wa Kiingereza, asilimia 97.3 huzungumza lugha hii vyema. Wanafunzi asilimia 2.8 walikiri kuwa huzungumza lugha ya Kiingereza vibaya kama ilivyodhihirika. Kutokana na wakati na umuhimu unaopewa lugha hii katika shughuli nyingi za kila siku, wanafunzi hawana budi kuwa na stadi bora ya kuzungumza lugha hii. Jinsi wanavyokuwa na ustadi bora wa kuitumia, ndivyo wanavyoshawishika kuiteua na kuitumia. Mambo haya mawili (ustadi na uteuzi) yanaingiliana na kuchangia katika kuwa na mielekeo chanya kwa lugha ya Kiingereza. Kwa upande ule mwingine, mielekeo huweza kuchangia katika kukuza stadi kwani mielekeo huweza kuathiri kwa namna chanya au hasi kuteuliwa kwa lugha ili itumike.

Jedwali la 4: Jinsi ya kuzungumza Kiingereza

Namna	Maratokezi	Asilimia
Vibaya	2	2.8
Vyema	71	97.3
Jumla	73	100.0

Matokeo hayo yalibainisha viwango tofauti vya namna ya kuzungumza kila mojawapo ya lugha hizo. Kwa kurejelea waliokiri kuwa wao wanazungumza lugha vibaya, asilimia 5.5 walisema wanazungumza lugha asili vibaya; 97.3% huzungumza Kiswahili vibaya. Ni asilimia 2.8 pekee ya wasailiwa wote ambao huzungumza lugha ya Kiingereza vibaya. Hata hivyo, asilimia ya wanafunzi wanaozungumza lugha asili vibaya, inatofautiana.

Ni asilimia 5.5 pekee ya wanafunzi wanaoizungumza lugha hii vibaya. Matokeo hayo yanaweza kufafanuliwa kwa mujibu wa mielekeo chanya waliyonayo wanafunzi kwa lugha ya Kiingereza na lugha ya Kiswahili. Sababu nyingine ni ule muda unaotengewa lugha hizi na pia katika miktadha ambapo lugha hizi hutumika. Kwa upande wa Kiingereza, hii ndiyo lugha rasmi. Kiswahili kinatambuliwa kama lugha ya taifa. Kulingana na ukweli huu, inadhihirika kwamba hizi lugha mbili ndizo lugha zilizo na hadhi kuliko lugha asili na pia kutambuliwa hivyo katika katiba ya Kenya. Mbali na hayo, lugha hizi mbili zimefunzwa na kutiliwa mkazo katika shule.

Asilimia 5.5 ya wanafunzi ambao hawazungumzi lugha asili vizuri yaweza kuelezwa kwa mujibu wa mabadiliko ambayo yamezikumba jamii za kisasa. Vizazi vya kisasa vimezaliwa na kulelewa mijini ambapo lugha asili hazitumiki sana. Pia, wazazi wengi wameingilia shughuli za ajira na kuvifanya vizazi hivi visitangamane sana na wazee wao ambao huwa amali kuu katika kupitisha lugha asili. Pia kiwango cha kutumiwa kwa lugha asili kinadidimia kila uchao kutokana na mabadiliko ya jamii.

4.2.3 Kiasi cha kuchanganya lugha chuoni

Baada ya kuchunguza matumizi ya lugha katika maeneo maalum yaliyoteuliwa kuafiki malengo ya tasnifu hii, ililazimu kuchunguza na kujadili hali ya kuchanganya lugha. Uhalisia wa kuchanganya lugha ulifungua hamu ya kutaka kujua zaidi kuhusu hali hii katika vyuo vikuu. Hamu hii pia ilizuliwa na dhana kuwa, katika jamii yenye lugha nyingi, wanajamii wake huwa na ujuzi wa lugha mbili au zaidi, hata kama ni kwa viwango tofauti. Jambo hili huchangia wanajamii kuchanganya lugha kwa urahisi katika matumizi ya kila siku. Kuchanganya lugha ni matumizi ya lugha mbili au zaidi kwa pamoja. Hali hii hutokana na uwezo wa mzungumzi aliye katika mazingira ya wingi lugha kumudu lugha hizo kwa viwango takriban sawa. Lugha zilizo katika hali hii, huwa zinang'ang'ania nafasi ya kutumiwa na mara nyingi, hutokea ambapo zinatumiwa kwa pamoja kutekeleza jukumu la kuwasiliana.

Katika majedwali ya ruwaza za matumizi ya lugha, na mijadala iliyofuata majedwali hayo, ilibainika kuwa, mara kwa mara, wanafunzi huchanganya lugha katika shughuli zao za kila siku. Jedwali hizo pia, zilibainisha ni lugha zipi huchanganywa na pia ni asilimia ipi ya wanafunzi huchanganya lugha zipi katika maeneo yapi. Takriban asilimia 97.3 ya wanafunzi walikubali kuwa, wao huchanganya lugha katika mazungumzo yao. Ni asilimia 2.7 pekee ya wanafunzi ambao walisema kuwa wao hawachanganyi lugha.

Kwa mara nyingi, ilibainika kuwa, lugha asili, lugha ya Kiswahili, lugha ya Kiingereza na lahaja ya Sheng' huchanganywa kwa pamoja katika maeneo mbalimbali. Sababu za kuchanganya lugha, zinaweza kuzuliwa na ikiwa dhana fulani au kitu fulani kinapatikana katika lugha moja lakini hakipatikani katika lugha ile nyingine na basi, mshiriki anaweza kutumia lugha ile nyingine kueleza maana kwa kiasi fulani cha kileksia au cha kisarufi. Hali hii hata hivyo, hutokea ambapo lugha moja haina kabisa dhana hiyo. Sababu nyingine inayoweza kufafanua hali hii ya kuchanganya lugha ni, ikiwa dhana husika ni tata au isiyo wazi katika lugha moja, mzungumzaji anaweza kutumia dhana inayolingana na hiyo kutoka kwa lugha ile nyingine.

Sababu nyingine inayoweza kuoanishwa na kuchanganya lugha, ni uwazi uliobainika baada ya miktadha mbalimbali kutafitiwa na uhalisia wa matumizi ya lugha katika taifa nzima la Kenya kwa ujumla. Mazingira ambayo wazungumzaji wanakumbana nayo ni ya kuchanganya lugha; hivyo, wanafunzi wa vyuo vikuu wanazungumza kwa namna hiyo hiyo kwa vile ni kama desturi ya jamii hii. Hata hivyo, kiasi cha kuchanganya lugha kinatofautiana kama wasailiwa walivyothibitisha katika jedwali lifuatalo.

Jedwali la 5: Kiasi cha kuchanganya lugha

Kiwango cha kuchanganya lugha	Maratokezi	Asilimia
Hachanganyi	2	2.7
Kidogo	14	19.2
Wastani	32	43.8
Sana	25	34.2
Jumla	73	100.0

Katika jedwali hili, asilimia 43.8 ya wanafunzi walisema kuwa wao huchanganya lugha katika matumizi yao ya lugha kwa wastani ilhali asilimia 34.2 ya wasailiwa huchanganya lugha sana katika maongezi yao. Ni asilimia 19.2 pekee ya wanafunzi ambao huchanganya lugha katika kiwango cha 'kidogo'. 2.7% ya wanafunzi walisema kuwa wao hawachanganyi lugha. Asilimia hii ni ya chini mno ikilinganishwa na asilimia 34.2 ya wanafunzi ambao huchanganya lugha kwa kiwango cha 'sana'. Kuwepo kwa lugha nyingi chuoni, pamwe na hiari ya lugha, husababisha hali hii ya kuchanganya lugha.

Katika jedwali la lugha wanazozitumia wanafunzi chuoni (jedwali la 2, uk.35), ilibainika kuwa, wanafunzi wengi hutumia lugha tatu, nne na tano. Basi, lugha hizi hung'ang'ania nafasi ya kutumika; hivyo, kulazimisha wanafunzi kuzitumia kwa pamoja. Katika uchunguzi shiriki, ilibainika kuwa, wanafunzi hawana umahiri wa kujieleza moja kwa moja bila kuchanganya lugha jambo linalochangia kuwepo kwa hali hii. Sababu hapa ni kwamba, wanafunzi wana lugha kadhaa ambazo wanaweza kuzitumia kwa pamoja kama ilivyodhihirika kwa wale wanaojua zaidi ya lugha asili moja. Kwa upande ule mwingine, kuchanganya lugha kunaweza kuzua mielekeo hasi kwani, hakumpi mtumizi lugha nafasi ya kuifanyiza kazi lugha mahususi ili kukuza stadi yoyote ya kuitumia, jambo linalochangia katika kutoteuliwa kwa lugha. Jinsi mtu anavyoitumia lugha ndivyo anavyopata umahiri katika lugha husika na ndivyo atakavyoshawishika na kuwa na motisha ya kuiteua ili kuitumia katika shughuli mbalimbali. Mbali na hayo, dhana ya kuhamisha ndimi iliibuka. Kwa mujibu wa Hoffmann (1991), kuhamisha ndimi huhusisha utumizi badala wa lugha mbili katika tamko moja. Basi dhana hii hushirikisha tabia au mazoea na sehemu muhimu ya maingiliano ya wanafunzi miongoni mwao.

4.3 Mielekeo ya Wanafunzi kwa Lugha wanazozitumia

Sehemu hii iligawanywa katika sehemu nne kuu kutegemea hali tofauti za matumizi ya lugha. Habari kuhusu upendelevu wa wanafunzi kutumia lugha mbalimbali zilikusanywa. Wasailiwa waliulizwa lugha wanazopendelea kutumia katika hali nne tofauti. Hali hizi ni kuzungumza, kuandika, kusikiliza na kusoma zilizokuwa msingi muhimu katika kuweza kutimiza lengo la pili la utafiti. Kwa kuzingatia upendelevu wa kutumia lugha, utafiti ulifanikiwa kutambulisha mielekeo ambayo wanafunzi wanayo kwa lugha wanazozitumia. Kutokana na nadharia ya kitendo kilichofikiriwa, kupenda au kutopenda kitu au jambo huwa kigezo muhimu katika kutambulisha mielekeo aliyonayo mtu kwa kitu au jambo hilo.

4.3.1 Lugha inayopendelewa katika mazungumzo

Asilimia 72.6 ya wasailiwa wote, walisema kwamba hawapendelei kuzungumza lugha asili ikilinganishwa na asilimia 26 ya washiriki waliosema kuwa wanapendelea kuzungumza lugha asili. Matokeo haya yanathibitisha kuwa, wanafunzi wengi wa chuo kikuu wana mielekeo hasi kwa lugha asili ingawa Kaniu (2003), aligundua kuwa, wanafunzi hupenda kuzungumza lugha asili zao kuliko lugha nyingine yoyote.

Hali ya matokeo ya Kaniu yanaweza kuelezwa kwa misingi ya muktadha wa utafiti wake. Sehemu aliyoishughulikia katika utafiti wake, ni muktadha halisi wa kule Maragua ambapo lugha asili inatumika kwa kiasi kikubwa. Haya ni tofauti na matokeo ya utafiti huu kwa sababu muktadha wa chuo kikuu unaakisi tofauti nyingi kilugha. Katika chuo kikuu, wanafunzi husajiliwa kulingana na nafasi zilizopo chuoni. Pia uteuzi wa wanafunzi watakaojiunga na chuo fulani, haufanywi kwa misingi ya kundi kabila au eneo analotoka mwanafunzi.

Jedwali la 6: Upendelevu wa kuzungumza lugha asili

Hali	Mara tokezi	Asilimia
Wasiopendelea	53	72.6
Wanaopendelea	19	26.0
Jumla	72	98.6
Waliokosa kujibu	1	1.4
Jumla	73	100

Wasailiwa waliosema hawapendelei kuzungumza Kiswahili ni 53.4%. Matokeo haya yana tofauti kubwa na yale ya jedwali la 6 hapo juu ambapo asilimia 72.6 ya wanafunzi walijibu kutopendelea kuzungumza lugha asili. Ni asilimia 26.0 pekee ya washiriki waliosema wanapendelea kuzungumza lugha asili ikilinganishwa na asilimia 45.2 ambao walisema wanapendelea kuzungumza lugha ya Kiswahili. Tofauti hizi, zinaweza kuelezwa kulingana na hadhi inayopewa lugha mbalimbali nchini Kenya. Pia majukumu yanayotekelezwa na lugha husika na muda unaotumiwa kukuza stadi mbalimbali.

Jedwali la 7: Upendelevu wa kuzungumza Kiswahili

Hali	Mara tokezi	Asilimia
Wasiopendelea	39	53.4
Wanaopendelea	33	45.2
Jumla	72	98.6
Waliokosa kujibu	1	1.4
Jumla	73	100.0

Kwa upande wa Kiingereza, hali ni iyo hiyo. Asilimia 53.4 ya wahojiwa walisema hawapendelei kuzungumza lugha ya Kiingereza ikilinganishwa na asilimia 45.2 ya washiriki ambao wanapendelea kuizungumza lugha ya Kiingereza. Kutokana na hadhi ya lugha hii kama lugha ya kutolea mafunzo katika ngazi zote za elimu nchini Kenya, wanafunzi wafaa kuwa radhi kuzungumza lugha hii. Tofauti na kauli hizo, matokeo haya, yanadhihirisha kinyume kwani, zaidi ya asilimia 50 ya wasailiwa walithibitisha kutopendelea kuzungumza lugha hii.

Ugunduzi kuwa wanafunzi wengi wana mielekeo hasi kwa lugha ni daro kubwa katika juhudi za ufundishaji wa lugha na stadi za mawasiliano. Hii ni kwa sababu ya umuhimu mkubwa unaopewa lugha katika kukuza uwezo wa kuwasiliana. Pia, ruwaza za lugha huthibitika kimazungumzo kabla ya kujifunza kuandika. Viwango hivi vikubwa vya ukosefu wa lugha inayopendelewa katika namna ya kuzungumza miongoni mwa wanafunzi, vinaweza kusababishwa na ukosefu wa sera ya lugha katika vyuo vikuu. Pia mielekeo hasi kwa lugha mbalimbali inayozua desturi mbaya za kusoma miongoni mwa wanafunzi huweza kusababisha hali hii. Hatimaye hali hii inakuwa chanzo cha ukosefu wa umilisi wa kuwasiliana kwa kutumia lugha yoyote ile. Ukosefu wa umahiri huu unaweza kusababisha kuwepo kwa mielekeo hasi. Bayana ni kwamba, katika vyuo vikuu kuna uhiari wa lugha. Basi, kwa kuwa wanafunzi wanatumia au wamaweza kutumia lugha yoyote ile, hawawezi kubadili na kuweka ujuzi wao wa hali na muundo wa lugha waliofunzwa katika viwango tofauti vya elimu katika uwezo wa kuwasiliana kwa njia ya mazungumzo. Matokeo haya yanathibitisha kauli kuwa, ruwaza zote za matumizi ya lugha huthibitika kimazungumzo kabla mtu ajifunze kuandika.

4. 3.2 Lugha inayopendelewa katika kuandika

Sehemu hii ya pili ilihusu kutambulisha ni lugha ipi wanafunzi wanapendelea kutumia katika kuandika. Asilimia 95.9 ya washiriki, walisema kuwa, hawapendelei kutumia lugha asili kuandika. Wasailiwa 2.7 % pekee ndio waliojibu kwamba, wanapenda kutumia lugha asili katika maandishi. Katika kuchunguza lugha ya Kiswahili, 89% ya washiriki walisema kuwa hawapendelei kutumia lugha ya Kiswahili kuandika ikilinganishwa na asilimia 9.6 ya wasailiwa waliosema kwamba, wanapendelea kuandika kwa kutumia lugha ya Kiswahili.

Jedwali la 8: Upendelevu wa kuandika kwa Kiswahili

Hali	Maratokezi	Asilimia
Wasiopendelea	65	89.0
Wanaopendelea	7	9.6
Jumla	72	98.6
Waliokosa kujibu	1	1.4
Jumla	73	100.0

Matokeo hayo yanalingana sana na matokeo ya kupendelea kuandika kwa lugha asili ambapo asilimia ya wasiopendelea kuandika inazidi ile ya wanaopendelea. Hali hii, inaweza kuelezwa kama inayozuliwa na mielekeo hasi ya wanafunzi kwa lugha hizi mbili. Pia, lugha hizi hazitumiki sana katika maandishi tofauti na ilivyo kwa lugha ya Kiingereza. Aghalabu kati ya masomo yote katika ngazi zote za elimu, huandikwa kwa Kiingereza isipokuwa ya lugha za kigeni na ya Kiswahili. Aidha, Kiswahili sanifu huwa na urasmi mkubwa ambao huchangia katika kuwepo kwa mielekeo hasi kwa lugha ya Kiswahili.

Kwa upande wa lugha ya Kiingereza, asilimia 93.1 ya wasailiwa wanaipendelea lugha hii katika hali ya kuandika ilhali asilimia 6.9 ya wasailiwa hawaipendelei. Matokeo hayo ya kupendelewa kwa Kiingereza kutumika katika hali ya kuandika inaweza kuelezwa kwa mujibu wa wakati unaotumika katika kuandika katika lugha ya Kiingereza. Ni bayana kwamba, wakati mwingi wanafunzi wanaandika mambo yao katika lugha hii. Katika shule za msingi na zile za upili, wanafunzi hawaruhusiwi kuandika kwa lugha nyingine ila Kiingereza ijapokuwa katika somo la Kiswahili pekee. Katika vyuo vikuu, ikiwa mwanafunzi hajachukua somo la Kiswahili, hapana wakati wowote ataandika kwa Kiswahili. Hali hii inaelekea kulemaza stadi za wanafunzi za kuandika katika lugha ya Kiswahili na lugha asili. Jambo hili linazua mielekeo hasi kwa lugha husika hususan kwa kuzingatia kwamba mwanafunzi anafaa kuwa na umahiri wa kuwasiliana ikizingatiwa kiwango chake cha elimu. Elimu ya chuo kikuu huelekea kumpa mtu hadhi kubwa; uwezo wa kuwasiliana kwa njia iliyo bora ni kigezo kimoja cha kukoleza hadhi hii.

Ingawa mtafiti hakushughulikia ustadi huu, ukosefu wa stadi kama hizi huweza kusababisha mielekeo hasi kwa lugha husika. Hii ndio sababu kuu ya kuwa na asilimia kubwa ya wanafunzi ambao hawawezi kuandika katika lugha asili zao.

Matokeo hayo yanaweza kuelezwa kwa mujibu wa kiasi cha wakati unaotumiwa katika kukuza stadi tofauti tofauti katika lugha mbalimbali. Kama lugha ya kutolea mafunzo na somo la lazima katika shule, wanafunzi huwa na tajiriba kuu ya kusoma na kuandika zaidi katika Kiingereza kuliko lugha nyingine yoyote tangu wanapojiunga na shule. Zaidi, wanafunzi hawa wana uzoefu mkubwa katika kuandika kuliko kusoma; sababu ni kuwa, kuna insha za kutahiniwa lakini hakuna mtihani wa kusoma na basi inawawia rahisi kuandika katika Kiingereza kuliko kusoma na kujieleza.

4. 3.3 Lugha ambayo Wanafunzi wanapendelea kusikiliza

Katika sehemu ya tatu, utafiti uliazimia kugundua ni lugha ipi wasailiwa wanapendelea kusikiliza. Asilimia 71.2 ya wasailiwa, walijibu kutopendelea kusikiliza lugha asili, huku asilimia 27.4 ya washiriki wakijibu kuwa wanapendelea kusikiliza lugha hii. Wengi wa wanafunzi hawapendelei lugha hii inapotumika katika hali tangulizi (kuzungumza na kuandika), ilibainika pia kuwa hawapendelei kuisikiliza. Matokeo haya yanadhihirisha uwepo wa mielekeo hasi kwa lugha hii kwani, licha ya kuwepo kwa idhaa zinazotangaza vipindi kwa lugha asili, bado asilimia ya washiriki wanaopendelea kusikiliza lugha hii ni ya chini.

Kwa upande wa lugha ya Kiswahili, ilibainika kuwa asilimia 53.4 ya wasailiwa hawapendelei kusikiliza lugha ya Kiswahili ilhali asilimia 45.2 wanapendelea. Matokeo haya yanalingana na matokeo awali ya utafiti kuhusu kupendelea kutumia lugha ya Kiswahili katika hali tofauti zilizotangulia. Asilimia ya wasiopendelea inazidi ile ya wanaopendelea. Inabainika kuwa, kutopendelea kwa mshiriki kutumia lugha husika katika hali moja, kunaelekea kuathiri hali nyingine hususan kwa upande wa lugha asili na Kiswahili. Kutopendelea huku kunazuliwa na mielekeo ya washiriki kuhusiana na lugha husika, hadhi ya lugha hiyo na majukumu yake.

Jedwali la 9: Upendelevu wa kusikiliza Kiswahili

Hali	Maratokezi	Asilimia
Hapendelei	39	53.4
Anapendelea	33	45.2
Jumla	72	98.6
Aliyekosa kujibu	1	1.4
Jumla	73	100.0

Kwa upande wa lugha ya Kiingereza, asilimia 62.5 ya washiriki walijiibu kuwa wanapendelea kusikiliza lugha ya Kiingereza ikilinganishwa na asilimia 37.5 ya washiriki ambao hawapendelei. Matokeo haya yanalingana na yale ya wanaopenda kuandika kwa Kiingereza ambao ni wengi wakilinganishwa na wasiopendelea. Matokeo haya yanaashiria kuwepo kwa mieleko chanya kwa lugha ya Kiingereza.

4.3.4 Lugha ambayo Wanafunzi Wanapendelea Kusoma

Kwa upande wa washiriki wasiopendelea kusoma katika lugha asili, ni asilimia 91.8 huku asilimia 6.8 pekee ya wasailiwa walijiibu kuwa wanapendelea kusoma katika lugha hii. Sababu kuu ya hali hii ni kuwa, lugha asili Haitiliwi maanani katika mitaala ya elimu. Ukweli wa matokeo haya pia unatokana na uhalisia wa lugha hii kimaandishi. Ni bayana kuwa, kuna maandishi haba sana katika lugha asili. Mbali na hayo, ingawa hakuna kundi kabila lolote ambalo halina maandishi kwa lugha asili, katika uchunguzi-shiriki, ilidhihirika kuwa kuna makundi kabila ambayo yana maandishi kama haya na hayayasomi. Kundi kabila la Wameru wanaoshiriki dini ya Kipresbitaria (P.C.E.A) linasoma bibilia iliyoandikwa kwa lugha ya Kikikuyu ingawa kunayo bibilia kwa lugha ya Kimeru ni mfano bora.

Kwa upande wa lugha ya Kiswahili, asilimia 82.2 ya wasailiwa hawapendelei kusoma katika lugha hii ilhali ni asilimia 16.4 ya wasailiwa waliosema kuwa wanapendelea kusoma kwa Kiswahili. Uhalisia huu unaakisiwa pia na idadi ya maandishi katika lugha hii

Jedwali la 10: Upendelevu wa kusoma kwa Kiswahili

Hali	Maratokezi	Asilimia
Hapendelei	60	82.2
Anapendelea	12	16.4
Jumla	72	98.6
Aliyekosa kujibu	1	1.4
Jumla	73	100.0

Matokeo hayo yanaweza kufafanuliwa kwa mujibu wa tofauti zilizokithiri kati ya maandishi na mazungumzo rasmi na yale yasiyo rasmi. Ukweli ni kwamba Kiswahili sanifu kinachotumika katika mazungumzo au maandishi huwa kina urasmi mwingi kuliko Kiswahili

cha matumizi ya kawaida. Hali hiyo hupelekea wanafunzi kutoiteua ili kuitumia lugha hii. Aidha, kuna ule uwoga wa kwamba mzungumzi hazungumzi Kiswahili ipasavyo.

Katika jedwali la 11 hapa chini, asilimia 91.8 ya wanafunzi wanapendelea kusoma katika lugha ya Kiingereza ikilinganishwa na asilimia 6.8 ya wasailiwa ambao hawapendelei. Wengi wa wanafunzi wanaopendelea kutumia Kiingereza katika hali mbalimbali, waweza kuelezwa kwa mantiki ya msisitizo unaotiliwa lugha hii katika ngazi tofauti za usomi. Lugha ya Kiingereza, ndiyo lugha rasmi ya kutolea mafunzo katika taasisi za elimu. Pili, kuna ule uhalisia wa kuwepo kwa maandishi mengi katika lugha ya Kiingereza. Hii huweka wazi nafasi ya kusomwa kwa makala haya pindi tu mwanafunzi anapojihisi kutaka kusoma.

Licha ya kuweka wazi kwa kiasi kikubwa kuteuliwa kwa lugha hii ya Kiingereza, kuwepo kwa vitabu katika lugha hii kunachangia pakubwa katika kukuza stadi za mawasiliano katika lugha hii jambo linalofanya lugha hii kupendelewa na basi kuteuliwa. Kwa upande wa majarida hali ni hiyo hiyo. Hali hii inakuza mielekeo chanya kwa lugha hii na hivyo kuteuliwa na wanafunzi wengi.

Jedwali la 11: Upendelevu wa kusoma kwa Kiingereza

Hali	Maratokezi	Asilimia
Hapendelei	5	6.8
Anapendelea	67	91.8
Jumla	72	98.6
Aliyekosa kujibu	1	1.4
Jumla	73	100.0

Wakati unaotengewa lugha mbalimbali ili kukuza hali hizo (kuzungumza, kuandika na kusoma) hutofautiana pakubwa. Lugha asili aghalabu hutumika katika viwango vya chini vya elimu hususan darasa la kwanza hadi la tatu katika shule za msingi ingawa tajiriba iliyopo sasa inaonyesha kudidimia kwa hali hii. Kuna ushurutishaji wa kutumia lugha mahususi na hata kuna adhabu iwapo mwanafunzi atatumia lugha asili akiwa shuleni. Mielekeo hasi kwa lugha asili na lugha ya Kiswahili huweza kuibuliwa na adhabu na huchangia katika kutoteuliwa kwa lugha hizi.

Kutoteuliwa kwa lugha, kunasababisha kudididmia kwa kiwango cha umahiri wa kuitumia na hapo wanafunzi wanateua lugha ambayo wanaweza kuitumia bila matatizo. Ni dhahiri, kutokana na matokeo ya utafiti kuwa, idadi kubwa ya wanafunzi wanapendelea kutumia lugha ya Kiingereza katika hali yoyote ile jambo ambalo lina misingi yake tangu mwanafunzi alipojiunga na mfumo rasmi wa elimu. Ukweli huu unaashiria kuwepo kwa mielekeo chanya kwa lugha ya Kiingereza. Katika sehemu ya kuzungumza ilidhihirika kuwa, asilimia 43.8 ya wanafunzi wanapendelea kuzungumza Kiingereza ikilinganishwa na asilimia 45.2 ya wanafunzi ambao wanapendelea kuzungumza lugha ya Kiswahili, na, asilimia 26.4 ya wasailiwa wanaopendelea lugha asili. Hali ni iyo hiyo katika hali ya kuandika ambapo, asilimia 2.8 pekee ya washiriki ndio waliojibu kuwa wanapendelea lugha asili ilhali katika Kiswahili, ni asilimia 9.7 pekee zikilinganishwa na ile asilimia ya Kiingereza ambayo ni 93.1. Kutokana na matokeo haya, linaloibuka ni kwamba, ni idadi ndogo sana ya wanafunzi ambao wanapendelea lugha asili zao zinapotumika katika hali hizo nne tofauti. Hali ya kupendelea kuandika kwa lugha asili, kulikuwa na asilimia ya chini kuliko hali hizo zingine zote. Katika hali hii ni asilimia 2.8 pekee iliyopendelea kuandika kwa lugha hii. Katika msururu wa kupendelewa, Kiswahili kinashikilia nafasi ya pili huku kikiwa na asilimia ya kati.

Mfumo wa elimu nchini Kenya huwahitaji wanafunzi kusoma na kuandika kwa Kiingereza na Kiswahili. Hivyo basi, inawawia rahisi kuziteua lugha hizo mbili na kuzitumia. Swala la mielekeo chanya kwa lugha ya Kiingereza linajidhihirisha hapa ilhali watumizi wa lugha ya Kiswahili na lugha asili wanaonekana kuwa na mielekeo hasi. Aidha, kuwa katika chuo kikuu kunasibishwa na umahiri wa kusoma hivyo wengi licha ya kutopendelea kuzungumza lugha ya Kiingereza, hung'ang'ana na kuitumia.

4.3.5 Lugha inayotumiwa na wanafunzi Kuandika Barua

Kulingana na Musonyi (2001), hali ya uzungumzi na uandishi katika matumizi ya lugha inafaa kuwa na kazi mahususi na huru katika mawasiliano. Hata hivyo, hali hizi hung'ang'ana katika kupata hadhi wakati ambapo zinafaa kujengana. Ni kwa mujibu wa madai haya ambapo habari kuhusu lugha inayotumiwa na wasailiwa kuandika barua kwa marafiki zilichunguzwa. Pia, lugha ya kuandika barua kwa wazazi. Kuhusiana na lugha ya kundika barua kwa wazazi, asilimia 47.9 ya wanafunzi walisema kwamba, wao huandika barua kwa Kiingereza, 30.1% kwa Kiswahili, 15.1% kwa lugha asili.

Wazazi wengi, ilibainika kuwa hawasisitizi ruwaza za matumizi ya lugha ambazo ni thabiti. Aidha, wazazi wengi siku hizi hujimudu kwa lugha ya Kiingereza. Umahiri wa kuzungumza lugha fulani ulidhihirika kuweza kumotisha mzungumzaji kuitumia katika namna nyingine za matumizi kama vile kuandika.

Jedwali la 12: Lugha inayopendelewa Kuandika Barua kwa Wazazi

Lugha	Maratokezi	Asilimia
Kiingereza	35	47.9
Kiswahili	22	30.1
Lugha Asili	11	15.1
Kiswahili na Lugha Asili	2	2.7
Kiingereza na Lugha Asili	1	1.4
Kiswahili na Kiingereza	2	2.7
Jumla	73	100.0

Jambo la pili ni kuwa, wanafunzi wengi (57.5%) licha ya kusema kuwa wanazungumza lugha asili vyema sana, ilibainika katika uchunguzi shiriki kuwa, hawawezi kuandika kwa lugha asili. Hali hii ilijitokeza katika uchunguzi shiriki ambapo wanafunzi walikiri kwamba wanafahamu na kuelewa wanaposikia lugha asili zao zikizungumzwa ingawa wao wenyewe hawawezi kuziandika kwa ufasaha. Hii inathibitisha kwamba, ingawa wanafunzi wanafahamu lugha asili, lugha ya Kiswahili na lugha ya Kiingereza, wengi wao wanaandika vyema kwa lugha ya Kiingereza ikifuatwa na lugha ya Kiswahili na hatimaye lugha asili. Sababu ya hali hii ni kuwa, mfumo wa elimu nchini Kenya, hautoi nafasi hata kwa wanafunzi walio katika viwango vya chini vya usomi kufunzwa lugha asili zao. Hivi leo shule zinasisitiza lugha ya Kiingereza na Kiswahili hususan katika shule za mjini. Matokeo haya yanadhihirisha kukosekana kwa umahiri katika kuandika katika lugha fulani jambo linalochangia katika kuamua ni lugha ipi mwanafunzi atateua kuitumia. Kwa kuwa wanafunzi wa vyuo vikuu huchukuliwa kama vielelezo vya jamii, inawalazimu wateue lugha ambayo wanajimudu kwayo ili kuafiki mtazamo huo wa jamii pana. Hakuna mwanafunzi aliye katika chuo kikuu ambaye angependa kuonekana akiandika barua yenye makosa ama asiyejimudu kwa lugha.

Usasa pia umeingilia jamii ya wasomi sana na hawajaepukana na athari za usasa huu kama inavyodhihirika katika jedwali hilo la kuandika barua kwa wazazi. Kuwa katika chuo kikuu kunasibishwa na hadhi fulani katika jamii. Mtazamo huo hupelekea wanafunzi wa vyuo vikuu kutazamwa kwa jicho kali kuhusiana na mambo wanayoyafanya kutumia lugha kwa ufasaha kukiwa miongoni mwa mambo kama hayo.

Katika kuandika barua kwa marafiki, asilimia 87.7 ya wanafunzi walikiri kwamba wao huandika barua kwa kutumia lugha ya Kiingereza. Lugha ya Kiswahili na mchanganyiko wa lugha ya Kiingereza na lahaja ya Sheng' hutumiwa na asilimia sawa ya wanafunzi yaani 4.1%. Lahaja ya Sheng', lugha asili na mchanganyiko wa lugha ya Kiswahili na lahaja ya Sheng', hutumiwa na asilimia 1.4 ya wanafunzi. Kwa kuwa hakuna ukweli wowote katika asilimia za wanafunzi ambao walijibu kuandika barua kwa kutumia lahaja ya Sheng', asilimia hizo hazikuwa muhimu katika kueleza matumizi ya lugha kuandika barua.

Hata hivyo, asilimia 4.1 ya wanafunzi waliojibu kuwa wanachanganya lugha ya Kiingereza na lahaja ya Sheng' ilikuwa muhimu hasa katika kuweka wazi kuwa, katika uandishi wa barua kuna kuchanganya lugha. Aidha, asilimia hii ya wanafunzi inabainisha kundi lao la rika. Kila rika au kundi la watu hujitambulisha kiisimu kwa kuwa na lugha yao mahususi. Kwa mfano wazungumzaji waliokomaa kiumri watakuwa na lugha yenye msamiati mzito uliojaa maneno ya busara. Lahaja ya Sheng' sanasana huambatanishwa na rika kama hili na basi ili wanafunzi waweze kujitambulisha na wenzao, wanaitumia kuwasiliana. Mbali na hayo, matumizi ya lahaja hii katika kuandika barua yanadhihirisha athari zake katika mawasiliano kwani inabainika kuwa, haijajikita katika mawasiliano ya mdomo tu bali pia katika mawasiliano ya maandishi.

Lugha ya Kiingereza ilidhihirika kuwa inatumika sana; dhihirisho kuwa hii ndiyo lugha ambayo wanafunzi wameizoea na kuifahamu zaidi. Matokeo haya yanakubaliana na matokeo kuhusu kupendelewa kwa lugha ya Kiingereza inapotumika katika hali ya maandishi ambapo, asilimia 93.1 ya wanafunzi, walikiri kuipendelea. Hata hivyo, kwa mujibu wa jedwali la 10 ni asilimia 44.4 ya wanafunzi ambao wanaipendelea lugha hii ionapotumika katika hali ya kuzungumza. Hii inadhihirisha tofauti za umahiri katika stadi mbalimbali na pia mielekeo tofauti kwa lugha ya Kiingereza inapotumika katika hali mbalimbali.

Matokeo kuhusu lugha inayotumiwa kuandika barua yalibainisha kuwa, lugha ya Kiingereza hutumika sana. Asilimia 15.1 ya wanafunzi walisema kuwa, wao hutumia lugha asili kuandika barua kwa wazazi wao. Lugha asili ndiyo lugha ambayo wanaweza kusoma na kuelewa. Aidha, inadhihirisha utambulisho wao na kabila lao. Kwa upande ule mwingine, asilimia 47.9 ya wanafunzi walisema kwamba wao hutumia lugha ya Kiingereza katika kuandika barua kwa wazazi wao. Asilimia hii yaweza kulinganishwa na uwezo wa wanafunzi wa kuandika kwa lugha asili. Ingawa utafiti haukuzingatia ustadi wa wanafunzi wa kuandika katika lugha asili, katika uchunguzi shiriki wanafunzi waliulizwa sababu ambayo huwafanya wasitumie lugha asili kuandika barua. Miongoni mwa sababu walizozitoa ni ukosefu wa ustadi huu.

Ni bayana kuwa, wengi hawana ule umahiri na weledi wa kuandika katika lugha asili. Wazo hili linathibitishwa na tofauti kubwa inayojitokeza baina ya asilimia ya wanafunzi wanaotumia lugha asili na lugha ya Kiswahili na Kiingereza. Asilimia ya wanafunzi wanaotumia lugha ya Kiingereza kuaandika barua kwa marafiki (kiume na kike) ni ya juu kuliko ile ya kuandika barua kwa wazazi kwa kutumia lugha hii. Matokeo haya yanawiana na madai ya Whiteley (1974) kuwa, lugha ya Kiingereza hufanya kazi kama lugha ya siri ambayo kwayo washiriki hujadiliana mambo ya kiheba. Hata hivyo, matumizi ya lugha ya Kiingereza hayaakisiwi vyema katika mazungumzo ambapo lugha ya Kiswahili ilibainika kupendelewa (Jedwali 4) ingawa wanafunzi huwa wamekumbana zaidi na lugha ya Kiingereza kuliko lugha asili na lugha ya Kiswahili. Ilibainika kuwa, wanafunzi wanapendelea kutumia lugha ya Kiingereza katika hali ya maandishi kuliko kuzungumza. Sababu kuu ni kwamba, wanafunzi hawa huwa wametumia muda wao mwingi katika kujifunza stadi za kuandika na sio kuzungumza.

4. 3.7 Lugha inayopendelewa katika Vyombo vya Habari

Matokeo kuhusu kusikiliza vipindi vya redio na kusoma magazeti katika lugha tofauti yalichunguzwa. Ili kutimiza lengo hili, wanafunzi waliulizwa kuchagua idhaa wanazosisikiliza na magazeti wanayosoma. Wanafunzi wengi walisema kwamba wao husikiliza vipindi vya radio kwa lugha hizi: Lugha asili, Kiswahili na Kiingereza ingawa kwa vipimo tofauti. Ilibainika wanafunzi wengi (asilimia 76.7) husikiliza vipindi kwa lugha ya Kiingereza.

Ni asilimia 1.4 pekee ya wanafunzi waliokiri kusikiliza vipindi katika lugha ya Kiingereza kwa kiwango 'kidogo'. Katika kiwango cha 'wastani,' asilimia 21.9 ya wanafunzi, husikiliza vipindi vya radio katika lugha ya Kiingereza.

Kwa upande wa kusikiliza vipindi katika lugha ya Kiswahili, matokeo yalikuwa kama ifuatavyo: asilimia 43.8 ya wanafunzi walisema kuwa husikiliza vipindi vya radio katika lugha ya Kiswahili kwa wastani, 41.1% ya wasailiwa katika kile kipimo cha kidogo, 13.7% kwa kipimo cha sana na asilimia 1.4 ya washiriki wakakiri kuwa wao hawasikilizi vipindi katika lugha ya Kiswahili.

Kwa upande wa lugha asili, licha ya kuwa nchini Kenya kuna idhaa nyingi zinazotangaza vipindi katika lugha asili, asilimia 43.8 walisema kuwa hawasikilizi vipindi katika lugha hii. Asilimia 37 ya wanafunzi husikiliza vipindi katika lugha asili kwa kiasi kidogo. Ni asilimia 8.2 pekee ya wanafunzi ambao husikiliza vipindi katika lugha asili kwa kipimo cha wastani ikilinganishwa na asilimia 11.0 wanaosikiliza vipindi katika lugha asili kwa kiasi cha sana.

Matokeo hayo yanabainisha kuwa, wanafunzi wengi husikiliza vipindi vya radio katika lugha tatu, ingawa katika vipimo tofauti. Ugunduzi huu unamaanisha kuwa, lugha zote tatu ni mashuhuri katika nyanja hii ya utangazaji nchini Kenya. Kusikiliza vipindi vya radio kwa kipimo cha 'sana' na 'wastani' kunaweza kutia shime na kuimarisha bidii za wanafunzi kupata umahiri katika lugha husika hivyo kuchangia uteuzi wa lugha fulani. Daro hili huchangiwa na hamu ya kupata misamiati mipya na kuweza kuitumia kisahih. Hata baada ya kuwepo kwa idhaa zinazotangaza vipindi vyake kwa lugha asili, watangazaji wa idhaa hizi bado wanatumia lugha ya Kiingereza katika utangazaji wao jambo ambalo linadhihirisha utawala wa lugha hii.

4.3.8 Lugha inayopendelewa Kusoma Magazeti

Kwa mujibu wa jedwali la 13 (uk 52), asilimia 86.3 ya wanafunzi walijibu kuwa hawasomi gazeti kwa lugha asili. Ni asilimia 11.0 pekee ya wanafunzi ambao husoma magazeti kwa kipimo cha kidogo katika lugha asili. Katika kipimo cha 'wastani' na 'sana', asilimia 1.4 pekee ya wanafunzi ndio waliojibu kutumia lugha asili katika vipimo hivyo. Sababu ya kuwa na idadi kubwa ya wanafunzi ambao hawasomi magazeti katika lugha asili ni kutokana na uhalisia wa lugha mbalimbali katika uwanja wa maandishi nchini Kenya. Kuna magazeti machache mno katika lugha asili na yaliyopo ni katika lugha asili za makundi kabila yenye ushawishi mkubwa kiidadi na kiuchumi; kwa mfano kundi kabila la Wakikuyu.

Asilimia 1.4 ya wanafunzi waliosema kuwa wao husoma magazeti katika lugha asili wanawakilisha makundi kabila haya na zaidi pia maeneo fulani ya taifa la Kenya. Aidha, hawa ni wale wanaofahamu zaidi ya lugha asili moja na hivyo kuteua kusoma gazeti katika lugha hiyo.

Jedwali la 13: Usomaji gazeti kwa lugha asili

Kipimo cha kusoma gazeti	Maratokezi	Asilimia
Hasomi	63	86.3
Kidogo	8	11.0
Wastani	1	1.4
Sana	1	1.4
Jumla	73	100.0

Kutokana na uhaba wa kuwepo kwa magazeti katika lugha asili kunadhihirisha mielekeo hasi kwa lugha asili. Katika sura ya pili, ilitajwa kwamba, kuna magazeti matatu makuu kwa lugha ya Kiingereza ilhali kunalo gazeti moja tu kwa lugha ya Kiswahili. Kwa kuwa magazeti yaliyopo katika lugha asili ni haba na yamejikita katika eneo moja la kisiasa na kijiografia, haiwezekani kusema ni mangapi. Hata hivyo, katika chuo kikuu hakuna hata jarida moja ambalo limeandikwa kwa lugha asili hivi kwamba wanafunzi wa kutoka kundi kabila fulani wanaweza kulisoma. Majarida yote yalimo chuoni ni ya lugha ya Kiingereza.

Uandishi ni dhana muhimu ambayo hukuza lugha. Pia, huchangia uwezo wa wanafunzi kwa upande wa msamiati, kukuza ujasiri wa kuitumia. Zaidi, hukuza mielekeo chanya kwa lugha husika hivyo basi kuweza kuiteua kuitumia. Mbali na hayo, hakuna sababu mwafaka ya kutokuwa na magazeti au hata majarida katika vyuo vikuu na nchini Kenya kwa lugha asili, kwani kila lugha huwa na uwezo wa kueleza dhana zote wakati wowote.

Kuhusu usomaji wa gazeti kwa lugha ya Kiswahili, kulikuwepo na asilimia 56.2 ya wanafunzi ambao husoma magazeti kwa lugha hii 'kidogo'. Katika kipimo cha 'wastani', asilimia 20.5 ya wasailiwa husoma gazeti kwa lugha ya Kiswahili ikilinganishwa na asilimia 19.2 inayowakilisha wanafunzi waliosema kuwa hawasomi magazeti kwa Kiswahili.

Sababu zinazopelekea kutoteuliwa kwa gazeti la Kiswahili ni pamoja na kuwepo kwa habari finyu ikilinganishwa na habari ambazo ziaangaziwa katika magazeti ya Kiingereza.

Asilimia 4.1 ya wanafunzi waliojibu kuwa wao husoma magazeti katika lugha hii kwa kipimo cha kidogo. Licha ya kuwa kunalo gazeti moja tu katika lugha ya Kiswahili nchini Kenya hali ambayo pia ni dhahiri katika vyuo vikuu, kuna asilimia ya wanafunzi ambao husoma gazeti katika lugha hii. Asilimia hiyo inawakilisha wanafunzi ambao wana hamu ya kujikuza katika nyanja ya ushairi ambayo huwa imezingatiwa katika gazeti la *Taifa Leo*. Juu ya hayo, gazeti hili huwa na hadithi na visa ambavyo humvutia msomaji. Haya ni mambo ambayo huchangia mtu katika kuwa na mielekeo chanya kwa lugha. Asilimia hii ya wanafunzi pia yaweza kuelezwa kwa mujibu wa jedwali la 14 (uk 54) ambapo kuna asilimia 21.9 ya wanafunzi ambao walisema kuwa wanaafikiana na kauli ya swali hilo kwa kiasi cha “nakubali kabisa”. Asilimia hii ya wanafunzi inawakilisha jumuiya ya wanafunzi wa vyuo vikuu ambao wana mielekeo chanya kwa lugha hii.

Wanafunzi wengi walisema wao husoma magazeti kwa Kiingereza kwa kiasi ‘sana’. Asilimia 95.9 ya wanafunzi walioshirikishwa, walikiri kusoma magazeti katika kiwango hicho. Matokeo haya yaweza kuelezwa kwa kuangazia ukweli kwamba, nchini Kenya kunayo magazeti matatu makuu kwa lugha ya Kiingereza yaani *Daily Nation*, *Standard* na *People Daily* na katika mwaka wa 2005, kulianzishwa gazeti lingine la *The Leader*. Kuwepo kwa magazeti haya kunatoa nafasi kubwa ya kusoma maandishi kwa lugha hii. Kwa upande ule mwingine, kuna gazeti moja tu katika lugha ya Kiswahili yaani *Taifa Leo*. Katika lugha asili, ni nadra sana. Aidha, katika vyuo, hata majarida yanayotolewa huwa katika Kiingereza. Kwa mfano chuoni Egerton, kunayo majarida ya *News Link*, *Oasis* na *Gender Connection*

4.3.9 Ufaafu wa Lugha ya Kiswahili kutumika chuoni

Mojawapo wa madhumuni ya utafiti huu yalikuwa ni kujaribu kutambulisha mielekeo ya wanafunzi kuhusiana na lugha wanazozitumia hususan lugha asili, Kiswahili, na Kiingereza. Kuhusu kufaa kwa lugha ya Kiswahili kutumika chuoni, wanafunzi waliulizwa kuweka vipimo vya sikubali kabisa, sikubali, sina uhakika, nakubali na nakubali kabisa kwa mujibu wa kipimo cha Likert. Kwa kuwa mielekeo ni maoni ya ndani ya mtu kuhusu kupendelea au kutopendelea jambo fulani yanayotokana na tajiriba zake za maisha (Allport katika Gardner 1985); maoni ya washiriki kuhusu ufaafu wa lugha ya Kiswahili yalibainisha mielekeo kuhusiana na lugha.


Asilimia 27.4 ya wanafunzi walisema kuwa hawakubaliani na kauli hiyo, 24.7% ya wanafunzi wakajibu kuwa wanakubaliana na kauli hiyo. Asilimia 21.9 ya wasailiwa walikiri kukubaliana kabisa na kauli ya swali hilo ilhali asilimia 17.8 ya washiriki wakasema kuwa hawakubaliani kabisa na kauli hiyo. Ni asilimia 8.2 pekee ya wanafunzi waliosema kuwa hawana uhakika kuhusiana na ufaafu wa lugha ya Kiswahili kutumika chuoni. Kwa mujibu wa matokeo hayo, asilimia kubwa ya wanafunzi inabainika kuwa na mielekeo hasi kwa lugha ya Kiswahili; hivyo kuteua jawabu la kutokubali na kutokubali kabisa.

Mielekeo hii hasi inaweza kuwa chanzo cha kuwa na asilimia kubwa ya wanafunzi ambao hawapendelei kuzungumza lugha ya Kiswahili au lugha hii inapotumika katika hali hiyo ambapo, asilimia 54.2 ya wanafunzi walisema kuwa hawaipendelei. Chanzo cha wanafunzi kuwa na mielekeo hasi kwa lugha ya Kiswahili kunatokana na wakati na umuhimu unaopewa lugha mbalimbali. Licha ya lugha hii kuwa imetambuliwa na sheria za Kenya, bado hakuna mikakati mwafaka inayoipa lugha ya Kiswahili nafasi nzuri ya kutumiwa hususan katika hali rasmi.

Katika chuo kikuu, hakuna sera madhubuti inayohusiana na lugha jambo ambalo linachangia katika udidimiaji wa matumizi ya lugha ya Kiswahili. Mbali na hayo, katika uchunguzi shiriki, wanafunzi wengi walilamikia tofauti kubwa iliyopo baina ya Kiswahili sanifu na matumizi ya kawaida ya lugha ya Kiswahili.

Jedwali 14: Ufaafu wa lugha ya Kiswahili kutumika chuoni

Jawabu	Maratokezi	Asilimia
Sikubali Kabisa	13	17.8
Sikubali	20	27.4
Sina uhakika	6	8.2
Nakubali	18	24.7
Nakubali Kabisa	16	21.9
Jumla	73	100.0



4.3.10 Kutumika kwa lahaja ya Sheng'

Asilimia 67.1 ya wasailiwa walisema kuwa hawakubali kabisa kwamba lahaja hii haitumiki chuoni. Asilimia 20.5 ya wahojiwa wakajibu hawakubali; ilhali wanafunzi asilimia 8.2 na 2.7 wakasema kuwa lahaja hii haitumiki chuoni kwa kuweka jawabu la nakubali na nakubali kabisa. Ingawa lahaja ya Sheng haijafikia kiwango cha kuwa lugha kama ilivyo kwa lugha asili, Kiswahili na Kiingereza, lahaja hii imekita mizizi yake katika kutumiwa kama inavyodhihirishwa na matokeo hayo. Iligunduliwa kuwa lahaja hii inatumika sana katika hali ya mazungumzo ambapo wanafunzi wanaichanganya na lugha zile za kiasili, Kiswahili na Kiingereza. Kutumika kwa lahaja hii, huenda kunatokana na kile kizazi kilichopo katika vyuo vikuu. Ni kizazi ambacho kimekulia katika mazingira ya lahaja hii na hupenda sana kujitambulisha kwa lahaja hii. Matumizi ya lahaja hii ya Sheng, hata hivyo, yamejikita baina ya wanafunzi wenyewe na zaidi pia yanapelekana na sehemu ambayo mwanafunzi ametoka. Ilibainika kuwa wanafunzi ambao wametoka mijini kama vile mji wa Nairobi, huwa na misamiati mipya zaidi katika lahaja hii na basi waliwaathiri wenzao kutoka sehemu za mashambani.

4.3.11 Uhuru wa kutumia Lugha Asili popote pale Chuoni

Utafiti uliazimu kuchunguza ikiwa wanafunzi hawa wenye taadhima machoni mwa wanajamii wana uhuru wa kutumia lugha asili popote pale chuoni kwa vile, katika vyuo vikuu hakuna ushurutishaji wa lugha. Kwa kufanya hivi mtafiti alidhamiria kujua kwa hakika kama kweli hiari ya lugha inatoa uhuru wa kutumia lugha hii wakati wowote ule pahali popote pale. Asilimia 32.9 ya wanafunzi walikubali kabisa kwamba wako huru kutumia lugha asili popote pale chuoni ilhali asilimia 19 ya wanafunzi hawakukubaliana na kauli hiyo. Asilimia 23.3 ya washiriki walikataa kabisa kwamba hawana uhuru wa kutumia lugha asili popote pale na wakati wowote ule chuoni. Asilimia 1.4 ya wasailiwa hawakuwa na uhakika kuhusiana na kauli hii.

Asilimia ya wanafunzi ambao walikubaliana na kauli ya kuwa huru kutumia lugha asili popote pale chuoni, inaweza kuelezwa kwa msingi kwamba, katika chuo kikuu kuna hiari ya lugha na hivyo basi wanafunzi wanaweza kutumia lugha yoyote almuradi wawasiliane. Aidha, hili ni kundi la wanafunzi ambao wanahisi kwamba, lugha yao ni bora na inaweza kutimiza mahitaji yote ya mawasiliano. Kila lugha huwa na uwezo wa kuelezea dhana yoyote ile; wanafunzi wanaweza kutumia lugha asili kuelezea mawazo yao.


Wanafunzi hao wana utambulisho chanya wa kundi kabila lao na wangependa kujitambulisha kwa lugha asili yao. Hata hivyo, ilibainika kwamba licha ya kuwepo kwa hiari ya lugha vyuoni, kuna asilimia ya wanafunzi ambao hawako huru kutumia lugha asili popote pale na wakati wowote ule chuoni. Kundi hili la wanafunzi ni kundi ambalo lina mielekeo hasi kwa lugha asili zao kwa upande mmoja hivi kwamba halingependa kuonekana likiitumia. Zaidi pia linajitambulisha na hadhi ya kuwa katika chuo kikuu ambapo lugha ya Kiingereza hunasibishwa na mazingira kama haya ya usomi. Kwa upande ule mwingine, ni kundi ambalo linazingatia uanuwai wa jumuiya ya wanafunzi na kuzingatia sheria za kiisimu jamii za mawasiliano kwamba, lazima wazungumzi wawe na ufahamu wa lugha husika ikiwa mawasiliano yatatokea, kutimiza kusudio na kukamilika.

Wanafunzi ambao hawakukubaliana na kauli ya uhuru wa kutumia lugha asili popote pale chuoni, wanaweza kutolewa ufafanuzi kwamba, wanatambua kuwepo kwa miktadha mbalimbali ya matumizi ya lugha. Miktadha hii itahitaji lugha tofauti kulingana na: misingi ya kazi ambazo lugha mbalimbali zimetengewa na kusudi la mawasiliano na kanuni za isimu jamii kama vile urasmi wa muktadha unaohusika. Mbali na hayo, kundi hili la wanafunzi linawakilisha jumuiya ya wanafunzi ambao wana mielekeo hasi kwa lugha asili.

Athari ya hiari ya lugha katika vyo vikiu ni dhahiri hususan inapozingatiwa kwamba kuna asilimia 1.4 ya washiriki ambao walikiri kutokuwa na uhakika kuhusiana na uhuru wa kutumia lugha asili popote pale chuoni. Ni wazi wanafunzi hawa, hawatambui iwapo inafaaa au haifai kuitumia lugha asili; kwa vyovyote vile, ni katika miktadha ipi na washiriki wapi.

Jedwali 15: Uhuru wa kutumia lugha asili popote pale chuoni


Jawabu	Maratokezi	Asilimia
Sikubali kabisa	17	23.3
Sikubali	19	26.0
Sina unahakika	1	1.4
Nakubali	12	16.4
Nakubali Kabisa	24	32.9
Jumla	73	100.0



Maoni mengine yaliyotafutwa ni kuhusiana na kupendwa kwa Kiingereza kuliko Kiswahili na lugha asili. Hili ni swali la mielekeo moja kwa moja kwa kuwa kupenda au kutopenda kitu hutawaliwa na mielekeo ya mtu kuhusu kitu hicho. Matokeo ya swali hilo yalikuwa kama ifuatavyo katika jedwali lifutalo

Jedwali 16: Kupendelewa kwa Kiingereza kuliko Kiswahili na Lugha Asili

Jawabu	Maratokezi	Asilimia
Sikubali kabisa	5	6.8
Sikubali	8	11.0
Sina uhakika	10	13.7
Nakubali	23	31.5
Nakubali kabisa	27	37.0
Jumla	73	100.0



Kutokana na jedwali hilo, ni bayana kuwa, lugha ya Kiingereza inapendelewa na wanafunzi wengi. Asilimia 37 ya washiriki wote walikiri kukubali kabisa kuwa lugha hii inapendelewa kuliko lugha asili na lugha ya Kiswahili. Hali hii ya kupendelewa kwa Kiingereza yaweza kutokana na majukumu ambayo lugha hii hutekeleza katika kufanikisha maisha ya usomi ya mwanafunzi. Mbali na hayo, wanafunzi wanakumbana na lugha hii zaidi katika mfumo wa elimu. Ili mwanafunzi awe katika daraja ya chuo kikuu, huwa ametumia miaka kumi na miwili katika shule ya msingi na shule ya upili. Katika daraja hizo za usomi, lugha ya Kiingereza ndiyo lugha rasmi ya kutolea mafunzo na pia hushinikizwa kutumika wakati wowote shuleni. Aidha, kuna maandishi mengi katika lugha ya Kiingereza, yakilinganishwa na maandishi katika lugha ya Kiswahili na lugha asili jambo linalochangia sana katika kuwekwa wazi kwa lugha hii ya Kiingereza kwa wanafunzi na kuwapa tajiriba kubwa.

Katika jedwali hilo (jedwali la16), ni asilimia 6.8 ya wanafunzi ambao walisema kuwa hawakubaliani kabisa na hoja hiyo. Hii ni asilimia ya chini mno ikilinganishwa na ile asilimia ya wanaokubaliana kabisa na hoja hii. Hii inadhihirisha kuwepo kwa mielekeo chanya kwa lugha ya Kiingereza.

Pia, tofauti hii inatomelea na kuthibitisha matokeo ya wanafunzi ambao walikiri kwamba wanazungumza vyema lugha ya Kiingereza na kuifurahia inapotumika katika namna mbalimbali. Asilimia hiyo ndogo ya wanafunzi ambao hawakubaliani kabisa na hoja hiyo, inawakilisha asilimia ndogo ya wanafunzi ambao wana msingi mwema katika Kiswahili na ambao wanakitumia kwa ufasaha katika stadi yoyote ile. Pia, hiyo ndiyo asilimia ya wanafunzi ambao walikiri kuzungumza Kiswahili vyema.

Inabainika kuwa, kuna uhusiano kati ya ujuzi wa lugha, mieleko na matumizi ya lugha. Jinsi mwanafunzi alivyoimarika katika lugha, ndivyo anavyokuwa na mieleko chanya kwa lugha hiyo na hivyo kuiteuwa kuitumia. Basi, uhusiano baina ya ujuzi na matumizi ya lugha unakuwa muhimu kwa mujibu wa kuwa tayari kwa wanafunzi kuteua au kutoteua lugha fulani. Mbali na hayo, asilimia hii inawakilisha baadhi ya wanafunzi ambao walisema kuwa hawachanganyi lugha na hutumia lugha ya Kiswahili pekee. Asilimia 11 ya wanafunzi walisema kuwa hawakubali hali hii; ilhali asilimia 13.7 ya washiriki wote walijibu kuwa hawana uhakika kuhusiana na swali hilo; asilimia ambayo inaelezwa kutokana na kuwepo kwa hiari ya kutumia lugha yoyote ile katika chuo kikuu. Asilimia 31.5 ya wasailiwa wakasema kuwa wanakubaliana na madai ya swali hilo.

Matokeo hayo yanatoa hali ya kuongezeka kwa asilimia ya wanafunzi kutoka hali moja hadi nyingine hadi kufikia kiwango cha kuwa na asilimia ya juu ya wanafunzi wanaokubali kabisa. Hii ni ithibati ya kutosha kuthibitisha kauli kwamba, wanafunzi wana mielekeo chanya kwa lugha hii ya Kiingereza. Ni hiyo mielekeo mizuri kwa Kiingereza, ambayo hasa inatokana na umuhimu wa lugha hii katika kukidhi mahitaji ya kielimu ya wanafunzi wa vyuo vikuu inayowafanya wengi wao kuipenda na wapende kuitumia katika miktadha mingi chuoni ingawa lugha asili na lugha ya Kiswahili pia hutumika.

4. 4 Ruwaza za Matumizi ya Lugha chuoni

Tabia ya wanafunzi aidha shuleni au nyumbani huathiriwa na mambo kadhaa, (Kaniu, 2003). Katika hali nyingi nyumbani na shuleni, masharti yanayowekewa wanafunzi kuhusiana na uteuzi wa lugha huwekwa wazi. Sera za shule nyingi nchini Kenya huhitaji wanafunzi wazungumze lugha ya Kiingereza. Tofauti na hali hiyo, wanafunzi wa vyuo vikuu wana uhuru aidha ni wa kutumia lugha au wa shughuli zao za kibinafsi. Ili kutambulisha tabia za lugha ya wanafunzi vyuoni, na ruwaza za matumizi ya lugha, wanafunzi waliulizwa kuhusu lugha

wanazozitumia katika miktadha mbalimbali kwa kuzingatia ukweli kuwa, vyuoni kuna mahali kwingi ambako wanafunzi huingiliana na kutumia lugha.

Kila mahali, dhifa na shughuli tofauti huhitaji lugha mahususi inayoafiki shughuli au mahali hapo (Kaniu 2003:33). Hata hivyo, katika utafiti huu, uti wa habari hizi ulikuwa ni hiari ya kutumia lugha yoyote popote pale, mradi wanafunzi waweze kuwasiliana. Ryan (1982), naye anatoa rai kuwa, jinsi lugha ilivyo na majukumu mengi na muhimu ya kutekeleza, ndivyo itakavyoteuliwa ili kutumiwa na wazungumzaji. Fishman (1971), anasema kuwa, hadhi ya lugha hupanda na kushuka kulingana na safu na umuhimu wa majukumu inayoyatekeleza. Anadai kwamba, lugha ya kikabila ina nafasi kubwa na uwezo wa kustahimili uhamiaji kutoka kwa taifa asili ikiwa itaendelea kutumika katika hali nyingi. Kwa mintarafu hiyo, wanafunzi waliulizwa kuhusu lugha wanazotumia chuoni katika vyumba vya kulala, vya maakuli, misafara ya kuhudhuria mihadhara, na katika vikundi vyao vya kuota jua.

Katika mgawo wa maeneo ya utumizi wa lugha, Fishman (1971) alibainisha migawo miwili mikuu. Hii ni miktadha rasmi na isiyo rasmi. Muktadha usio rasmi uliteuliwa kwa vile, kwa kawaida huwakilisha maeneo yasiyo ya ushurutishaji wa lugha na kumfunga mtumiaji lugha. Katika vyumba vya kulala, kulikuwepo na lugha kumi zilizobainika kutumika. Sita miongoni mwazo ni uchanganyaji wa lugha mbili au hata tatu. Matokeo haya yanabainisha halisia kadhaa za matumizi ya lugha katika vyuo vikuu. Kwanza, yanadhihirisha kuwa, wanafunzi wanachanganya lugha. Asilimia 11.0 ya wanafunzi walisema kuwa, wanatumia lugha ya Kiingereza na asilimia 41.1 ya wanafunzi wanatumia lugha asili ilhali asilimia 19.2 ya wanafunzi hutumia lugha ya Kiswahili jumla ikiwa ni asilimia 73.3. Hii inadhihirisha kuwa kuna asilimia 26.7 ya wanafunzi ambao huchanganya lugha katika viwango tofauti kwa kila aina ya lugha.

Uhalisia mwingine ni kuwa, lugha asili inashikilia nafasi ya kwanza kimatumizi katika muktadha huu ikifuatwa na lugha ya Kiswahili. Licha ya lugha ya Kiingereza kuwa na asilimia kubwa (64.4) kuliko lugha nyingine yoyote katika ile hali ya kuzungumzwa, katika muktadha huu, lugha hii haina umaarufu. Pia, ule uchanganyaji ndimi mbili au tatu. Lahaja ya sheng ambayo hudaiwa kutumiwa na watu wa rika kama hili, pia haina umaarufu sana ikiwa na asilimia 2.8 pekee ya wanafunzi kama ilivyo na ule mchanganyiko wa lugha asili na lugha ya Kiswahili. Uchanganyaji wa lugha asili na lugha ya Kiingereza ulikuwa na asilimia ya chini (1.4%). Matokeo haya yanalingana na matokeo ya wataalamu kama vile Fishman ambapo katika utafiti huu inabainika

kuwa vyumba vya kulala vinaweza kulinganishwa na muktadha wa kinyumbani ulioainishwa na tafiti za awali.

Jedwali la 17: Lugha inayotumiwa na wanafunzi Bwenini

Lugha	Maratokezi	Asilimia
Sheng'	2	2.7
Kiingereza	8	11.0
Kiswahili	30	19.2
Lugha Asili	14	41.1
Lugha Asili na Kiswahili	2	2.7
Lugha Asili na Kiingereza	1	1.4
L.A, Kiswahili na Kiingereza	3	4.1
Kiswahili na Kiingereza	6	8.2
Kiswahili na Sheng'	3	4.1
Lugha Asili na Sheng	2	2.7
Jumla	71	97.3
Waliokosa kujibu	2	2.7
Jumla	73	100.0

Katika vyumba vya maakuli, ilidhihirika kuwa hali ni tofauti na bweni. Hapa, lugha asili haina umaarufu. Uchunguzi shiriki ulibainisha sababu ya hali hii kuwa, wanafunzi hupiga foleni pasi na misingi ya kikabila tofauti na vyumba vya kulala ambapo wanafunzi huweza kuamua kuwa chumba kimoja na wanafunzi wa kundi kabila lao. Iwapo kutakuwa na matumizi ya lugha asili katika foleni hizi, ni finyu mno na hunuiwa kujitambulisha ili kupata hisani kama vile kusogeana katika foleni. Vyumba vya maakuli vinaweza kulinganishwa na miktadha inayoafiki matumizi ya lugha rasmi. Haja hii huzuliwa na tofauti za wanafunzi kwa misingi ya asili zao kwa kutumia kigezo cha makundi kabila. Lugha ya Kiswahili inashikilia nafasi ya kwanza katika kuteuliwa na kutumiwa na wanafunzi aghalabu ina asilimia 43.1 ya wanafunzi wanaoitumia. Baadhi ya matukio neni yaliyoibuka ni kama vile: kuazimana vijiko, kujuliana hali, kutaka kuingizwa katika foleni, maagano, kulalamikia kiasi na ubora wa chakula.

Asilimia ya wanafunzi wanaotumia lugha ya Kiingereza na lile kundi la wanafunzi wanaotumia mchanganyiko wa lugha ya Kiswahili na Kiingereza, linashikilia nafasi ya pili kwa asilimia 18.1. Uchanganyaji wa lugha asili, Kiswahili na Kiingereza unashikilia nafasi ya tatu ukiwa na asilimia 6.9. Sheng' ni ya nne katika mpangilio huo ikiwa na asilimia 5.6. Lugha asili ni ya tano ikiwa na asilimia 4.2 na kufuatiwa na mchanganyiko wa lugha asili na Kiswahili, Kiingereza na lugha asili na mchanganyiko wa hizo lugha zote kwa asilimia 1.4. Mchanganyiko wa lugha ya Kiswahili na lugha ya Kiingereza unatumiwa kwa kiwango cha juu (17.8) ukilinganishwa na mchanganyiko mingine. Sababu kuu ni kwamba, katika kuchanganya lugha, kuna baadhi ya lugha ambazo hazipendelewi; hivyo, kuufanya mchanganyiko huo kutotumiwa na asilimia kubwa ya wanafunzi. Aidha, wazungumzi waweza kuwa wa kundi kabila tofauti.

Lugha ya Kiswahili na lugha ya Kiingereza ni lugha rasmi ambazo zina uwezo wa kuwapatanisha wanafunzi kama hawa walio na tofauti zilizokithiri kwa mujibu wa asili zao. Sifa hii inaufanya mchanganyiko wa lugha hizi kupendelewa na hivyo kuteuliwa ili kutumika na wanafunzi wengi. Katika kuchunguza lugha ambayo wanafunzi hutumia wanapokwenda kuhudhuria mihadhara, asilimia 58.9 ya washiriki walikiri kutumia lugha ya Kiingereza, asilimia 21.9 ya wanafunzi hutumia mchanganyiko wa lugha ya Kiswahili na lugha ya Kiingereza, ilhali asilimia 12.3 ya washiriki hutumia lugha ya Kiswahili.

Asilimia 2.7 ya wanafunzi walikiri kutumia mchanganyiko wa lugha asili, lugha ya Kiswahili na lugha ya Kiingereza. Huu pia ni muktadha ambao kutokana na matokeo hayo waweza kuchukuliwa kuwa na sifa za muktadha rasmi. Ilibainika kwamba, lugha ya Kiingereza ina umaarufu wa kutumika kama ilivyo na mchanganyiko wa lugha ya Kiswahili na lugha ya Kiingereza. Mchanganyiko wa lugha asili, lugha ya Kiswahili na lugha ya Kiingereza na mchanganyiko wa lugha hizo zote hauna umaarufu wowote kuashiria kuwa, mchanganyiko ya hizo lugha haitumiki sana katika muktadha huo. Hali hii ya lugha ya Kiingereza kuwa na idadi kubwa (58.9%) ya wanafunzi wanaoitumia wanapokwenda mihadharani, yaweza kuelezwa kama matokeo ya wanafunzi kujitayarisha kiakili. Muktadha wa mihadhara katika vyuo vikuu, hutambulishwa na urasimi, hali inayopelekea wanafunzi kuanza kujiandaa kusoma. Aidha, mihadhara hutolewa katika lugha ya Kiingereza na hivyo basi haina budi mwanafunzi awe amejiandaa kiakili kufunzwa.

Uwanjani, lugha asili ilikuwa na asilimia 9.6 ya wasailiwa, lugha ya Kiingereza 19.2%, lugha ya Kiswahili 46.6%, mchanganyiko wa lugha asili na lugha ya Kiswahili 2.7%, mchanganyiko wa lugha asili, lugha ya Kiswahili na lugha ya Kiingereza 6.8%, mchanganyiko wa lugha ya Kiswahili na lugha ya Kiingereza asilimia 11.0 ya wanafunzi, nayo lahaja ya Sheng' 1.4%. Kiswahili kilidhihirika kuwa na umaarufu wa kutumika katika muktadha huu. Tofauti na maoni ya (Kaniu 2003), lahaja ya Sheng' haitumiki sana na pia ule mkusanyiko wa lugha asili na Kiswahili. Hata hivyo, matokeo haya yalithibitisha uhalisia wa kuchanganya lugha.

Kutopendelewa kwa lugha ya Kiingereza, kwaweza kuelezwa kwa mujibu wa urasmi unaoambatanishwa na miktadha tofauti tofauti na lugha yenyewe. Lugha ya Kiingereza nchini Kenya huwa imetambuliwa kama lugha rasmi hivi kwamba hata katika matangazo ya michezo katika vyombo vya habari hufanywa kwa Kiswahili. Uhalisia huo unapelekea kuathiri pia hali ya utangazaji na matumizi ya lugha katika viwanja vyuoni. Uwanjani ni mahali pasipo na urasmi wowote wakati wowote hususan inapozingatiwa shughuli za michezo.

Katika muktadha wa kuota jua, mkusanyiko wa lugha ya Kiswahili na Kiingereza ulionekana kupendelewa. Wanafunzi asilimia 37 walijibu kuutumia. Hii ndio asilimia ya juu zaidi katika muktadha huu ikilinganishwa na asilimia zingine. Lugha asili katika muktadha huu inatumiwa na asilimia 5.5 ya wanafunzi, lugha ya Kiingereza inatumiwa na asilimia 2.7, ilhali lugha ya Kiswahili inatumiwa na asilimia 6.8 ya wanafunzi.

Uchanganyaji wa lugha asili na lugha ya Kiswahili ulikuwa na asilimia 8.2 ya washiriki ilhali mchanganyiko wa lugha asili na lugha ya Kiingereza unatumiwa na asilimia 5.5 ya wasailiwa. Mchanganyiko wa lugha asili, lugha ya Kiswahili na lugha ya Kiingereza ulibainika kutumiwa na asilimia 28.8 ya washiriki. Asilimia ya juu ya wanafunzi wanaotumia mchanganyiko wa lugha ya Kiswahili na lugha ya Kiingereza, yaweza kufafanuliwa kwa ukweli ulioibuka katika uchunguzi shiriki ambapo ilibainika kuwa, katika vikundi vya kubarizi jua, wanafunzi hawajigawi kwa misingi ya kikabila.

Matokeo hayo hata hivyo, yanabainisha kuwa kuna asilimia 28.8 ya wanafunzi ambao hutumia mchanganyiko wa lugha asili, lugha ya Kiswahili na lugha ya Kiingereza. Kitengo hiki cha wanafunzi, kiliwakilisha vikundi vya wanafunzi ambao huwa katika mgao wa kikabila. Vikundi hivi huwa si vikubwa sana kwani huwa na takriban wanafunzi wawili au watatu wakizidi sana.

Kawaida, katika vikundi hivi, iling'amuliwa kuwa, maswala ya kijamii (kama vile uhusiano na wachumba, ukosefu wa vitu vya kimsingi vya kutumia chuoni hususan kwa waliokuwa wakijipikia katika vyumba vyao vya kulala, ukosefu wa chakula) ndiyo yaliyojiri. Matumizi ya lugha asili katika vikundi hivi vya kubarizi jua, viliakisi dhana ya kuwatenga baadhi ya wanafunzi kutokana na maswala yaliyokuwa yakijadiliwa.

4. 4.1 Lugha katika Dhifa za Wanafunzi na katika michezo ya kuigiza

Katika sehemu hii, utafiti ulichunguza lugha inayotumiwa katika mikutano ya kiwilaya, lugha ya kuwasilisha michezo ya kuigiza, na katika dhifa za wanafunzi. Kwa upande wa dhifa za wanafunzi, matokeo yalikuwa ifuatavyo: Kiswahili kilitumika kwa asilimia ya juu kuliko lugha nyingine. Aghalabu, asilimia 34.7 ya wanafunzi walisema kuwa, wao hutumia lugha hii katika dhifa za kijamii vyuoni. Lugha ya Kiingereza inafuata huku ikiwa na asilimia 22.2 ya wasailiwa nayo lugha asili ni ya tatu ikiwa na asilimia 20.8 ya wasailiwa.

Mchanganyiko wa lugha ya Kiswahili na lugha ya Kiingereza uliwakilishwa na asilimia 18.1 ya wasailiwa. Ni bayana kuwa, lugha ya Kiswahili inapendelewa na wanafunzi wengi wakati wa dhifa za kijamii kuliko lugha hizo nyingine. Maelezo ya hali hii yaweza kutokana na ukweli kuwa, lugha hii huwa ya kati ambayo hainasibishwi na kundi kabila lolote wala haipendelei kabila lolote lile. Katika uchunguzi shiriki, ilibainika kuwa, katika dhifa hizi, wanafunzi hawabaguani kwa misingi ya kikabila. Asilimia 97.2 ya wanafunzi walisema kuwa, wao huzungumza lugha ya Kiswahili vyema, hivyo, inakuwa heri kwao kutumia lugha ya Kiswahili. Ingawa wanafunzi asilimia 97.2 (jedwali 10) walisema kuwa wao huzungumza lugha ya Kiingereza vyema, ilibainika kuwa, sio asilimia kubwa ya wanafunzi wanaotumia lugha hii katika dhifa kama hizo.

Katika uchunguzi shiriki, ilibainika kuwa, kwa kutumia lugha ya Kiingereza, ile hali ya urasmi inayoambatanishwa na lugha hii inajitokeza na hivyo kutoafiki muktadha kama huu. Ukosefu wa urasmi katika dhifa hizi, unaeleza hali ya lugha ya Kiswahili kupendelewa zaidi kwani inaafiki hali zote mbili. Mbali na hayo, ni lugha inayowaunganisha watu wa asili anuwai bila kuamsha hisia zozote za kikabila.

Ukosefu wa urasmi katika dhifa hizo husababisha matumizi ya lugha asili kwa kiwango cha asilimia 20.8. Lugha asili, hazina urasmi hivyo, zinaafiki muktadha huu. Hata hivyo, asilimia hii ni ya chini ikilinganishwa na asilimia 63 ya wanafunzi wanaotumia lugha ya Kiswahili.

Kulingana na uchunguzi shiriki ni kuwa, dhifa hizi zinakusudiwa kuwaleta wanafunzi pamoja ili washerehekee na wajiliwaze kutokana na kazi za usomi. Mialiko ya kuhudhuria dhifa hizi licha ya kujikita kwa marafiki, haibanwi na misingi ya kikabila. Hivyo basi, haifai kuwaalika wanafunzi kutoka kundi kabila tofauti kisha watengwe kwa mujibu wa lugha asili katika mijadala inayoendelea. Asilimia inayotumia lugha asili ni pale ambapo mzungumzaji anataka kumwambia mwenzake kitu kwa siri ambacho hataki wenzake wakijuwe. Hususan katika kusengenya na kuomba hisani za namna fulani na kufanya mizaha. Mambo ambayo yalibainika katika hali hii haswa ni maswala ya kujadili wapenzi na kutoa maoni kuhusu upatanifu wao. Michanganyiko ya lugha sio maarufu kama ilivyodhihirika. Sababu kuu ni kutokana na kutokuwa maarufu kwa lugha moja miongoni mwa muungano ule.

Ilibainika kuwa utawala wa lugha fulani katika matumizi katika maeneo hayo yote hutunga kuteuliwa kwa lugha moja na pia hulemaza mazoezi ya lugha katika stadi mbalimbali. Matokeo ni kwamba, wanafunzi hawapendelei kuzungumza katika lugha husika kutokana na ukosefu wa ufasaha katika lugha hiyo.

Katika kuchunguza lugha inayotumika kuwasilisha michezo ya kuigiza chuoni, ilibainika kuwa, lugha asili hutumika kwa kiwango cha chini sana kwani, ni asilimia 1.4 pekee ya wasailiwa waliojibu kuwasilishwa kwa michezo hii katika lugha hiyo. Lugha ya Kiswahili inatumika kwa asilimia 15.1 ilhali, lugha ya Kiingereza inatumika kwa asilimia 72.6.

Jedwali la 18: Lugha ya kuwasilisha michezo ya kuigiza

Lugha	Maratokezi	Asilimia
Lugha Asili	1	1.4
Kiswahili	11	15.1
Kiingereza	53	72.6
Kiswahili na Kiingereza	8	11.0
Jumla	73	100.0

Matokeo hayo yanaweza kuelezwa kuwa, kutumiwa kwa lugha asili kunajiponza kwa sababu kunafaa kuwe na mawasiliano baina ya waigizaji na watazamaji. Lugha asili zikitumika, haja hii haitatimia kwani, wanafunzi wasioifahamu lugha asili husika, hawataelewa na kushiriki

ipasavyo katika hafla hizi. Zaidi, hali hii inaweza kuambatanishwa na ujuzi karibu sawa wa lugha hizi mbili katika stadi mbalimbali za kuzitumia ambazo wanafunzi wanazo kufikia kiwango cha kuweza kuzitumia kwa pamoja katika hali ya kuchanganya na kugeuza lugha.

Stadi hizi huchangia mwanafunzi kuwa na mielekeo chanya kwa lugha hizi mbili hivi kwamba huwa anajiamini anapozitumia jambo linalochangia kuteuliwa kwa lugha ya Kiswahili na lugha ya Kiingereza.

Mbali na hayo, wanafunzi hawa ni wasomi ambao wameingiliwa na usasa kiasi cha kutoona umuhimu wa kutumia lugha asili zao na hivyo basi lugha ya Kiingereza inatumika kwa kiasi kikubwa. Pia, wanafunzi wa vyuo vikuu wamekulia katika mazingira ambayo tajiriba iliyopo ni kwamba, michezo mingi ya kuigiza imekuwa ikiwasilishwa kwa lugha ya Kiingereza; hivyo wanaiga yanaoyotendeka katika jamii pana. Hata hivyo, michezo ya kuigiza iliyo katika lugha asili imeanza kushika kani na kuwa maarufu katika kumbi za maigizo jambo ambalo huenda baadaye likaathiri hali ilivyo sasa katika vyuo vikuu. Wanafunzi wengi (91.8%), walisema kwamba, wanapendelea lugha ya Kiingereza inapotumika katika hali ya kuandika. Pia, katika jedwali 4 (uk.39), wanafunzi wengi (97.2%) walisema kwamba, wao huzungumza lugha ya Kiingereza vyema. Matokeo hayo yanalenga kufafanua matokeo haya ya kupendelewa sana kwa lugha hii katika kuwasilisha michezo ya kuigiza. Kutoteuliwa kwa lugha asili kunaweza kufafanuliwa kwa misingi ya utamaduni wa Waafrika. Utamaduni wa Waafrika hufuata miiko ya lugha na kuzungumzia mambo ya aibu kwa kutumia lugha inayokubali aibu katika uhalisia wake. Hata hivyo, idadi kubwa ya wanafunzi walikiri kutopendelea lugha hii inapotumika katika hali ya kuzungumza chuoni. Takriban asilimia 55.6 ya wanafunzi wote walioshirikishwa walijibu kutoipendelea lugha ya Kiingereza katika hali hiyo.

4.4.2 Lugha ya kuwasiliana na Wauzaji wa kundi Kabila

Hapa utafiti uliazimia kuchunguza utambulisho wa kikabila unavyoathiri uteuzi wa lugha fulani badala ya nyingine. Mtafiti alichunguza ni kwa mara ngapi ambapo msailiwa hutumia Kiswahili, Kiingereza au lugha asili kuwasiliana na muuzaji wa kundi kabila lake na au asiye wa kundi Kabila lake. Kipimo cha upendelevu cha Likert kilichokuwa na viwango vitatu: - hatumii, mara chache na mara nyingi kilitumika kuyaratibu majibu. Katika hali ya kwanza (muuzaji wa kabila lake), asilimia 54.8 ya wanafunzi walisema kuwa wanatumia lugha ya Kiswahili kwa mara chache wanapohudumiwa na muuzaji wa kabila lao.

Asilimia 31.8 ya wanafunzi walisema kwamba hutumia lugha ya Kiswahili mara nyingi wanapohudumiwa na muuzaji wa kundi kabila lao ilhali asilimia 13.7 ya wanafunzi hawatamii lugha hii katika shughuli hiyo. Matokeo hayo yanadhihirika waziwazi katika jedwali lifuatalo.

Jedwali la 19: Utumiaji Kiswahili na Muuzaji wa kundi kabila

Mara ngapi unatumia Kiswahili	Maratokezi	Asilimia
Hatumii	10	13.7
Chache	40	54.8
Nyingi	23	31.5
Jumla	73	100.0

Inadhihirika kuwa, lugha ya Kiswahili haina umaarufu katika huduma za ununuzi hususan ikiwa muuzaji ni wa kundi kabila la mwanafunzi kwani, kutokana na jedwali hilo, zaidi ya asilimia 50 ya wanafunzi walijibu kuwa hakuna wakati ambao wanatumia Kiswahili na kama watakitumia ni kwa kiasi cha mara chache.

Katika kuchunguza idadi ya wanafunzi wanaotumia lugha ya Kiingereza na muuzaji wa kundi kabila, ilidhihirika asilimia 52.1 ya wasailiwa hutumia lugha ya Kiingereza kwa mara chache, ilhali asilimia 43.8 ya wanafunzi hawatamii lugha ya Kiingereza kuwasiliana na muuzaji wa kabila lao wanapohudumiwa naye. Asilimia 4.1 ya wanafunzi huitumia lugha hii kwa mara nyingi. Vilevile, kama ilivyo katika kutumiwa kwa lugha ya Kiswahili, inabainika kuwa, lugha ya Kiingereza kwa kiasi kikubwa hutumiwa mara chache katika hali hii.

Jedwali la 20 (uk 67) linaonyesha asilimia 74 ya wanafunzi wanaowasiliana kwa lugha asili na muuzaji wa kundi kabila lao. Asilimia 19.2 ya wanafunzi hutumia lugha asili kwa mara chache ilhali ni asilimia 6.8 pekee ya wanafunzi ambao hawatamii lugha asili kuwasiliana na muuzaji wa kundi kabila lao. Kwa kuzingatia matokeo hayo, ilidhihirika kuwa, utambulisho wa kikabila unatawala uteuzi wa lugha katika hali hii. Kwa mujibu wa jedwali la 20 jumla ya asilimia 93.2 ya wanafunzi hutumia lugha asili kuwasiliana na wenye duka wa kabila lao (19.2% kiwango cha mara chache na 74% kiwango cha mara nyingi).


Ingawa lugha asili inashikilia nafasi ya kwanza katika kuteuliwa na kutumika, ni wazi kuwa, hata lugha ya Kiingereza na ya Kiswahili zinatumiwa ingawa kwa asilimia ndogo

ikilinganishwa na ile ya lugha asili. Hali hii inaweza kuelezwa kwa msingi kuwa, wengi wa wanafunzi wangependa kuzua uhusiano mwema na wa karibu na wenye duka ili kuweza kupata turuhani na au kuuziwa bidhaa kwa bei iliyopunguzwa au hata kukopeshwa bidhaa.

Aidha, ilibainika kuwa, wengi hupiga hatua moja zaidi na kuzua majina yanahusishwa na kabila fulani. Katika hali moja ilishuhudiwa washiriki wakitambuana kwa jina “Nyumba” ambalo ni maarufu sana katika jamii ya Wakikuyu na hutumika na watu wenye uhusiano wa karibu.

Jedwali la 20: Utumiaji lugha asili na Muuzaji wa kundi kabila

Mara ngapi unatumia lugha asili	Maratokezi	Asilimia
Hatumii	5	6.8
Chache	14	19.2
Nyingi	54	74.0
Jumla	73	100.0



Hata hivyo, kwa kuwa wauzaji hawa walipitia mfumo rasmi wa elimu nchini, wana ufahamu wa lugha ya Kiingereza na lugha ya Kiswahili hali inayofafanua matumizi ya lugha hizo. Pia kuwepo katika chuo kikuu hunasibishwa na kuwa msomi. Sifa moja ya kuweza kutambuliwa kama msomi ni kuweza kutumia lugha ya Kiingereza. Hata kama wauzaji hawa hawajimudu kuwasiliana kwa lugha ya Kiingereza, kuwepo katika chuo kikuu kunawashinikiza kuitumia.


4.4.3 Lugha na Muuzaji asiye wa Kundi kabila la Mwanafunzi

Katika sehemu ya pili ya kutumia lugha, wauzaji wasio wa kundi kabila la mnunuzi walichunguzwa. Sehemu hii ilifaa ili kuthibitisha ile sehemu ya kwanza. Ni dhahiri kuwa kuna tofauti kama inavyodhihirika katika matokeo haya. Katika jedwali la 21 uk.68, asilimia 84.9 ya wanafunzi walikiri kwamba wanatumia lugha ya Kiswahili mara nyingi kuwasiliana na muuzaji asiye wa kundi kabila lake. Asilimia 13.7 ya wasailiwa wakasema kuwa wanaitumia lugha hii kwa mara chache, nayo asilimia 1.4 ya wasailiwa wakajibu kutotumia lugha ya Kiswahili.

Matokeo hayo yalibainisha kuwa, lugha ya Kiswahili ilipendelewa sana katika kuwasiliana na muuzaji asiye wa kundi kabila la mwanafunzi. Asilimia 84.9 ya wanafunzi walisema kuwa huitumia lugha ya Kiswahili ikilinganishwa na asilimia 24.7 ya wanafunzi ambao walisema kwamba hutumia lugha ya Kiingereza mara nyingi. Uhalisia ulioibuka ni kuwa, katika kile kiwango cha “mara nyingi”, hakuna mwanafunzi yeyote aliyesema kwamba anatumia lugha asili anapohudumiwa na muuzaji asiye wa kundi kabila lake.

Jedwali la 21: Utumiaji Kiswahili na Muuzaji asiye wa kundi kabila

Mara ngapi unatumia Kiswahili	Maratokezi	Asilimia
Hatumii	1	1.4
Chache	10	13.7
Nyingi	62	84.9
Jumla	73	100.0



Idadi kubwa ya wanafunzi (93.2%) hawa wakiwa ni zaidi ya robo tatu ya wasailiwa, walijibu kwamba hawatumii lugha asili wanapohudumiwa na muuzaji asiye wa kundi kabila ikilinganishwa na asilimia 8.3 ya wanafunzi ambao walisema kwamba wao wanatumia lugha ya Kiingereza na asilimia 1.4 ya wanafunzi ambao hutumia lugha ya Kiswahili katika kipimo hicho. Katika kutumia lugha kwa kiwango cha mara chache, lugha ya Kiingereza ilikuwa na idadi ya juu ya wanafunzi ikilinganishwa na lugha asili na lugha ya Kiswahili. Kupendelewa kwa lugha ya Kiswahili kunaweza kuelezewa kwa mujibu wa uhalisia wa lugha hii kuwa, lugha ya taifa.

Mbali na ufafanuzi huo, hivi leo, lugha ya Kiswahili inatumika kwa mapana na marefu kwa sababu ni lugha ya taifa. Aidha ni lugha sambazi na lingua franca. Basi, inadhihirika kuwa, uteuzi wa lugha unaathiriwa na asili ya wahusika ya kabila lao ndiposa lugha asili hazitumiki kwani, ingawa zinafanya kazi ya utambulisho wa kikabila na kuwaunganisha wanafunzi, zinawatenganisha na kuwabagua na makundi mengine. Uvumbuzi huo unalingana na matokeo ya Tchai (1991) kuwa, lugha za kiasili hazionekani kuwa na umuhimu na nafasi yoyote katika biashara. Hata hivyo, ugunduzi wake una mashiko pale ambapo hisia za kutaka kujitambulisha na muuzaji hazijiri.

4.4.4 Lugha nje ya Darasa na Wanafunzi wa kundi Kabila

Hii sehemu ilinuiwa kuthibitisha kweli utambulisho wa kiethnoisimu unaathrii uteuzi wa lugha nje ya darasa na pia kuweka uhakika katika ruwaza za matumizi ya lugha. Makisio yaliyokuwa ya kati katika swali hili ni kuwa wahusika wangukuwa huru kutumia lugha pasi kujali kutoelewana. Kwa mujibu wa jedwali la 22 hapa chini, lugha asili ilibainika kuwa ilitumika kwa kiwango cha juu kwani asilimia 39.7 ya wanafunzi walisema kwamba huitumia.

Jedwali 22: Lugha nje ya darasa na wanafunzi wa kundi kabila

Lugha ambayo mwanafunzi anatumia	Maratokezi	Asilimia
Lugha Asili	29	39.7
Kiswahili	6	8.2
Kiingereza	3	4.1
Kiswahili na Kiingereza	9	12.3
Lugha Asili na Kiswahili	16	21.9
Lugha Asili na Kiingereza	5	6.8
Lugha Asili, Kiswahili na Kiingereza	3	4.1
Jumla	71	97.3
Waliokosa kujibu	2	2.7
Jumla	73	100.0

Mchanganyiko wa lugha asili na lugha ya Kiswahili unafuata kwa asilimia 21.9 ya wasailiwa. Mchanganyiko wa lugha ya Kiswahili na lugha ya Kiingereza ni wa tatu kwa asilimia 12.3 ya washiriki ilhali lugha ya Kiswahili ni ya nne ikiwakilishwa na asilimia 8.2 ya wanafunzi. Mchanganyiko wa lugha asili na lugha ya Kiingereza unashikilia nafasi ya tano kwani ni asilimia 6.8 pekee ya wanafunzi waliokiri kuutumia na wanafunzi wa kundi kabila. Lugha ya Kiingereza inashikilia nafasi ya sita katika msururu huo kwa asilimia 4.1 kama ilivyo na ule mchanganyiko wa lugha asili, lugha ya Kiswahili na lugha ya Kiingereza.

Ushamiri wa mchanganyiko kati ya lugha asili na lugha ya Kiswahili unatokana na uhalisia uliobainika katika jedwali za 19 na 20 zilizoangazia lugha inayotumika baina ya wanafunzi na wenye maduka wa kabila lao. Katika jedwali la 19, asilimia 31.5 ya wanafunzi walisema kuwa wanapendelea lugha ya Kiswahili kuwasiliana na wauzaji hawa. Hii (31.5%) ni asilimia ya juu ikilinganishwa na asilimia 4.1 pekee ya wanafunzi waliokiri kutumia lugha ya Kiingereza kuwasiliana na wenye maduka mara nyingi. Katika jedwali 20, asilimia 74 ya wanafunzi walikiri kutumia lugha asili kuwasiliana na wauzaji wa kabila lao mara nyingi.

Matokeo haya yanapelekea kupendelea kutumia lugha asili na lugha ya Kiswahili aidha kila moja ikijisimamia au kwa kuzichanganya hususan iwapo washiriki ni wa kundi kabila moja. Kwa mujibu wa matokeo hayo ni wazi kuwa ule utambulisho wa kiethnoisimu unatawala uteuzi wa lugha ya kutumika. Aidha kauli hii inabainisha kuwa, kuna uhusiano kati ya ukabila na lugha ambayo ilituuliwa kutumika. Pia, ilibainika kuwa asilimia kubwa ya wanafunzi hutumia lugha asili zao jambo ambalo linadhihirisha umuhimu wa utambulisho wa kiethnoisimu na kundi kabila la washiriki.

Ingawa lugha ya Kiingereza hunasibishwa na wanafunzi wa daraja kama hili la usomi, ilibainika kuwa, lugha hii sio maarufu na haitumiwi sana wakati wanafunzi wa kundi kabila wanapowasiliana wao wenyewe. Sababu ya hali kuwa hivi ni kwamba, nje ya darasa huakisi muktadha ambao sio rasmi; hivyo, wanafunzi wanafuata kaida za urasimi na hali zisizo rasmi. Hata hivyo, kuna asilimia ndogo ya wanafunzi ambao wanatumia lugha ya Kiingereza kuwasiliana na wanafunzi wa kundi kabila lao. Sababu kuu ya wanafunzi kupendelea lugha asili zao ni kwamba, bado Wakenya wengi wanazionea fahari lugha asili zao. Isitoshe, lugha hizi huwa amali ya kuhifadhi utamaduni wao. Aidha, kwa kutumia lugha asili kuwasiliana, washiriki wanaonyesha umoja wao. Matokeo hayo yanapewa mashiko na jedwali lifuatalo (jedwali 24 uk 71) linaloangazia hali hiyo ingawa kwa kuangazia wanafunzi wasio wa kundi kabila na mzungumzi.

Katika jedwali la 20, lugha asili haitumiwi na asilimia kubwa ya wanafunzi, kuonyesha kudidimia kwa umuhimu wa lugha hii katika mawasiliano baina ya wanafunzi ambao sio wa kundi kabila. Huo ni ugunduzi ambao unapelekea kuthibitisha kwamba kuna uhusiano kati ya ruwaza za matumizi ya lugha, ukabila na mielekeo kwa lugha. Lugha asili inatumika na asilimia 1.4 pekee ya wasailiwa kama ilivyo kwa lahaja ya Sheng. Hii ni asilimia ya chini mno ikilinganishwa na asilimia 27.8 ya wanafunzi wanaotumia lugha ya Kiswahili na asilimia 19.4 ya

wanafunzi wanaotumia lugha ya Kiingereza. Uchanganyaji wa lugha ya Kiswahili na lugha ya Kiingereza unatumiwa kwa kiasi kikubwa ambapo asilimia 46.6 ya wasailiwa walijibu kuutumia. Matokeo haya yanaweza kuelezwa kwa mujibu wa ukweli kuwa, ikiwa washiriki watateua lugha asili ili waitumie na wanafunzi wasio wa kundi kabila lao, ile haja ya kuwasiliana haitakuwepo kwani katika uchunguzi shiriki, ni asilimia chache mno ya wanafunzi ambao wanafahamu lugha asili za makundi kabila mengine.

Jedwali 23: Lugha nje ya darasa na Wanafunzi wasio wa kundi kabila

Lugha	Maratokezi	Asilimia
Kiswahili	20	27.4
Kiingereza	14	19.2
Kiswahili na Kiingereza	34	46.6
L.A, Kiingereza na Kiswahili	2	2.7
Lugha Asili	1	1.4
Sheng'	1	1.4
Jumla	72	98.6
Waliokosa kujibu	1	1.4
Jumla	73	100.0

Katika jedwali la 3, ni asilimia 20.5 na 2.7 ya wasailiwa waliosema kwamba wanatumia lugha nne na tano. Hiyo ndio asilimia inayowakilishwa na asilimia 1.4 ya wanafunzi wanaotumia lugha asili na washiriki wasio wa kundi kabila kwani mzungumzi anielewa lugha asili ya msikizi au msikizi anaifahamu lugha ya mzungumzaji. Pia, kuna haja ya kutaka kuonyesha upatanifu wa kilugha na mshiriki asiye wa kundi kabila. Haja hii ya upatanifu wa lugha ilionekana kugemea sana kwa upande wa lugha ya kundi kabila linalotawala na lililo na nguvu kisiasa. Katika mazingira yaliyotafitiwa, wazungumzi wengi walionyesha upatanifu wa kilugha kwa upande wa lugha za makundi kabila yaliyo na ushawishi mkubwa aidha kiuchumi, kijamii au kisiasa.

Ilibainika kuwa, katika kuchanganya lugha miongoni mwa wanafunzi, uchanganyi huu umeshamiri zaidi kati ya lugha ya Kiswahili na lugha ya Kiingereza katika muktadha huu kuliko lugha nyingine zozote chuoni. Hali hii inatokana na umahiri wa wanafunzi wa vyuo vikuu wa lugha hizo ukilinganishwa na umahiri wa lugha nyingine zitumikazo vyuoni. Wanafunzi wengi, wana tajiriba kubwa katika lugha ya Kiingereza na lugha ya Kiswahili kwani ndizo lugha ambazo wamekumbana nazo kwa kiasi kikubwa tangu kujiunga na masomo. Basi, inawawia rahisi kuzitumia lugha hizo aidha kila moja ikijisimamia au kwa kuzichanganya. Juu ya hayo, kwa kuchunguza matumizi ya lugha na wauzaji wasio wa kundi kabila, hakukuwa na wanafunzi wowote waliotumia lugha asili kuwasiliana nao.

4. 4.5 Lugha ya Maingiliano.

Kuhusu lugha ambayo washiriki hutumia wanapokutana na wakubwa wa chuo wa kabila lao nje ya darasa, asilimia 90 ya wasailiwa walisema kuwa wao hutumia lugha ya Kiingereza. Lugha ya Kiswahili hutumiwa na asilimia 5.6 ya wanafunzi katika mawasiliano baina yao na wakuu wa chuo. Asilimia 4.4 ya wanafunzi walisema kuwa wao huchanganya lugha lugha ya Kiswahili na lugha ya Kiingereza. Uhalisia wa ruwaza za matumizi ya lugha miongoni mwa wanafunzi na wahadhiri unadhihirika.

Katika muktadha huu, lugha ya Kiingereza inatumika kwa asilimia ya juu (90 %) kuliko lugha nyingine. Kiswahili hakitumiki sana kama ilivyo na kuchanganya lugha ya Kiswahili na lugha ya Kiingereza. Ufafanuzi wa hali hii unatokana na nafasi ambazo wakubwa hawa wanashikilia katika chuo na pia ofisi zao. Kutokana na hali hiyo wanafunzi wanabidiika kuleta hali ya urasmi nje ya ofisi kwa kuheshimu ofisi ya mshiriki na pia hadhi ya mhusika. Licha ya kuwa wakuu wa vyuo wanashuhudia na wamo ndani ya mazingira ambapo lugha huchanganywa, tofauti za kiumri zinaathiri sana hali ya kuchanganya lugha. Lugha asili haitumiki. Matokeo haya yanathibitisha kuwa, lugha asili na lugha ya Kiswahili zikiwekwa pamoja, lugha ya Kiswahili itapendelewa.

Katika sehemu hiyo ya matumizi ya lugha katika maeneo mbalimbali, inabainika kuwa uteuzi wa lugha moja badala ya nyingine unatawaliwa kwa kiasi na mielekeo ambayo wanafunzi wanayo kwa lugha husika. Pia, ule utambulisho wa kiethnoliusimu unatawala uteuzi wa lugha; hivyo/ kuathiri kwa kirefu ni lugha ipi itatumika wapi na miongoni mwa akina nani.

Kwa mujibu wa nadharia ya kitendo kilichofikiriwa, watu hutathmini kitendo kabla ya kutenda. Utathmini huo hufanywa kwa kupima manufaa ya kitendo hicho kwa mtu binafsi na kwa watu wengine muhimu katika jamii ya mtendaji huyo, kauli hizo ziliweza kuthibitika katika sehemu hiyo. Kwa mfano, katika kuangazia lugha ambayo wanafunzi wanatumia na wamiliki maduka wa kundi kabila lao, wanafunzi wengi walikiri kutumia lugha asili ili kuweza kupata turuhani.

Ili kujitambulisha na mwenye duka ambaye kwa mujibu wa nadharia ya kitendo kilichofikiriwa ni mtu mhimu katika jamii ya mwanafunzi, ile kauli ya utambulisho wa kiethnoisimu iliyoasisiwa na nadharia ya utambulisho wa kiethnoisimu inathibitika ambapo wanafunzi wanatumia lugha asili zao ili kuzua umoja na ukuruba na wenye maduka. Ilibainika hata wanafunzi wasio wa kundi kabila la mwenye duka hujaribu kuzua dhana ya upatanifu wa lugha ili kuweza kuzua uhusiano wa karibu nao. Pia, ilibainika kuwa, lugha asili haiwezi kutekeleza majukumu yote ya shughuli za kila siku za wanafunzi; ndiposa lugha za Kiingereza, Kiswahili na lahaja ya Sheng' zinapata fursa ya kutumika vyuoni. Ilibainika kuwa, lugha ya Kiingereza ndiyo lugha ya pekee ya kutolea arifa vyuoni kwani arifa hizi hulenga kila mwanafunzi.

4.5 Hitimisho

Kazi hii ilichunguza uteuzi na matumizi ya lugha katika vyuo vikuu hususan katika chuo kikuu cha Egerton. Matumizi ya lugha ya Kiswahili, Kiingereza na lugha asili katika maeneo mbalimbali yalichunguzwa. Utafiti umeonyesha jinsi katika vyuo vikuu kuna makundi kabila anuwai. Kwa mujibu wa jedwali la kwanza (uk.33), kuna makundi kabila takriban 16 chuoni jambo linalodhihirisha kuwepo kwa makabila mbalimbali chuoni. Mbali na hayo, matokeo ya utafiti yamebainisha kuwa chuoni kuna matumizi ya lugha tatu kwa kuwa asilimia kubwa (69.9) ya wanafunzi walikiri kutumia lugha tatu. Hizi ni: lugha ya Kiswahili, lugha ya Kiingereza na lugha asili. Hata hivyo, ilibainika kuwa lugha hizi hutumika kwa viwango tofauti na hususan kwa kutegemea mahali alipo mzungumzi na mielekeo aliyonayo kwa lugha.

Kwa upande wa mielekeo, ilibainika kwamba wanafunzi wana mielekeo changamani kwa lugha zilizohusishwa katika utafiti. Kwa kuwa lugha hutumika katika namna mbalimbali kama vile kuandika, kusoma na kunena, ilibainika kuwa wanafunzi wanaweza kuwa na mielekeo

chanya kwa lugha fulani inapotumika katika hali ya maandishi lakini wasiiteue kuitumia kwa namna nyingine. Hali hii ilidhihirika ambapo kulikuwa na asilimia kubwa ya wanafunzi kwa mfano ambao walisema kwamba hawapendelei lugha asili inapotumika katika hali ya maandishi ilhali walikiri kwamba wanaizungumza vyema. Hata hivyo, ilibainika kuwa wanafunzi wengi wana mielekeo chanya kwa lugha ya Kiingereza na mielekeo hasi kwa lugha asili na lugha ya Kiswahili.

Uvumbuzi huo ndio uliophelekea kuweka wazi ruwaza za matumizi ya lugha katika vyuo vikuu na kubainika kwamba, kuna ruwaza zilizokithiri na bainifu za matumizi ya lugha katika vyuo vikuu. Katika mgao wa maeneo ya matumizi ya lugha uliobainishwa na watalamu kama vile Fishman, kuna maeneo rasmi na maeneo yasiyo rasmi. Utafiti huu ulizingatia maeneo yasiyo rasmi. Katika maeneo ya vyumba vya kulala, ilibainika kwamba lugha asili ndio lugha ambayo hutumika sana haswa ikizingatiwa kwamba wanafunzi huweza kuamua kuishi katika chumba kimoja na wenzao wa kutoka kundi kabila lao. Hali hiyo ni tofauti na hali ilivyo wakati wanafunzi wanaenda kuhudhuria mihadhara ambapo lugha inayoteuliwa kutumika ni lugha ya Kiingereza.

Katika vikundi vya kubarizi jua, wanafunzi hutumia mchanganyiko wa lugha ya Kiswahili na lugha ya Kiingereza tofauti na lugha ambayo wanafunzi hutumia wanapohudumiwa na wauzaji ambao ni wa kundi kabila lao ambapo wanatumia lugha asili. Katika vyumba vya maakuli, ilibainika kwamba wanafunzi huteua lugha ya Kiswahili na kuitumia kwa kiwango cha juu kuliko lugha zile zingine. Ilibainika kwamba, lugha asili na Kiswahili hutumika sana katika mawasiliano miongoni mwa wanafunzi na wenye duka wa kundi kabila lao aidha kila lugha ikijisimamia au kwa pamoja kwa kuchanganywa.

Matokeo hayo yalilingana na uvumbuzi wa Grojean (1982) kuwa, mzungumzaji wa lugha mbili au zaidi, huwa mzungumzi-msikizi mahiri ambaye amekuza umahiri wa kimawasiliano ambapo anaweza kutumia lugha moja au ile nyingine au zote mbili kwa pamoja katika ile hali ya kuchanganya lugha. Kwa sababu hii, wanafunzi wanaweza kufanya uteuzi kutegemea namna nne za uteuzi wa lugha (lugha zile mbili au zaidi na mitindo au mifumo mbalimbali ya kuchanganya au kuhamisha lugha kwa vile wana uwezo wa kuchanganya na kuhamisha lugha katika lugha zote). Hata hivyo, hali hii haijapelekea kutotumika kwa lugha ya Kiingereza chuoni kwani kama ilivyodhihirika, kuna majukumu ambayo lugha asili imeshindwa kuyatekeleza hususan kama lugha ya kutolea mafunzo.

Ilidhihirika pia kuwa, mzungumzi huteua lugha kwa kuzingatia anayezungumziwa. Kwa wanafunzi, uteuzi kama huu unaelekea kuathiriwa na dhana za kijamii na mihimuko, kiisimu, mada na kinafsia.

SURA YA TANO

MUHTASARI, HITIMISHO NA MAPENDEKEZO

5.1 Utangulizi

Katika sura hii, mambo muhimu yaliyoibuka kutokana na utafiti uliofanywa yanarejelewa. Pia, inaelezea mafanikio na matatizo yaliyokumba mtafiti. Mwisho wa sura hii mapendekezo yatatolewa kuhusiana na maeneo ya kufanyiwa utafiti zaidi.

5.2 Muhtasari

Utafiti huu ulichunguza hali ya matumizi ya lugha ilivyo katika vyuo vikuu haswa kwa kuzingatia lugha tatu; Lugha asili (lugha zote za kikabila katika utafiti wa tasnifu hii, ziliweka katika kundi hili), lugha ya Kiswahili na lugha ya Kiingereza. Mjadala uliendelezwa jinsi ukabila na mielekeo ya wanafunzi inavyoathiri uteuzi na matumizi ya lugha vyuoni kwa kutumia chuo kikuu cha Egerton kama mfano. Katika vyuo vikuu, kwa ambavyo kuna makabila mengi, kuna lugha nyingi zinazotumika kwa pamoja. Hali hii hupelekea wanafunzi kuteua lugha moja badala ya nyingine ili kuitumia katika kuwasiliana. Kutokana na uteuzi na matumizi hayo ya lugha, kazi hii imeonyesha jinsi kuna ruwaza zilizokithiri za matumizi ya lugha katika vyuo vikuu.

Azima kuu ya utafiti huu ni kuonyesha jinsi ukabila na mielekeo kwa pamoja huathiri uteuzi na matumizi ya lugha katika vyuo vikuu. Hata hivyo, kuna dhana nyingine kama vile kuchanganya lugha ambazo zilibainika katika mazingira ya wingi lugha. Mwelekeo kama huu ulidhihirika katika vyuo vikuu, na hivyo umejadiliwa katika tasnifu hii pasi kupotoka kutoka kwa azima kuu. Mpangilio wa tasnifu hii kwa upana basi unaakisi mikabala mitatu muhimu katika utafiti wa jinsi ukabila na mielekeo ya wanafunzi inaathiri uteuzi wa lugha vyuoni.

Kwanza, kuna mtazamo wa uchanganuzi wa maeneo ambao huhusisha vipengele kama vile, washiriki, mahali na mada. Vipengele vya washiriki na mahali vilikuwa muhimu haswa katika kubainisha ruwaza za matumizi ya lugha miongoni mwa wanafunzi; hivyo kuweza kutimiza lengo la pili la utafiti wa tasnifu hii. Mkabala wa pili unahusu dhana za kinafsia na kipengele muhimu hapa ni utambulisho wa kiethnoisimu. Mkabala huu ulifaa hususan katika kuweza kutambulisha athari za wanafunzi kutaka kujitambulisha na kundi kabila lao na basi kuweza kuteua lugha yao asili kwa ajili ya matumizi.

Tatu ni mkabala wa mbinu za kiantropolojia katika kutafitia uteuzi wa lugha. Kwa mujibu wa mkabala huu, uteuzi wa lugha lazima ubainishe jambo kuhusiana na mielekeo ya wazungumzaji kwa lugha katika jamii za wingi lugha. Mojawapo ya madhumuni ya utafiti huu ilikuwa ni kubainisha mielekeo ya wanafunzi kwa lugha wanazozitumia. Aidha, eneo lililotafitiwa ni kiunzi kidogo cha jamii yenye wingi lugha.

Ili kuweka wazi madhumuni yaliyotafitiwa, tasnifu hii imegawika katika sura tano kuu. Katika sura ya kwanza, usuli wa mada, mada ya utafiti, madhumuni na nadharia tete za utafiti zinashirikisha kiini cha sura hii. Zaidi ya hayo, sura hii inajadili kwa kifupi sababu za kuchagua mada na upeo na mipaka ya utafiti. Sura ya pili ni mapitio ya yaliyoandikwa kuhusiana na mada ya utafiti. Maadishi haya yamechunguzwa kwa kina pamoja na nadharia zilizoongoza utafiti wenyewe. Sura hiyo (ya pili) ni tahakiki ya kazi mbalimbali zinazohusiana na mada ya utafiti. Aidha, ni katika sura hii ambapo kuna kutalii kwa kina nadharia zilizotumiwa katika utafiti. Katika sura ya tatu, mbinu za utafiti na vifaa vilivyotumika kukusanya deta, uteuzi wa sampuli na wasailiwa na vile vile ukusanyaji na kukodiwa kwa deta kumeshughulikiwa.

Katika sura ya nne, mtazamo mpana wa kisosiolojia na kiisimujamii ulichukuliwa katika kueleza matokeo ya utafiti. Utafiti huu ulichukuwa mtazamo wa kijamii kwa mujibu wa uteuzi na matumizi ya lugha. Mtazamo huu ulichukuliwa kwani deta iliyokusanywa ilikuwa sare kwa mujibu wa mwelekeo wa vikundi na ruwaza za matumizi ya lugha. Wakati huo huo, wanafunzi ambao waliteuliwa kuwa wasailiwa, walioshirikisha jumuiya iliyotafitiwa, iliwabidi kufanya maamuzi aidha kutumia au kutotumia lugha zilizozingatiwa katika utafiti uliofanywa.

Zaidi ya hayo, kwa vile maamuzi ya kibinafsi hufanywa na mikakati ya kibinafsi kutekelezwa, kuna kuhusishwa kwa baadhi ya vibadiliki vya kijamii kama vile ukabila na mielekeo katika utafiti uliofanywa. Kufikia hapo, tasnifu hii inatoa rai kuwa nadharia ya kitendo kilichofikiriwa na utambulisho wa kiethnoisimu ziliweza kutoa mchango wenye thamani kubwa na kutoa umaizi wa utaratibu unaohusika katika uteuzi na matumizi ya lugha katika jamii yenye wingi lugha katika miktadha tofauti tofauti.

5.3 Muhtasari wa Matokeo Muhimu

Ilibainika kuwa vyuo vikuu huwa viunzi vidogo vinavyoakisi jamii nzima. Hili lilidhihirika kupitia matokeo kwamba, jamii ya vyuo vikuu huwa anuwai na yenye lugha nyingi. Matokeo haya yalielekeza katika ukweli kwamba, kuna lugha nyingi zinazotumiwa na wanafunzi katika shughuli zao za kila siku. Katika mkusanyiko wa lugha wanazozitumia wanafunzi, asilimia 69.9 walisema kuwa wao hutumia lugha tatu. Basi ilibainika kuwa hali ya matumizi ya lugha tatu ipo katika vyuo vikuu na ni hali ya kudumu. Katika utafiti, ilibainika kwamba katika chuo kikuu cha Egerton, kuna makundi kabila takriban 16 (Wakikuyu, Wameru, Wakamba, Waembu, Wataita, Waluhya, Wajaluo, Wakalenjin, Wagiriana, Wamaasai, Waturkana, Warendille, Waboran, Wakisii, Wachonyi na Wasomali) na ambayo tofauti zao kilugha na kiutamaduni haziwezi kupuuzwa.

Pili kuna ruwaza bainifu za matumizi ya lugha vyaoni katika miktadha ya hali zisizo rasmi. Lugha ya Kiswahili inatumika na kupendelewa sana katika vyumba vya maakuli, uwanjani, na katika sherehe za kuzaliwa. Katika vikundi vya wanafunzi wakiota jua, mchanganyiko wa lugha ya Kiswahili na lugha ya Kiingereza ulitumika sana. Ingawa lugha ya Kiingereza ina hadhi kuliko lugha ya Kiswahili na lugha asili, haijakuwa kikwazo katika kutumiwa kwa lugha hizo. Kutokana na ukweli huo, tasnifu hii inatoa rai kuwa, lugha hii inafaa katika kazi na miktadha mbalimbali.

Ilidhihirika kuwa, uwezo wa wanafunzi wa kutumia lugha huwa muhimu katika uteuzi na matumizi ya lugha. Aidha, uwezo huu huchangia pakubwa mielekeo ya wanafunzi kuhusiana na lugha. Asilimia kubwa ya wanafunzi walikiri kwamba hawapendelei kutumia lugha ya Kiswahili na lugha asili katika hali ya kuandika, kusoma, kusikiliza na kuzungumza; hivyo, ni ithibati kwamba, wanafunzi wa vyuo vikuu wana mielekeo hasi kwa lugha hizi hususan zinapotumika katika hali hizo. Mfumo wa elimu una nafasi ya kati sana katika ukuaji wa kibinafsi na wa kijamii wa mtu. Uwezo na stadi za mawasiliano za kutumia lugha kwa umahiri ni muhimu kwa mwanafunzi yeyote yule kwani kila wakati anatumia lugha. Ilibainika kuwa vyombo vya habari vina nafasi muhimu katika kuchangia uteuzi na matumizi ya lugha. Vipindi vya runinga na redio vinaweza kukuzwa kwa minajili ya elimu. Nchini Kenya, runinga inatoa nafasi bora zaidi katika kutangaza na kuzipa hadhi lugha za Kiswahili na Kiingereza, lakini juhudi zaidi lazima zifanywe katika kukuza lugha asili.

Vile vile, ilidhihirika kwamba, kuna kuchanganya lugha kunakohusu lugha za kiasili, Kiswahili na Kiingereza ingawa kwa viwango tofauti na kutegemea muktadha walimo washiriki. Zaidi ya hayo, ilibainika kuwa, mielekeo ya wanafunzi kwa lugha wanazozitumia na pia utambulisho wao wa kiethnoisimu unaathiri uteuzi na matumizi ya lugha. Hususan ilibainika kuwa, ambapo kujitambulisha na kundi- kabila kunaweza kuleta manufaa fulani kwa wahusika, athari huwa bayana. Kwa mfano kujitambulisha na kundi kabila la mwenye duka ili mwanafunzi apate turuhani. Ugunduzi huo unawiana sana na kauli ya nadharia ya kitendo kilichofikiwa kwamba, mtu hutathmini vitendo vyake kwa vigezo vya manufaa ya vitendo hivyo. Uteuzi wa lugha moja badala ya nyingine pia, hutawaliwa na mielekeo aliyonayo mtu kwa lugha hizo.

Mielekeo ya wanafunzi kwa lugha wanazozitumia ilibainika kuwa changamani. Lugha zilizoshirikishwa katika utafiti zilibainika kuwa zina maeneo mahususi ambamo zinatumiwa ugugunduzi uliobainisha kupendwa na hivyo kuteuliwa kwa lugha mbalimbali katika maeneo tofauti tofauti. Hivyo basi, sio rahisi kudai kwamba wanafunzi wana mieleko hasi au chanya kwa lugha bila kuzingatia eneo ambalo lugha inatumika. Hata hivyo, kwa ujumla, lugha ya Kiingereza ilibainika kupendwa na kutumika zaidi jambo ambalo linabainisha kwamba inateuliwa zaidi na wanafunzi ili waitumie.

Kuhusiana na kuwepo kwa uhusiano kati ya ukabila, mielekeo na ruwaza za matumizi ya lugha, matokeo ya utafiti huu yalibainisha kuwa, kuna uhusiano kati ya dhana hizo. Ilidhihirika kwamba, wanafunzi wanapowasiliana na wanafunzi wa kundi kabila lao nje ya darasa, wanatumia lugha asili na wanapokuwa katika vyumba vya kulala. Matokeo haya yanalingana na tafiti za awali ambapo muktadha huu waweza kulinganishwa na muktadha wa nyumbani ambao tafiti hizo zilichunguza. Huu ni muktadha ambao kwa kirefu huakisi jamii sawa kwa misingi ya kikabila. Basi, inakuwa mwafaka kutumia lugha asili na pia kuitumia kama utambulisho wao. Lugha ya Kiingereza ilibainika kuwa inayopendelewa sana na wanafunzi na kutumika katika misafara ya kwenda kuhudhuria mihadhara. Katokana na hali hiyo, ilibainika kuwa kuna uhusiano kati ya ukabila, mielekeo na ruwaza za matumizi ya lugha.

Bali na hayo, popote ambapo lugha ni kipimo muhimu cha utambulisho wa kundi kabila, kaida za kikundi zinaweza kuamua matumizi ya lugha ya kundi kabila. Imani na umahiri ambao umepatikana kupitia mitagusano hii ya kiethnoisimu ni kipatanishi cha kati cha tabia ya lugha ingawa uteuzi wa lugha unaweza kuathiriwa na vidokezi vya muktadha, mada na wahusika katika hali ya mawasiliano.

Juu ya hayo, uteuzi wa lugha katika mitagusano ya baina ya vikundi, huamuliwa kwa kiasi kikubwa na nguvu-tendi za kiethnoisimu za vikundi hivyo kuliko na dhana za kimuktadha za hali ya mawasiliano. Vidokezi vya muktadha vinaweza kuamua uteuzi wa lugha katika hali mahususi, lakini matumizi ya lugha huweza kuamuliwa pakubwa na mtagusano wa kibinafsi wa mtandao wa lugha ambao nao kwa upande wake, unaathiriwa na nguvu-tendi za kiethnoisimu za jamii husika.

Tofauti na tafiti za awali zilizotoa rai kuwa lugha asili zinafifia, utafiti huu ulidhihirisha kuwa lugha hizi zimekita mizizi vyuoni. Lugha hizi ni sehemu muhimu ya utambulisho wa wanafunzi hususan katika nyanda za utamaduni na asili yao. Aidha huwa ndizo lugha walizokumbana nazo mwanzo kabisa; hivyo, kuzitumia kuufasri ulimwengu uliowazunguka katika miaka ya mwanzo. Sio maeneo yote ambayo huhitaji matumizi ya lugha asili kutokana na tofauti za mpangilio wa wanafunzi na hata jamii nzima. Hata hivyo, ni muhimu kwamba lugha asili ziwe na wajibu wa kutekeleza aidha katika mpangilio wazi au fiche wa lugha.

Ilibainika kuwa wanafunzi wana mielekeo changamani kwa lugha wanazozitumia. Katika lile swali la moja kwa moja lililohusu kupendwa kwa lugha ya Kiingereza kuliko lugha asili na lugha ya Kiswahili, wengi wa wasailiwa (39%) walijibu kukubaliana na wazo hilo kabisa jambo lililoonyesha mielekeo hasi kwa lugha ya Kiswahili na lugha asili. Hata hivyo walipoulizwa kuhusu kujihisi kuwa huru kutumia lugha asili popote pale na wakati wowote ule, asilimia 32.9 ya wanafunzi walikubaliana na kauli hiyo ikilinganishwa na asilimia 23.3 ya wanafunzi waliokataa kauli hiyo.

5.4 Mafanikio na matatizo

Kwa upande wa matatizo, utafiti ulitekelezwa kwa wakati mahususi na kwa kutumia fedha za mtafiti ambazo zilikuwa haba. Dhana hizi mbili zilimbana mno mtafiti kwani ilikuwa inalazimu ahitimishe kazi yake kwa wakati ufaao. Pili kutokana na uchangamani wa ratiba ya vyuo vikuu, ilikuwa vigumu sana kuweza kutazama hali nyingi za matumizi ya lugha katika muktadha mahususi. Licha ya matatizo hayo madogo madogo, utafiti kwa kiasi kikubwa ulifanikiwa katika kutimiza madhumuni ya utafiti. Tasnifu imeeleza kwa tafsili matumizi ya lugha katika vyuo vikuu na kupambanua ruwaza za matumizi ya lugha vyuoni.

5.5 Mapendekezo

Ingawa nafasi za kazi zimezidi kuwa haba, zile zinazopatikana zinahitaji umahiri na umilisi mkubwa wa lugha ili kuweza kujieleza aidha kwa kuandika au kuzungumza. Kwa bahati mbaya, wanafunzi wanaohitimu kutoka vyuo vikuu hudaiwa kuwa na upungufu wa umilisi huu. Ingawa ukabila na mielekeo ya wanafunzi inaathiri uteuzi wa lugha, ruwaza za matumizi ya lugha zilibainika kusababisha ukosefu wa umilisi wa stadi za mawasiliano. Kwa mujibu huu, mapendekezo yafuatayo yalipendekezwa:

Kwanza, Idara ya Lugha na Isimu kwa udhamini wa chuo kikuu, inafaa ianzishe kozi ya msingi katika Kiswahili ili kuweza kukuza ustadi wa wanafunzi katika lugha hii. Pia, walimu hawana budi kujaribu kukuza na kudumisha mielekeo chanya kwa lugha zungumzwa. Hili lawezekana iwapo Idara ya Lugha na Isimu itachukua jukumu la kukuza utambuzi wa umuhimu wa kuweza kuwasiliana kwa ustadi katika lugha ya Kiswahili. Pili, ugunduzi kuwa, kuna ruwaza nyingi na changamani za matumizi ya lugha katika vyuo vikuu, inaelekeza kwamba wanafunzi hawazingatii lugha mahususi katika mawasiliano yao. Hivyo basi filosofia ya kukuza ustadi wa wanafunzi katika kuwasiliana ni daro kuu. Chuo kikuu kwa mujibu huu chafaa kuhimiza matumizi ya lugha mahususi. Kuna haja ya kukuza lugha aidha ni lugha rasmi au lugha ya taifa kwa kuwa na sera madhubuti. Chuo kikuu ni daraja moja katika kuwezesha ufanisi wa hali hii.

Zaidi, ni muhimu kuwa na vyombo vya habari vinavyojaliza na kushamirisha juhudi kama hizi. Lugha asili zinafaa kukuzwa kupitia taratibu makinifu katika vyombo hivi na kwa njia hiyo wema wa utamaduni utadumishwa na kukuzwa. Wanafunzi wanahitaji kuelewa historia yao ya kijamii, kitamaduni, kiuchumi na kisiasa ili kuweza kufahamu na kung'amua haja ya kutumia amali hii. Wajibu wa kila lugha katika kila jamii au na taifa unafaa kutambuliwa. Kila lugha ina mchango chanya katika utambuzi, ufundishaji wa maadili na ustawi wa wanafunzi. Wanafunzi watafurahia mchango chanya ambao utamaduni unaweza kutekeleza kupitia kwa lugha zao iwapo vyombo vya habari na taasisi za elimu kama vile chuo zitatoa nafasi kwa wanafunzi kujifunza lugha hizo.

Kwa jumla, nia kuu ya tasnifu hii ilikuwa kutambulisha jinsi ukabila na mieleko ya wanafunzi huathiri uteuzi wa lugha. Kwa kiasi kikubwa utafiti ulifanikiwa katika kuafikia lengo hilo. Hata hivyo, katika utafiti wowote ule unaohusiana na uteuzi wa lugha katika jamii za wingi lugha, mwanzo kabisa yafaa mtafiti afahamikiwe kwamba, uteuzi huu hauhusishi maamuzi ya kiholela kwa upande wa mzungumzi, lazima kuwe na ruwaza mahususi.

Uteuzi huu waweza kuwa wa hiari au usio wa hiari. Hata hivyo, kama ilivyobainika, uteuzi wa lugha haufanyiki katika obwe tupu. Hulazimu kwamba, kuwe na zaidi ya lugha moja. Kwa mintaarafu ya tasnifu hii, lugha asili, lugha ya Kiswahili na lugha ya Kiingereza ilihusishwa. Basi, namna moja ya kuangazia matumizi ya lugha katika jamii ni kwa kuyaangalia kwa misingi ya kufanya uteuzi. Mawasiliano ya binadamu huhusu kuteua miongoni mwa mkusanyiko wa lugha uliopo. Yaani kupendelea lugha fulani na kususia nyingine. Kufikia hapo, tasnifu hii inatoa rai kwamba, wingi lugha ni sifa kuu katika vyuo vikuu nchini Kenya. Wingi lugha huu huzuka na kuenea kutokana na kuwepo kwa wazungumzaji wa lugha tofauti katika eneo moja.

5.6 Mapendekezo ya maeneo ya utafiti zaidi

Kwa kugeza katika matokeo ya utafiti, mapendekezo yafuatayo yalitolewa kwa minajili ya utafiti zaidi;

- ✧ 1. Utafiti ulijikita katika kuchunguza matumizi ya lugha katika chuo kikuu cha Egerton- bewa la Njoro. Utafiti kama huu wafaa kufanywa katika chuo kikuu kingine hususan cha kibinafsi kuthibitisha matokeo ya utafiti ili kuweza kujumulisha na kufaa kwa vifaa vilivyotumiwa.
2. Ilibainika pia kuwa kuna kuchanganya lugha vyuoni. Hii ni dhana ambayo inafaa kuchunguzwa zaidi hasa kwa kulenga athari zake katika ukuaji na uendeleaji wa lugha.
3. Ilidhihirika kwamba uwezo wa kutumia lugha na mieleko ni dhana mbili zinazoingiliana na kuathiriana. Yafaa uhusiano huu na athari hii itafitiwe ili kubainisha ni ya kiwango kipi.

MAREJELEO

- Abdulaziz, M.H (1982). Patterns of Language Acquisition and Use in Kenya; Rural and urban Differences. – *Introduction to Language and community. International Journal on Language and Society.No. 34.*
- Ajzen, I. Na Fishben M. (1980). *Understanding Attitudes and Predicting Social behaviour.* New Jersey: Prentice-hall Inc.
- Angogo, R. (1980). Linguistic and Attitudinal Factors in the Maintenance of the Luyia Group Identity katika *Egerton Journal Vol IV, numbers 2 &3.* Njoro: Egerton University Press.
- Appel, R na Muysken P. (1987). *Language Contact and Bilingualism.* London: Edward Arnold Publishers.
- Beebe, L. M. na Giles, H. (1984). Speech Accommodation Theories: A Discussion in Terms of Second language Acquisition. *International Journal of the Sociology of Language No 46.*
- Blake L. na Lambert W. (1979). Student's view of English, Canadians, French Canadians tensions in Canada: *The influence of underson schooling.* Mimeo: Mcgill University.
- Carranza, M.A. (1982). Attitudinal research on Hispanic Varieties katika Ryan, E.B na Giles, H. (Wahariri): *Attitude towards Language Variation: Social and Applied Contexts.* London: Edward Arnold.
- Chai F. (1991). *Matumizi ya lugha mjini Malindi: Jinsi mielekeo inavyo athiri uteuzi wa lugha.* Tasinifu ya M.A: Kenyatta University.
- Chimerah, R.M. (1998). *Kiswahili Past, Present and Future Horizons.* Nairobi: Nairobi University Press.
- Clement, R., Gardener R. na Symth P.C. (1977). Motivation variables in second language acquisity. A study of francophone learning English katika: *Canadian journal of Behavioral Science.*
- Colony and Protectorate of Kenya (1949). African education in Kenya. *Report of Committee appointed to inquire into the Scope, Content, Methods and Administration of the African Education.*(Beecher Report) Nairobi: Government Printer.
- Crystal, D. (1994). *The University of Cambridge Language Encyclopaedia.* Madrid: Taurus.
- Evans, C. (1998) *Language people: The experience of teaching and learning modern languages in British Univeristy.* Startford: Open Univeristy Press.
- Edwards, R. J. (1977). Ethnic identity and Bilingual education katika Giles, H. (Mhariri): *Langage, ethnicity and intergroup relations.* London: Academic Press.

- Edwards, R. J. (1982). Language attitudes and their implication among English speakers katika E.B Ryan and H. Giles (Ed): *Attitudes toward language variation: Social and applied contexts*. Uk 20-33. London: Arnold.
- Edwards, R. J. (1985). *Language, Society and Identity*. Oxford: Basil Blackwell.
- Fishman, J. (1970). *Readings in the Sociology of Language*. The Hague: Mouton Publishers.
- Gardner, R.C na Lambert, W. E (1972). *Attitudes and Motivation in Second language Learning*. Mass: Newbury House, Rowley.
- Gardner, R. C. (1979). Social- Psychological aspects of Second Language Acquisition. In Giles, H. na St. Clair, R. N (Ed): *Language and Social Psychology*. Oxford Basil Blackwell.
- Giles, H. na Johnson, P. (1981). The Role of Language in Ethnic group Relations. In Turner, J. na Giles, H. (Ed): *Intergroup Behaviour*. Uk 199-243. Oxford: Blackwell.
- Giles, H. na Johnson, P. (1987). Ethnolinguistic identity theory: A social psychological approach to language maintenance. *International Journal of the Sociology of Language* 68 uk 69-91, 256-269.
- Giles, H. na P. Robinson (wahariri) (1990). *Handbook of Language and Social Psychology*. England: John Wiley and sons Limited.
- Gorman, T. P (1970). *Language in Education in Eastern Africa*. Nairobi: Oxford Univesity Press.
- Gorman, T. P (1974). The Development of Language Policy in Kenya with Particular Reference to the Educational System. In Whiteley, W. H. (Ed) *Language In Kenya*. Nairobi: Oxford University.
- Grojean, F. (1982). *Life with two languages: An Introduction to bilingualism*. Cambridge, Mass: Harvard University Press.
- Haarman, H. (1986). *Language in Ethnicity: A View of Basic Ecological Relations*. Berlin: DeGrugter.
- Harrison, G. J. na Piette, A. B. (1980) Young Bilingual Children's Language Selection, *Journal for Multilingual and Multicultural Development* 1 No 3.
- Hoffman, C. (1991). *An Introduction to Bilingualism*. New York. Longman Inc.
- Hutasoit M. na Prator C. (1965). *A study of the "New Primary Approach" in the schools of Kenya*. Ministry of Education & Ford Foundation.

- Kaniu, M. G. (2003). *Patterns of Language use and their effects on the Acquisition of English Oral Communication skills: A case study of secondary school students in Kandara division of Maragwa distict.* (Unpublished M.A Project Report): Egerton University.
- Kenya Institute of Education (KIE) (1992). *Secondary School Syllabuses.* (Volume five). Nairobi Kenya Literature Bureau.
- Kimemia, J. N (2001). *Kiswahili: The Dilemma of Developing a National Language.* Njoro: Egerton University Press.
- Kioko, A.N. & M. J. Muthwii (2001). The Demands of a Changing Society: English in Education in Kenya today. *Language, Culture and Curriculum*, Vol. 14. In <http://www.google.com>. Agosti 2005
- Lambert, W.E na Gardner, R. (1968). A study of the roles of Attitudes and Motivation in Second language learning. In Fishman, J.A (Ed) *Reading in the Sociology of language.* The Hague: Mouton Publishers.
- Lopez L. E. (2000). Cognition, culture, language and learning: An Introduction for Educational planners in Multilingual and Multicultural contexts. In *Distance Learning Course on the Language of Instruction in Basic Education.* (November 27, 28, 29, December 1, 2000.)
- Lowley, E. G. (1983). Ethnic activists view of the ethnic revival and its language consequences: An interview study of three American Ethnolinguistic minorities. *Journal of Multilingual and Multicultural Development* 163-179. Vol IV
- Lyons, J. (1968). *Introduction to Theoretical Linguistics.* London: Cambridge University Press.
- Makau, B.M. & Somerset H.C.A. (1980). *Primary School Leaving Examinations Basic Intellectual Skills and Equity: Some Evidence from Kenya.* A Discussion Paper No. 271. Institute of Development Studies: University of Nairobi.
- Martinelli, P. (1984). *Ethnicity in the Sunbelt: Italian American Migrants in Scottsdale, Arizona.* Unpublished PhD Dissertation. Arizona State University, Arizona in <http://www.google.com> Agosti 2005
- Marylin, J. (1998). *Investigations in Language Use in Kenya.* Nairobi: Nairobi University Press.
- Mathooko, P. M (2003). Language and Conflict Management in Multilingual Settings: The Role of Kiswahili in Kenya. *Katika Egerton Journal Vol IV, numbers 2 &3.* Njoro: Egerton University Press.
- Mercer, N. (1979). Linguistic and Cultural Affiliation amongst young Asian people in Leicester: *Language and Ethnic Relations.* Oxford: Oxford University Press.

- Mesthrie, R. (2001). *Concise Encyclopaedia of Sociolinguistics*. Oxford: Elsevier Science.
- Milon, J.P. (1992). Discourse in the primary English syllabus of Botswana. Katika Udo Bude (Mhariri). *Culture and Environment in Primary Education: The demands of the curriculum and the practice in schools in sub-Saharan Africa*. Bonn: Education, Science and documentation Centre. German Foundation for International Development.
- Milroy, L. (1987). *Observing and Analysing Natural Language*. Oxford: Blackwell.
- Ministry of Education (1976). Use of Language in Lower and Upper Primary. Circular Ref. INS/C/1/1 Vol.II/175. 48
- Mugambi, H. M. (2005) *Language Choice and Shift in Kenya: A look at the changing roles of Kiswahili and Indegenous Languages* katika <http://www.google.com> Agosti 2005
- Musau (2002). Polemics Versus reality: building the gap in Kiswahili research Katika Keneth Inyani (Mhariri) *Utafiti wa Kiswahili*. Nairobi: Moi University Press
Down town printing.
- Nader, L (1968). A Note on Attitude and the use of language. In Fishman, J.A. (Ed) *Reading in the sociology of language*. Pans mouton and company N.V publisher.
- The Nuffield Foundation and the Colonial Office (1953). African Education. *A Study of the Education Policy and Practice in British Tropical Africa*. (Chairperson A.L. Binns). London: Oxford University Press.
- Obura, A. (1996). Languages in Conflict in Anglophone Africa. (Unpublished PhD Thesi. Bonn: Nelde University.
- Ogodo, O. (2004). Teaching of Kiswahili in Universities Wanting. *EastAfrican Standard*, Saturday, January 24th 2004.
- Onyango J.O. (1990). *Mielekeo ya Wasomi kuhusu Matumizi ya Lugha ya Kiswahili nchini Kenya*. Tasnifu M.A: Chuo Kikuu cha Kenyatta.
- Philip M. S. (1997). *Language Social Psychological Perspectives*. New York: New York Pergamon press.
- Platt, J. (1980). The *Lingua Franca* of Singapore: An Investigation into State views of Inter-ethnic Communication. In Giles, H. na Robinson, W. P. na Smith, P.M. (Ed). *Language: Social psychological perspectives*. Uk 171-177. Oxford: Pergamon.
- Kenya, Republic of (1976). *Report of the National Committee on Educational Objectives and Policies*. (Chairperson: Peter Gachathi.) Nairobi: Government Printer.

- Ryan, E. B. Giles, H. na Sebastian, R. J. (1982). An Intergrative Perspective for the Study of Attitudes towards Language variation. In Ryan, E. B. na Giles, H. (Ed) *Attitudes towards Language Variation: Social and Applied Contexts. Uk. 1-19*. London: Arnold Publishers.
- Schiffman, H. (1996). *Linguistic Culture and Language Politics*. London: Routledge.
- Schmied, J. (1991). *English in Africa: An Introduction*. New York: Longman.
- Sifuna, D.N. (1975). *Revolution in Primary Education: The New Approach in Kenya*. Nairobi: East Africa Literature Bureau.
- Sifuna, D.N. (1980). *Short Essays in Eeducation in Kenya*. Nairobi: Kenya Literature Bureau.
- Skutnabb-Kangas, T. (1984). *Bilingualism or not: Multilingual Matters*. United Kingdom: Clevedon.
- Stuart, O. (1991). *Attitudes and Opinions*. New Jersey: Prentice hall, Inc Eaglewood cliffs.
- Wardhaugh, R. (1992). *An Introduction to Sociolinguistics (2nd Edition)*. United Kingdom: Blackwell Publishers.
- Whiteley, W. H (Ed.) (1974). *Language Use in Kenya*. Nairobi: Oxford University Press.
- World Bank (1988). *Education in Sub-Saharan Africa: Policies of Adjustment, Revitalism and Expansion*. Washington D.C.

KIAMBATISHO A:

Hojaji kwa Wanafunzi:

Naazimu kupata habari za kweli kuhusu matumizi ya lugha mbalimbali chuoni.

Tafadhali jibu maswali yote kwa kujaza nafasi zilizoachwa au kwa kuchagua kati ya majibu uliyopewa kwa kuweka mviringo mbele ya jibu lako

MAANA YA VIFUPISHO (kwa maswali 18-21)

N.K – Nakubali kabisa

S – Sikubali

N – Nakubali

S.K – Sikubali Kabisa

S.U – Sina Uhakika

Habari za kibinafsi

Uana _____, Mwaka (Academic Year) _____

Kabila _____, Kitivo (Faculty) _____

Maswali kuhusu Lugha, Mielekeo na Matumizi ya Lugha.

1. Unazungumza lugha ngapi chuoni? _____
Tafadhali ziorodheshe _____

2. Kati ya lugha unazozitungumza ni ipi uko radhi (comfortable) nayo unapoitumia katika hali hizi?
(a) Kuzungumza _____, (c) Kusikiza _____
(b) Kuandika _____, (d) Kusoma _____
3. Tathmini jinsi unavyotumia lugha hizi ukizingatia vigezo hivi: i) *Vyema*, ii) *Vibaya*
(a) Lugha Asili (mother language) _____, (b) Kiswahili _____
(c) Kiingereza _____
4. Je watumia lugha ipi
(a) Wakati uko chumbani mwa kulala? _____
(b) Wakati uko chumba cha maakuli? _____
(c) Wakati uko misafara ya kuhudhuria mihadhara? _____
(d) wakati uko Uwanjani? _____

5. Unatumia lugha ipi kuandika barua kwa

(a) Rafiki zako _____?

(b) Wazazi wako _____?

6. Je unasikiza vipindi vya radio katika lugha zifuatazo kwa kipimo kipi?

(a) Kiingereza _____, (b) Kiswahili _____,

(c) Lugha mama _____

{Kipimo: (a) Sana (b) Wastani (c) Kidogo (d) Hasikilizi}

7. Je unasoma gazeti katika lugha hizi kwa kipimo kipi?

(a) Lugha mama _____, (b) Kiswahili _____

(c) Kiingereza _____

{Kipimo: (a) Hasomi (b) Wastani (c) Kidogo (d) sana}

8. Unapohudumiwa na muuzaji wa kabila lako ni mara ngapi unatumia

(a) Kiswahili _____

(b) Kiingereza _____ Kuwasiliana naye?

(c) Lugha mama _____

(i) Chache, (ii) Nyingi, (iii) Situmii

9. Je iwapo si wa kabila lako ni mara ngapi unatumia

(a) Kiswahili _____

(b) Kiingereza _____ Kuwasiliana naye?

(c) Lugha mama _____

(i) Chache, (ii) Nyingi, (iii) Situmii

10. Unachanganya lugha katika mazungumzo yako _____?

Kwa kiasi kipi _____?

{Kipimo: (a) Sana (b) Wastani (c) Kidogo (d) Sichanganyi}

11. Unapokuwa nje ya darasa pamwe na wanafunzi wenzako wa kabila lako unazungumza lugha ipi au zipi?

(a) Lugha asili (b) Kiswahili (c) Kiingereza

12. Unapokuwa nje ya darasa pamwe na wanafunzi wenzako wasio wa kabila lako unazungumza lugha ipi au zipi?

(a) Lugha asili (b) Kiswahili (c) Kiingereza

13. Unapohudhuria michezo ya kuigiza chuoni hua inawasilishwa katika lugha ipi?
(a) *Lugha asili* (b) *Kiswahili* (c) *Kiingereza*
14. Unapohudhuria dhifa za kijamii k.v 'Birthday parties, densi n,k unazungumza lugha ipi? (a) *Lugha asili* (b) *Kiswahili* (c) *Kiingereza*
15. Unapokutana na wakubwa au wahadhiri wa chuo wa kabila lako nje ya darasa huwa mnatumia lugha ipi? (a) *Lugha asili* (b) *Kiswahili* (c) *Kiingereza*
16. Toa maoni yako kuhusu lugha zote zinazotumika chuoni ukianzia na lugha unayoipenda na kuionea fahari sana hadi kwa lugha unayoipenda kidogo.

17. Lugha ya Kiswahili ifanywe lugha rasmi chuoni.

- (a) N.K (b) N (c) S.U (d) S (e) S.K

18. Lahaja ya Sheng' haitumiki chuoni.

- (a) N.K (b) N (c) S.U (d) S (e) S.K

19. Najihisi huru kutumia lugha asili popote pale chuoni na wakati wowote nipendao.

- (a) N.K (b) N (c) S.U (d) S (e) S.K

20. Lugha ya Kiingereza inapendwa zaidi ya lugha asili na lugha ya Kiswahili chuoni

- (a) N.K (b) N (c) S.U (d) S (e) S.K

Asante!

EGERTON UNIVERSITY LIBRARY